# Kimo Cha Mtu Mkamilifu

Jeffersonville, Indiana, USA

Oktoba 14, 1962A

1 Asante, Ndugu Neville. Bwana awabariki.

Ni vizuri kurudi maskani tena asubuhi ya leo. "Habari za asubuhi" za neema, kwenu nyote. Nami ninatumaini ya kwamba hii itakuwa ni siku kuu kwetu sote, katika U—Uwepo wa Bwana wetu. Na sasa nina somo asubuhi ya leo. Ninataka kuingia moja kwa moja kwenye somo hili, kwa maana ni… Nafikiri ni muhimu. Na ni ninii … Na kuufanya umati usifadhaike sana, mwajua, inawabidi kukaa muda mrefu, wengi wamesimama. Nitaingia moja kwa moja kwenye somo.

2 Na sasa, usiku wa leo, ninataka kuzungumza juu ya somo la *Kiongozi wa Maisha Yangu*. Nami ninatumaini ya kwamba wengi wanaoweza, watu wengi iwezekanavyo, watahudhuria wakati huo kwa ajili ya usiku wa leo. Hata hivyo, kama una kanisa lako mwenyewe, sisi tuna … bila shaka, tunataka uwe kwenye—kanisani mwako. Hilo ni jukumu lako kuwa pale, mahali ulipo wajibu wako, kuruhusu nuru yako iangaze.

Sasa, tunaendelea kutumaini ya kwamba, kila wakati mtakaporudi, tutakuwa na nafasi zaidi kidogo hapa. Lakini tunapata shida na jambo hilo, loo, kila mahali. Hiyo halmashauri ya wadhamini hapana shaka wamechimbua kila kitu. Nao wakipeleka mahali fulani, wataliidhinisha; kisha wanaipeleka kwingine, pia wanaikatalia. Na wanawarudishia, na wanaliidhinisha *hapa*, na kuirudisha. Loo, tumekuwa na wakati ulioje! Lakini, mnajua, Shetani daima ni mpinzani wa ukweli. Kumbuka tu, wewe daima uko sahihi kuhusu …

3 Nilikuwa nashangaa ulikuwa wapi, Anthony. Ninaona ulikutana na baba yako. Nami nikaangalia upande wa pili, huko kwenye wasikilizaji. Yeye alisema ulikuwa umeketi pale. Tunafurahi kuwa na wewe na baba yako hapa pamoja nasi, Ndugu Milano kutoka New York. Nikitumainia, nikienda nchi za ng'ambo wakati huu, nitapata nafasi nyingine, kutoka New York, huko nje mahali fulani, Bwana akipenda.

Na kwa hiyo tuna furaha sana kwa ajili ya kila mmoja wenu. Ni—ni sawa tu kwenu kuwa hapa.

Nasi tulikuwa na wakati mzuri sana jana usiku, ama angalau nilikuwa nao. Nilikuwa na … [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] "Na Isaya hekaluni." Na kwa hiyo wewe …

Na asubuhi ya leo, tunataka kuzungumza juu ya somo, ama kufundisha, hasa, tukiweza, "Kuijenga maskani hai; kuijenga ma—kuijenga maskani hai ya mahali pa kukaa Mungu aliye hai, Mtu mkamilifu; maskani iliyo hai ya Mungu aliye hai, ambapo Yeye anaishi." Na kama …

4 Ninafahamu ya kwamba wana baadhi ya huu uimbaji mzuri hapa. Sipati nafasi ya kuusikiliza. Na usiku wa leo, nitajaribu kuja hapa. Mke wangu ameniambia juu ya Ndugu mmoja Ungren, ninaamini ndilo jina lake, kutoka hu—huko Tennessee. Sasa, yeye alikuwa hapa jana usiku. Simwoni asubuhi ya leo, bali nadhani yuko hapa mahali fulani. Nami ningetaka kumsikia akiimba usiku wa leo, kama naweza, ya kwamba, Ama *Chini Kutoka Utukufuni Mwake*, ama *Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu*. Ningependa kuusikia huo. Ni wangapi wangetaka kumsikia Ndugu Ungren? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Loo, na—napenda uimbaji mzuri. Na Meda alisema alikuwa na namna fulani ya sauti ya kiume ya wastani. Na inanikumbusha juu ya Ndugu yetu Baxter; yeye ni mwimbaji, pia, kama sisi sote tunavyojua. Na Aliposhuka Kutoka Kwenye Utukufu Wake, ama Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu. Ninaamini nimeona alipo sasa, kule… Hilo litakuwa sawa, Ndugu Ungren, usiku wa leo, ukitaka, kama usipoondoka? Utakaa, ama utajaribu kukaa ungojee ibada ya usiku? Vema, ni—ni … Vema, usininii … Ninawaambia, vipi kuhusu jambo hili, kama sisi … Sitaki kusababisha msuguano wo wote kwa mtu ye yote. Lakini kwa nini isiwe, basi, tukiweza, katika wakati wa *Ile Mihuri Saba*, tutakapoihubiri hiyo, kama ungeweza kuja. Ningetaka kuunasa kwa kanda, unaona, ili kuupata, Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu, na, pia, *Aliposhuka Kutoka Kwenye Utukufu Wake*, wakati ule.

5 Loo, si ni jambo la ajabu kumtumikia Bwana? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Sijui ningefanya nini kama sikuwa Mkristo. …?… Ni vizuri sana kuwa Mkristo. Ninajisikia tu kama kuruka—ruka na kupiga mayowe, kwa sauti yangu yote. Kuwa Mkristo, wazia jambo hilo, yote yametiwa nanga katika Kristo!

Ninajua ninaita jina la mtu huyu vibaya kila wakati. Ama ni S.T. ama T.S, ama kitu kama hicho. Sumners, Ndugu Sumner. Yeye … Ninataka kumshukuru yeye na mke wake wa thamani. Nadhania kwamba alichukua kama, ilionekana kama, kama miezi sita, kupiga chapa hiki *Nyakati Saba za Kanisa*. Na sasa tuko nacho kimerudishwa hapa, kimepigwa chapa, ni tayari kwa kusahihishwa, na kufanywa kitabu, *Nyakati Saba za Kanisa*. Dada Sumner, popote ulipo, hakika utaturuhusu tulipe kwa ajili ya jambo hilo. Hicho, hicho kimekuwa na kazi kubwa sana. Kumbe, ni kinene *hivi*. Kingenichukua kama miezi sita kukipitia. licha ya kukitoa kwenye kanda, halafu kukigeuza na kuondoa marudio, na kukifanya kitabu. Tutakitayarisha na kukituma kwenye mtambo wa kuchapisha mara moja, kwa maana tunafikiri ni kitu ambacho watu wanapaswa kuwa nacho sasa hivi, nanyi mnaweza kukisoma kwa undani. Na Billy alikuwa tu akinionesha, nilipoingia kwa undani kule nyuma, dakika chache zilizopita, ya kwamba—ya kwamba—ya kwamba kilikuwa—kilikuwa kiko tayari sasa kwenda kwenye mtambo wa kuchapisha. Kwa hiyo, dada, maskani itakulipa kwa ajili ya jambo hilo. Sikutarajii kufanya hivyo bure. Na—na ama ama sisi … Kama

tukikipata kitabu hicho na itubidi kukiwekea bei, ama cho chote kile, tutakiwekea bei ambapo utapata kitu fulani kila kiuzwapo, cho chote kile. Hebu zungumza tu na halmashauri, halmashauri ya wadhamini, ama baadhi yao kule, nao watashughulikia jambo hilo kwa ajili yako. Bwana awabariki sana.

6 Maskini mzee Ndugu na Dada Kidd wanaoketi hapa, naam, chini ya mia moja, kidogo tu. Nami nilikutana naye muda mfupi uliopita, naye akasema, "Vema, huu labda utakuwa ndio wakati wangu wa mwisho kukuona, Ndugu Billy." Kasema, "Ninazeeka sana."

Nikasema, "Loo, jamani! Sitaki kukusikia ukisema jambo hilo. Wewe ni kama mama na baba mdogo." Tunawapenda Ndugu na Dada Kidd. Sisi, kila mmoja, tunawapenda. Na ni ninii tu …

Linanifanyia jambo fulani wakati ninapowaona wakiingia kanisani, na mke na mume wazee wa thamani namna hiyo. Na wazia tu, walikuwa wakihubiri Injili kabla sijazaliwa. Nami ni mzee. Hata hivyo, wazia tu, walikuwa wakihubiri kabla sijazaliwa. Nami niko hapa sasa, ninafikiri ninazeeka sana. Karibu nianze kufikiria niko tayari kuacha. Ninawaona Ndugu na Dada Kidd wakiingia, "Utukufu kwa Mungu! Haleluya!" Ninasema, "La, ninajisikia vizuri." Naam, bwana. Kuwaona, jinsi wanavyoweza, jinsi wanavyokutia moyo!

Ndipo unatambua ya kwamba, ni karibia umri wangu, mara mbili, halafu wangali wanasonga mbele katika huduma. Wamekuja hapa asubuhi hii na kuomba vitabu, kama wangeweza kuchukua vitabu na kuviuza. Walitaka kanda, kusudi waweze kutoka, wawavute watu kwa kucheza kanda hizi, kwenye umri wa karibu miaka mia moja. Sasa yako wapi "mabawa yako mawili" tuliyokuwa tukinena habari zake jana usiku? Naam. Nilianza kufikiria juu ya, "Yako wapi yangu?" wakati aliposema hivyo—hivyo jana. Una umri gani, Dada Kidd? [Dada Kidd anasema, "Mimi nina themanini na moja." — Mh.] Themanini na moja. Una umri gani, Ndugu Tom? [Ndugu Kidd anasema, "Themanini na mbili."] Miaka themanini na moja na themanini na miwili, na wangali wakitumia mabawa yao, katika matendo, wangali wanaendelea.

7 Jambo lo lote likiharibika Ohio, ambalo Dada Kidd ana habari zake, simu inapigwa nyumbani. Hivi majuzi, alipiga simu, na mtoto mchanga, mtoto mchanga, mtoto mchanga wa kike, ninaamini ilikuwa hivyo, alizaliwa, na matumbo yakiwa yako nje. [Dada Kidd anasema, "Kibofu." — Mh.] Kibofu, upande wa nje wa mtoto mchanga. Naye daktari hakujua la kufanya kuhusu hilo, naye aliogopa kumfanyia upasuaji. Tuliomba. ["Walimfanyia upasuaji, Ndugu Branham, na kukirudisha, kwa sababu, wao walisema, 'Asingeweza kuishi.' Nao walirudisha matumbo yake ndani."] Wakarudisha matumbo ndani, kwa upasuaji, nao wakadhani asingeweza kuishi. Naye aliishi. ["Hakuna njia."] Hakuna njia kwa hiyo—kwa ninii…kutoka kwenye kikundu, kwa chakula kupitia. Ndipo Dada Kidd akapiga simu tena. Tuliomba tena, na sasa ana njia ya kawaida. Na huyu hapa, kama shahidi; daktari, pia. Mnaona? Ni ushuhuda ya kwamba Bwana Yesu, Ndiye Muumba mkuu! Mnaona yale Shetani alijaribu kufanya? Kuyafupisha maisha ya mtoto huyo. Na halafu basi, mnaona, halafu ninaamini huyo bibi alikuja kwa Bwana. ["Alirudi kwa Bwana, pale pale nyumbani kwangu."] Alimrudia Bwana. Dada Kidd alimwongoza kurudi kwa Kristo, baada ya muujiza huu mkuu kutukia kwa mtoto wake mchanga.

8 Nilipata simu kutoka California, jana, ndugu mhudumu mpendwa kule, niliyekuwa naye wakati nilipoenda California kwa mara ya kwanza, miaka mingi iliyopita. Maskini mjukuu wake alizaliwa akiwa—akiwa na ninii nne…vilango vinne vimeziba ndani ya moyo wake. Nami nikamwambia kuhusu jambo hilo. Nikasema, "Mungu ambaye aliweza kumuumba huyu mwingine na kumfanya mzima, bila shaka anaweza kumponya mjukuu wako." Mwambie tu mvulana huyo awe na ujasiri.

Na mvulana huyo alikuwa mkutanoni wakati nilipokuwa California kwa mara ya kwanza, yapata miaka kumi na minane iliyopita sasa, miaka kumi na sita iliyopita, imekuwa hivyo. Nami nilikuwa huko California. Naye … Mkutano ulimshawishi sana mvulana huyo mpaka … Wakati ule walipompata huyo mtoto mchanga, naye alikuwa amezaliwa, nao wakaona kulikuwa na kasoro, alikuwa bluu, nao wakajaribu kumtia oksijeni, na kadhalika. Na hakuonekana kana kwamba angeishi, nao madaktari basi wakamfanyia uchunguzi, wakapata kwamba vilango vitatu vilikuwa vimeziba ndani ya moyo wake. Hakuna mlango kabisa, mnaona, ni—ni kilango kimoja tu kinasukuma. Ndipo akamwita baba yake, na kusema, "Baba, mwite Ndugu Branham, mara moja. Mwambie ya kwamba yote … 'Na amwombe Kristo tu. Yeye atafanya hivyo.'" Hivyo ndivyo ilivyo. Loo, jamani! Ushawishi huo, yale wanayoona, mnaona, tuliyazungumzia, jana usiku. Jambo sahihi kwa wakati unaofaa.

9 Vema, tukiendelea kuzungumza, kamwe hatutafikia lile somo, sivyo? Ni kama tu sukari guru kwenye asubuhi yenye baridi, ni nzito sana iwezavyo kuwa, mwajua, na yote inashikana. Tuna furaha sana kuwa na ushirika kama huo. Naam, bwana.

Kwa hiyo sasa hebu na tunyamaze, sasa, na tufikie somo sasa. Huenda labda … Sijui kama mnaweza kuona jambo hilo au hamwezi, ubaoni. Labda kama nikiugeuza namna *hiyo*, kwa dakika chache, mbona, tutaweza, sasa, baadhi yenu, kuninii… [Ndugu Edgar "Doc" Branham anasema, "Unataka mahali fulani?" — Mh.] Unasemaje? [Je! unataka umulikiwe mwanga?"] La, sidhani hivyo, sasa hivi, Doc. Labda tu katika muda kidogo. ["Moja kwa moja sakafuni, ninaweza kuweka alama juu yake."] Vema, tu—tutafanya hivyo nitakapopata ninii chache… Una kurunzi hapa? Vema. Hebu tuumulikie tu moja kwa moja. Mnaweza kuona huko nyuma kabisa? Mnaweza? Kama unaweza kuona, inua mkono wako, kama unaweza kuona huo ubao,

kusoma hayo juu yake. La. Vema. Pata mahali hapo. Sasa, wakati wanapojitayarisha kufanya hivyo…

10 Ninaanza nikiwa nimechelewa asubuhi ya leo; ama, la, la, kama dakika kumi na tano mapema. Na kwa hiyo, basi, tutachukua wakati wetu sasa, kwa sababu hatutaki kuharakisha. Unapofanya haraka, basi unaharibu tu mambo uliyokuwa ukitaka kusema. Sasa, nilikuwa nikisikiliza kanda, hivi majuzi, kama nilivyowaambia, nami nikajionea aibu sana; si yale niliyokuwa nikisema, bali jinsi nilivyokuwa nikiyasema upesi sana, na ni wasiwasi tu. Ninajisikia kama kungojea. Ni …

11 Ni—niliona tu hivi majuzi ambapo walikuwa wakienda kujenga bustani kubwa ya wanyama, hapa katikati ya Louisville. Naye Bw. Brown, naamini ilikuwa ndiye, kule, alitoa dola millioni moja kwa ajili ya hifadhi hiyo. Vema, kama ningelikuwa nazo, takribani ningewapa hizo kusudi wawaachilie hao wanyama. Si—siamini katika kufungia kitu cho chote kizimbani namna hiyo. Ninaninii tu … Ninaenda kwenye hizo hifadhi na kuwaona maskini hao wanyama duni, dubu, na simba, na kadhalika, wakienda huku na huko, wamefungwa kifungo cha maisha, unaona. Inakufanya ujisikie vibaya. Inakufanya ujisikie vibaya. Hata hivyo, wanashikwa na akili za mtu aliye na akili kuliko wao. Mnaona? Nao wanawakamata na kuwaweka kifungoni.

Nami ninafikiri juu ya Ibilisi kufanya jambo hilo. Anachukua watu wa thamani ambao wanapaswa kwenda kwenye majumba makuu ya Mungu, na mashamba, na—na mambo kama hayo, kisha wanamfunga kwenye magereza ya madhehebu fulani, ama baadhi ya kanuni za imani, ama cho chote kile, na kuwafungia huko. Na ni jambo la kuchukiza jinsi gani.

Na mimi sipendi hifadhi za wanyama. Lakini ninajisikia kitu kama mmoja wa wanyama hao, wakati umefungiwa tunduni kabisa na unajaribu kuwa huru, unajua, ku—kutoka ufanye jambo fulani.

12 Sasa, kabla hatujaliendea Neno, hebu na tumwendee Mwandishi wa Neno, tunapoinamisha vichwa vyetu sasa katika maombi.

Baba yetu wa Mbinguni mwenye neema, tumekusanyika asubuhi ya leo tena katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao wa thamani. Mungu, aliyefanyika mwili, alikuja duniani, kwa ajili ya upatanisho wa dhambi zetu, na akafa, Mwenye Haki; kusudi sisi, kwa haki Yake, tukiwa wasio haki tupate kufanywa wakamilifu katika Yeye. Tunakuja tukikiri ya kwamba hatustahili, Bwana. Hakuna kitu kizuri kwetu. Nasi sote tuko katika jela moja kubwa. Haidhuru tunasimama kwenye kona gani, tungali tuko gerezani. Mmoja asingeweza kumsaidia mwingine. Lakini, Mungu, katika rehema Yake isiyo na kikomo, alishuka na kufungua milango ya gereza, kutuweka huru. Hatujafungiwa tena kizimbani sasa. Hatuko katika hifadhi ya wanyama ya ulimwengu, bali sasa tuko huru. Tuko nje.

13 Loo, jinsi tunavyompenda na kumwabudu! Jinsi tunavyoweza kutembea kupitia katika mashamba makubwa ya ahadi Yake, na kuziona zikidhihirishwa mbele zetu! Na kwa macho yetu wenyewe, tuone yule Mungu mkuu wa Milele akijifunua Mwenyewe mbele zetu, na kujidhihirisha, kama alivyofanya kwa wale manabii wa kale. Tukijua jambo hili, ya kwamba wao wamepumzika na uhakika, ya kwamba siku moja tutarudishwa tena, baada ya maisha haya kwisha, na ufufuo, kwa Uzima wa Milele ambao hautakufa kamwe. Miili yetu haitazeeka. Nasi kamwe hatutakufa. Na hatutakuwa na njaa kamwe. Na kamwe hatutakuwa na uhitaji. Bali tutatembea pamoja Naye. Tunataka kumsikia Yeye akisema, "Ingieni katika raha ya Bwana, mliyoandaliwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Kule nyuma kabla ya dhambi kuingia, jinsi alivyokwisha fanya matayarisho, kama yale yaliyokuwa kwa ajili ya Adamu na Hawa, ya kwamba wasingekuwa wagonjwa wala kupata shida. Na sasa Yeye alitutayarishia hilo, Naye alitangulia kujua ya kwamba tunakuja. Dhambi ilifanya kizuizi kikuu, na sasa dhambi imeondolewa, kwa Damu ya Yesu. Sasa, tunaelekea kwenye Nchi ya ahadi, kwa ahadi ya Mungu, ambayo ni ya Milele.

14 Tubariki sasa, Baba, tunapojifunza Neno Lako. Tunataka kujua tunapaswa kuwa watu wa namna gani, kusudi tuwe kule. Tusaidie leo katika shule hii, tupate kuwa na Mwalimu Mkuu mkuu pamoja nasi, Roho Mtakatifu, ambaye angeshuka na kujifunua Mwenyewe kwetu, kwa Neno Lake. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

15 Sasa, kwanza, ningetaka mfungue pamoja nami katika Petro wa Pili, mlango wa 1. Ninataka kusoma sehemu ya Maandiko haya, Petro wa Pili, mlango wa 1. Na sasa kwenu ninyi mlio na penseli zenu na karatasi …

Nami ninaamini niliambiwa asubuhi ya leo ya kwamba—ya kwamba mara nyingi, ninapogeuza kichwa changu kutoka pale, jambo hilo linapunguza sauti ya kanda. Kwa kweli simaanishi kufanya hivyo. Nami ninaamini, mara nyingi, kama tungefikiria juu ya kupata ma—maikrofoni ya wavuti, na kuining'iniza kwenye dari hapa. Haidhuru ungekuwa wapi wakati huo, ungekuwa sahihi. Ingekuwa ni kamilifu, kila mahali tu, maikrofoni tu juu ya dari.

16 Na sasa, wakati nikizungumza; na endapo ninyi, baada ya ibada, ama mkitaka, mnaweza mfutilie mbali mchoro huu hapa. Halafu pia nikauchapishe hapa. Nitachukua kipini na kuubandika hapa mbele, kama mngetaka kufanya jambo hilo wakati mwingine. Njooni mapema kidogo alasiri ya leo, tupate

kufahamu.

17 Sasa tunaikaribia ile *Mihuri Saba*. Tumemaliza tu *Nyakati Saba za Kanisa*. Na huu ni Ujumbe wa mafundisho, unaomwingiza mtu ndani, atakayekombolewa kwa Damu ya Bwana Yesu, na atakayekuwa katika wakati ule wa Kanisa, ule wakati wa Milele wa Kanisa mwishoni mwa ile Mihuri. Sasa tunajua ya kwamba tuna Baragumu Saba, Mapigo Saba, Vitasa, na kadhalika, tunavyoendea, tunapoendelea. Lakini tunangojea nafasi zaidi ili watu waweze kuketi.

Nami nilifikiri hili lingeshikamana mahali tu ambapo nilikuwa nikitarajia. Sikutarajia kuchora mchoro huu, lakini hivi majuzi nilikuwa na marafiki zangu wapendwa, akina Cox, huko Kentucky. Nilienda huko, nikafikiri labda nitapata siku moja zaidi ya kuwinda kindi kabla msimu wake haujakwisha. Nami nilikuwa huko mwituni pamoja na rafiki yangu, Charlie, tukisimama pale, na Rodney, ndugu yake. Hata sikuona kindi. Nafikiri niliwatisha wote, nilipopiga makelele kule mwituni. Hili ndilo lililonijia, jamani, na—na Dada Nellie na Margie, na nilipowaambia ningewaambia Jumapili nitakapolifundisha. Hilo ndilo lililonijia mimi, juu ya ujumbe niliokuwa nihubiri. Na jinsi hayo mengine yalivyoingiana moja kwa moja ndani yake! Na, loo, ninapenda jambo hilo. Nilikuwa na roho ha—halisi—halisi ya kupaza sauti, huko mwituni.

18 Kwa hiyo sasa, hebu na tusome sasa, Petro wa Kwanza, ama … Petro wa Pili, hasa, sura ya 1, sehemu Yake.

> *Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika haki ya Mungu wetu, na Mwokozi wetu Yesu Kristo.*

Ninapenda jinsi hilo limesemwa hapo kabisa, kwa maana somo langu lote asubuhi ya leo limewekwa msingi juu ya imani. Mnaona? Hebu nisome hilo tena. Sikilizeni kwa makini.

> *Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale* wanaopata—*waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika haki ya Mungu wetu,…na Mwokozi wetu Yesu Kristo.*

Angalieni, Yeye anasema, ya kwamba, "Nimepokea imani hii, nami ninawaandikia haya hao waliopata imani moja na sisi yenye thamani." Ninataka … Si kwa ulimwengu wa nje. Hili ni kwa ajili ya Kanisa, mnaona, wale walio katika Kristo.

> *Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na* (kwa) *Yesu Bwana wetu.*
>
> *Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote…uweza wake wa Uungu sasa umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima…utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe:*
>
> *Tena kwa hayo ametukirimia…ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo* (ahadi hizi) *tupate kuwa washirika wa tabia ya Uungu…*

19 Sasa hebu hilo na lipenye ndani sana sasa. Si kuhubiri asubuhi ya leo; tunafundisha tu somo hili. "Tabia ya Kiungu." Hebu nisome kifungu hicho cha 4 tena sasa, ili kwamba msilikose. "Kwa hiyo tumepewa …"

> *Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo* (ahadi hizi) *tupate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.*

Mnaona, "ulimwengu," tumeponyoka hayo sasa. Yeye analiandikia Kanisa jambo hili. Hiyo ndiyo sababu tuko hapa asubuhi ya leo, ni kutaka kujua kwamba njia ni ipi, kwamba masharti ya Mungu ni yapi. Hakuna mtu hapa ndani, anayempenda Mungu, ila yule anayetaka—anayetaka kuwa, anayetaka kufanana zaidi na Kristo. Sasa imewekwa hapa. Kila Mkristo! Mimi ni mzee mkongwe. Waangalie Ndugu na Dada Kidd hapa, labda wao ndio wazee kuliko wote jengoni. Lakini kama ningaliwauliza, "Shauku ya moyo wenu ni nini?" Ingekuwa, "Kuwa karibu na Mungu zaidi." Unapojifunza juu ya Kristo, kuna kitu fulani kumhusu Yeye ambacho ni cha upendo sana, unajaribu tu kuingia ndani Yake.

20 Samahani kwa tamshi hili. Nilimwambia mke wangu, hapa si muda mrefu uliopita, yeye…sote wawili tunazeeka, nami nilimwambia, nilisema, "Je! unanipenda kama ulivyokuwa ukinipenda?"

Akasema, "Kwa kweli nakupenda."

Nami nikasema, "Unajua, ninakupenda mno mpaka ningetaka kukuchukua na kukuvuta nikuingize ndani yangu, kusudi tupate kuwa, kwa kweli, tuwe mmoja, zaidi."

Sasa, huo, zidisha huo kwa milioni mia moja, ndipo utaona jinsi ambavyo mwamini, ambaye anampenda Kristo, anavyotaka kuingia ndani Yake, kwa sababu ni upendo. Na hapa Yeye atatuonesha jinsi ambavyo, kupitia katika ahadi hizi, tunaweza kuwa washirika wa tabia ya Uungu wa Kristo. Hii, miili

inayopatikana na mauti, jinsi ambavyo tunaweza kuwa washirika,

21 Huenda nikasema jambo fulani hapa. Sababu ya mimi kuamini … Sasa mtu fulani amenikosea kabisa, hapa si muda mrefu uliopita. Nilipata barua kutoka kwa shirika la wahudumu, ambayo ilisema ya kwamba mimi niliamini kulikuwa na… "Tuliunganishwa kinafsi. Na lazima tuwaache wenzi wetu kama hatujaunganishwa kinafsi nao, tukaoe mwingine ambaye tumeunganishwa kinafsi naye." Loo, jamani!

Nikasema, "Sina hatia ya uzushi kama huo." Daima nimekuwa nikipinga jambo hilo. Si—siamini katika hilo. Hakika siamini. Ninaamini ya kwamba Mungu hutupa mwenzi. Hiyo ni kweli. Na ndipo tunakuwa sehemu ya mmoja kwa mwingine. Hiyo ni kweli. Na kabla ya mwanamume kuoa, anapaswa kufikiria mambo haya vizuri, ayaangalie kwa makini.

22 Kijana mmoja aliniuliza hivi majuzi, akasema, "Unafikiri ningeweza, ninapaswa kuoa, Ndugu Branham, mshichana *fulani*?

Nikasema, "Unafikiri unampenda kiasi gani?"

Akasema, "Loo, jamani, ninampenda tu."

Nikasema, "Vema, kama hutaishi bila yeye, afadhali umwoe basi. Lakini kama unaweza kuishi bila ya yeye, afadhali usimuoe. Kwa hiyo, bali kama jambo hilo litakuua, afadhali—afadhali uchukue hatua umwoe," nikasema. Na kwa hiyo jambo nililokuwa nikijaribu kumwambia, ni hili, ya kwamba, kama unampenda sana.

Sasa, sasa hivi, kabla hujafunga ndoa, kila kitu ni sawa na ni kizuri sana. Lakini baada ya kufunga ndoa, basi taabu na majaribu ya maisha yanaingia. Hapo ndipo huna budi kuwa na upendo sana hivi kwamba mnaelewana. Akikuvunja moyo, nawe ukamvunja moyo, mngali mnaelewana.

23 Hivyo ndivyo ilivyo na Kristo. Mnaona? Hatuna budi kupendana Naye sana, mpaka wakati tunapomwomba jambo fulani, Naye hatupi, hilo halitutikisi kamwe. Mnaona? Mnaona? Kwa nini? Na njia pekee unayoweza kufanya jambo hilo, ni kuwa mshiriki wa tabia Yake ya Kiungu, ndipo utafahamu ni kwa nini Yeye hawezi kukupa ulilomwomba. "Washiriki wa tabia Yake ya Kiungu."

Na hebu angalia hapa, "Baada ya kuokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa." Mmeokolewa nao! Mnaona imeandikiwa akina nani? Ni kwa Kanisa, hao walio katika Kristo, wameinuliwa juu ya mambo haya. Si eti yeye amejiinua, bali Kristo alimwinua.

24 Kwa ndugu zangu na dada zangu weusi waliopo asubuhi ya leo, sisemi jambo hili ili kuwaudhi. Lakini, nilikuwa mkutanoni wakati fulani uliopita, sijui kama niliwahi kusema jambo hilo maskanini. Nimelisimulia mahali pengi. Kulikuwa na dada mweusi aliyesema, "Je! naweza kutoa ushuhuda, ama nishuhudie?"

"Bila shaka, dada, endelea moja kwa moja."

Akasema, "Ninataka kutoa ushuhuda huu kwa utukufu wa Mungu." Akasema, "Mnajua, mi—mimi siko jinsi ninavyopaswa kuwa," kisha akasema, "si—siko jinsi ninavyotaka kuwa, bali," akasema, "kuna jambo moja la hakika, mimi siko nilivyokuwa." Mnaona? Alikuwa ametoka mahali fulani. Alikuwa ameinuliwa.

25 Hivyo ndivyo tunavyojua tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Tunaangalia nyuma kwenye shimo tulikokokotwa. Mnaona? Sisi hatuko vile tunavyotaka kuwa; hata hatuko vile tunavyopaswa kuwa; bali jambo moja tunaloshukuru kwa ajili yake, hatuko jinsi tulivyokuwa. Hiyo ni kweli. Tuko njiani.

26 "Na baada ya kuokolewa na uharibifu uliomo duniani." Baada ya kuokolewa na huo, tamaa na uharibifu wa duniani, wewe uko juu ya hayo. Sasa hiyo ni—sasa huyo ndiye mtu wa aina ambayo Yeye anazungumza naye, mtu ambaye ameokolewa na mambo haya, mnaona, uharibifu uliomo duniani.

*Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa,*

*Na katika maarifa yenu kiasi,…katika kiasi chenu saburi,…katika saburi yenu utauwa,*

*Na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo.*

27 Sasa Yeye ametupa muhtasari hapa wa yale tunayopaswa kufanya, kujua jinsi ya kufanya jambo hilo. Sasa, kama nilivyosema, sisi sote tunajaribu kumkaribia Mungu. Hiyo ndiyo sababu niliuchagua Ujumbe huu asubuhi ya leo, kwa ajili ya kanisa, nikijua ya kwamba watu wanasafiri. Kwa kuwa jana usiku, nilisema, "Ni wangapi walioko hapa, kutoka nje ya mji?" Yapata asilimia tisini na nane ya watu, kutoka nje ya mji. "Ni wangapi walio hapa kutoka maili mia moja?" Mbona, ilipita, nakisia, asilimia themanini. "Ni wangapi walio hapa kutoka zaidi ya maili mia tano?" Na takribani the—theluthi moja ya watu walikuwapo hapa kutoka zaidi ya maili mia moja, umbali wa maili mia tano. Wazia jambo hilo, ya watu wanaosafiri. Vema, watu hao hawaji kanisani namna hiyo wapate kuonekana tu. Hakuna…kama vile ulimwengu wa nje ungeona uzuri wo wote mahali hapa. Wote ni watu wa kawaida, maskini, watu waliovalia kawaida.

Hakuna nyimbo kuu za dini kutoka kwa kwaya fulani inayojifanya kwamba ni ya Kimalaika, vyombo vya filimbi, na baadhi ya madirisha yenye vioo vya picha za kuona. Mna wakati mgumu kupata mahali pa kuketi kwenye benchi na kusimama kwenye ukuta. Hawaji kwa ajili ya jambo kama hilo. Bali wanakuja kwa sababu ndani yao kuna kitu kinachoona uzuri ambao jicho la kawaida halioni. Ni jicho la Kiroho ndilo linaloona uzuri wa Kristo. Hiyo ndiyo sababu wanakuja.

28 Kwa hiyo, kwa siku kadha kabla hatujafanya ibada, mimi huomba bila kukoma. Huenda mwituni, ninachukua mfukoni mwangu… Ninamwambia mke wangu, "Ninatoka kwenda kuwinda kindi asubuhi ya leo." Nami ninaweka penseli na bunda la makaratasi la kuandikia mfukoni mwangu. Mara kunapopambazuka vya kutosha kuona, nimeketi nikiegemea mti mahali fulani, mikono hewani, na nikisema, "Bwana, nifanye nini leo? Utanipa nini kwa ajili ya watoto Wako?"

Ndipo ninapoguswa na jambo fulani ambalo linaonekana linachoma moyo, kunakuja kitu kama hiki. Wakati Uwepo Wake unapokaribia, ninaanza kusikia kitu fulani kana kwamba kiko huko mbali sana, kitu kama hiki. "Mbili mara mbili ni nne." Karibu zaidi, "Mbili mara mbili ni nne. Mara mbili mbili sawa na nne. Mbili mara mbili ni nne. [Ndugu Branham anazungumza kila na kurudia upesi kidogo — Mh.] Kuendelea, kuendelea, kuendelea, namna hiyo. Ni Uwepo Wake ukiingia.

29 Jinyenyekeze, na punde si punde unaachana na mwili wako. Ono linatokea, "Nenda mahali *fulani*, na jambo *fulani*." Mnaona? Inaanza, toka akili yako kumtafakari Mungu, unatoka katika ulimwenguni, mbali na ulimwengu, huko nje nyikani, uko peke yako mwenyewe.

Nayo inaanza kuja, "Moja, moja…" Ninatamka, namba yo yote, ama cho chote kile, kitu fulani tu kinaanza polepole, kinaingia kwa mnong'ono wa mbali. Halafu kinakuja haraka zaidi, haraka zaidi. Unaketi pale na kuinua mikono yako, usiseme neno, inua tu mikono yako hewani. Muda si muda unajua, utu wako wote unatwaliwa. Ndipo unaona mambo anayokutaka ujue, anakuonesha mambo yajayo.

Mara nyingi inafikia mahali, mpaka mahali fulani, kisha inakoma. Haiingii kwenye ono. Ndipo Maandiko yanamiminika pamoja. [Ndugu Branham anadata kidole chake mara tatu — Mh.] Ninanyakua penseli yangu, nisije nikasahau, na kuandika, ninaandika.

Ndipo ninakuja nyumbani na kuangalia tena, na kulisoma. Na mara nyingi hata halileti maana kwangu ninapoliangalia tena. Halafu basi, punde si punde, hili hapa! Hilo linashuka kwa kasi, na hiloo linaondoka tena. Ndipo ninachukua kitabu kidogo namna *hii*, na kuanza tu kuandika, upesi tu niwezavyo, yale Yeye anayoniambia. Nikawaza, "Bwana, ninashuka kwenda maskanini na kuwaambia. Mimi … 'Mje huku.' Nina jambo fulani kwa ajili yao." Vema, hivyo ndivyo linavyokuja. Hiyo ni kweli kabisa. Mpaka, kwanza, Yeye anipe, siwezi kulitoa.

Kwa hiyo, basi, kutokana na michoro hii midogo ambayo mnaniona nikiangalia. Na jambo hili, kwanza, nilianza. Sikupata sehemu hii hapa mpaka yapata siku moja ama mbili zilizopita, huko mwituni.

30 Sasa, watu hawa ni—ni … Petro anasema, hapa, jinsi ambavyo hatuna budi kuwa washiriki wa tabia Yake ya Uungu. Sasa, kila mmoja wetu anajaribu kukua kufikia kimo cha Mungu.

Sasa, baada ya sisi kumaliza ile Mihuri Saba, basi, kwenye wakati huo wa kutangazwa kwa ule Muhuri wa Saba, ama kufunguliwa… Bila shaka, tunajua muhuri ni kitu gani, ni kufungulia huduma, kufungulia Mihuri Saba. Nasi tutaona jambo hilo papa hapa kwenye mchoro huu. Ni kufunguliwa kwa Ujumbe fulani, kitu ambacho kimetiwa muhuri.

31 Jumapili iliyopita usiku, nilihubiri juu ya, "Ufunguo." Na ufunguo ni imani. Imani inashikilia ufunguo, na ufunguo ni Maandiko. Naye Kristo ndiye Mlango. Mnaona? Kwa hiyo imani inachukua hizo kanuni ndogo za Maandiko na kufungua utukufu na wema wa Mungu, kuwapa watu Wake. Mnaona? Kwa hiyo, ni, imani inashikilia ufunguo unaomfungulia Kristo kwa watu; inaufungua, inaufunua.

Kwa hiyo, leo, tutajaribu kuchukua ufunguo ule ule, tupate kufungua njia ya kufanyika Mkristo mwema katika kimo cha Mungu, huyo, na kuwa maskani iliyo hai ambamo Mungu aliye hai ataishi.

Kumbuka, Mungu hujifunua Mwenyewe katika njia tatu. Mara ya kwanza, Yeye alijifunua Mwenyewe katika Nguzo ya Moto, ambayo iliitwa Ubaba. Ndipo Mungu huyo huyo, aliyedhihirishwa katika Yesu Kristo, ambaye aliujenga mwili, akaufanya mwili huu. Tatu, kupitia mauti ya mwili huo, Yeye alitakasa Kanisa ambalo anaweza kuishi ndani yake. Ilikuwa ni Mungu juu yetu; Mungu pamoja nasi; Mungu ndani yetu; Mungu yeye yule.

32 Hiyo ndiyo sababu iliitwa Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Si Miungu watatu; ofisi tatu za Mungu mmoja. Wangewazia tu jambo hilo kwenye Baraza la Nikea, tusingechanganyikiwa kabisa, sivyo? Hiyo ni kweli. Si miungu watatu. Watu hawakuweza kufahamu jinsi Yesu alivyonena na Baba, na Yeye na Baba ni Mmoja. Vema, jambo lote liko hapo. Hakika, hulifunua tu. Hakika. Mnaona? Si Miungu watatu. Ofisi tatu! Ninii tatu- …

Ni kitu gani? Mungu akijidhili kwa viumbe Vyake. Mungu anataka kuabudiwa. Neno *Mungu* linamaanisha "kitu cha kuabudiwa." Na ni Mungu akijaribu kuwazoeza watu Wake, kusudi aweze kupata kutoka kwao kile alichowaumbia. Yeye hakukuumba kamwe kuwa kitu kingine mbali na mwana na binti wa Mungu. Kama umekosa jambo hilo, la kuwa mwana na binti wa Mungu, umekosa shabaha.

Na "kukosa," neno *d-h-a-m-b-i* maana yake ni "kukosa shabaha," kukosa shabaha. Basi, kama ninalenga shabaha, kulenga shabaha kwenye yadi hamsini, nami ninalenga; nichukue bunduki yangu na kulenga shabaha, na niikose, inchi nne ama tano, ni kitu gani kimetukia? Bunduki yangu inahitaji kurekebishwa. Kuna kasoro. Na kama nikikosa imani katika Mungu, kama nikikosa kuwa Mkristo … Mungu alikuweka hapa uwe Mkristo. Kama ukienda kando upande mmoja, rudi ukajirekebishe. Na kuna kitu kimoja tu kinachoweza kukurekebisha, hicho ni Maandiko. Roho Mtakatifu katika Maandiko, anakusahihisha, anakuleta moja kwa moja kwenye shabaha tena. Hiyo ni kweli.

33 Sasa, tutajifunza Neno Lake. Stefano alisema, katika Matendo 7, na pia katika … Hebu na tusome tu jambo hilo. (Tukizungumza sasa, tunazungumza juu ya Maskani ya Mungu.) Sasa, Stefano alisema … (Kwa kuwa, itakuwa ni Maskani iliyo hai ya Mungu aliye hai.) Stefano alisema, katika Matendo sura ya 7, nami naamini sisi … katika Matendo 7, kuanzia kwenye kifungu cha 44:

> *Ile hema ya ushahidi ilikuwa pamoja na baba zetu jangwani, kama alivyoagiza yeye aliyesema na Musa, ya kwamba aifanye sawasawa na mfano ule aliouona;*
>
> *Ambayo walikuwa nayo baba zetu, kwa kupokezana, wakaingia pamoja na Yesu katika milki ya Mataifa wale, ambao Mungu aliwafukuza mbele ya baba zetu, mpaka siku za Daudi;*
>
> *Aliyepata fadhili mbele za Mungu, naye aliomba ampatie Mungu wa Yakobo maskani.*
>
> *Lakini Sulemani alimjengea nyumba.*
>
> *Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, kama vile asemavyo nabii,*
>
> *Mbingu ni kiti changu cha enzi, na nchi ni pa kuwekea miguu yangu; ni nyumba gani mtakayonijengea? Asema Bwana, au ni mahali gani nitakapostarehe?*

34 Sasa katika … Sasa, "hema," ni, bila shaka, mahali ambapo tunaenda kustarehe, sasa, kuburudika, na kadhalika, kama vile kupumzika kutokana na usingizi, ama kadhalika. Sasa, Waebrania 10, na kifungu cha 5, Paulo anaingiza jambo hilo.

> *Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, asema, Dhabihu*…(Huyo ni Kristo.)…*Dhabihu na toleo hukutaka, lakini mwili uliniwekea tayari.*

Maskani ni nini sasa? Mwili, Mungu akifanya hema katika Mwili.

Mungu wakati mmoja, huko juu, wakati aliposhuka mlimani, hata kama fa—fahali ama ng'ombe angaliugusa ule mlima, hana budi kuuawa. Mungu ni mtakatifu.

Jana jioni, wakati wale Malaika walipofunika nyuso zao. Maserafi watakatifu wenye nyuso takatifu, hata hawajui dhambi ni nini, nao hawana budi kufunika nyuso Zao, Mbele za Mungu; kufunika miguu yao, katika unyenyekevu.

Sasa, Mungu mtakatifu asingeweza kupuuza dhambi, kwa hiyo hakuna kitu kingaliweza kugusa ule mlima alimokuwa Mungu.

Ndipo Mungu akafanyika mwili akakaa kwetu, katika umbo la Yesu Kristo, Mwanawe, uumbaji Wake. Ndipo Mwana huyo akatoa uhai Wake, na ile chembechembe ya Damu ya Mungu ikapasuliwa, kusudi ule Uhai upate kutoka katika ile Damu na kutujia sisi.

Kupitia kwa Damu hiyo tunasafishwa. Na sasa damu yetu, uhai wetu, uliokuja kwa kuishi kwa tamaa za kujuana kimwili, ikaleta uhai wetu duniani. Damu ya Yesu Kristo hutusafisha, inabadilisha tabia yetu, kwa kututumia Roho Mtakatifu; ndipo tunaingia katika tabia ya Uungu ya Mungu, ndipo tunakuwa mahali pa kuishi pa Mungu. Yesu alisema, "Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba Yangu, na Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Mnaona?

35 Tunajua jinsi ambavyo Mungu yumo ndani ya Kanisa Lake. Kanisa linapaswa sasa kuwa linachukua mahali pa Kristo, likiendeleza huduma Yake. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Mnaona? Hilo hapo, likiendeleza kazi Yake.

36 Sasa, Mungu, ama Biblia ilisema hapa, jambo hilo. Stefano alinena juu ya Sulemani kujenga hekalu, "Na Aliye juu haishi katika mahekalu yaliyofanywa kwa mikono. 'Kwa kuwa Mbingu ni Kiti Changu cha Enzi,

na dunia ni pa kuwekea miguu Yangu. Basi ni mahali gani nitakapostarehe?' 'Lakini Mwili umeniwekea tayari.'" Amina. Haya basi.

"Mwili umeniwekea tayari." Mungu anaishi katika umbile la binadamu, akijionesha Mwenyewe katika Kiumbe hicho. Ibada kamilifu! Mungu ndani yetu, tukiwa maskani Yake, Mungu akijidhihirisha. Loo, jinsi tungeweza kudumu kwenye jambo hilo mpaka karibu mngekosa hewa hapa ndani, kutokana na joto. Angalia, kwamba, Mungu daima, wakati wote, amejiakisi katika mwanadamu.

37 Huyo alikuwa ni Mungu katika Musa. Mwangalie, alizaliwa akiwa kiongozi; Kristo. Katika wakati ambapo alizaliwa kulikuwako na mateso ya watoto, wakijaribu kumpata; ndivyo ilivyokuwa na Kristo. Naye alikuwa—aliokolewa wakati huo; vivyo hivyo na Kristo pia. Yeye alikuwa ni mtoa sheria; vivyo hivyo na Kristo pia. Musa alipanda mlima, siku arobaini, na akapata zile amri, kisha akashuka. Kristo alienda jangwani, siku arobaini, kisha akarudi akisema, "Mmewasikia watu wa zamani, 'Usizini' Lakini, ninawaambia, mtu anayemwangalia mwanamke, kwa kumtamani, amefanya uzinzi naye tayari." Mnaona? Mambo yote haya mbalimbali, ambayo, Mungu akijiakisi Mwenyewe.

38 Mwangalie Yusufu, alizaliwa mvulana wa kiroho kati ya—kundi la nduguze. Wote walikuwa ni watu wazuri, hao wote ni wazee wetu. Lakini, wakati Yusufu alipokuja, alikuwa tofauti. Yeye angeweza kuona ono, kufasiri ndoto, naye alichukiwa na ndugu zake kwa sababu ya jambo hilo. Kwa sababu ya kazi ile ile ambayo Mungu alikuwa amempa duniani kufanya, ndugu zake walimchukia kwa ajili ya kazi hiyo. Mnaona? Na yote yalikuwa yakielekeza kwenye msalaba. Na, angalia, yeye aliuzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha, na ndugu zake. Akatupwa shimoni, apate kufa, na ndugu zake. Alichukuliwa kutoka kwenye shimo hilo, kisha akaenda akaketi kwenye mkono wa kuume wa Farao. Wala hakuna mtu angaliweza kuja kwa Farao, aliyeutawala ulimwengu wa wakati huo, hakuna mtu angaliweza kumjia Farao, ila tu kupitia kwa Yusufu. Hakuna mtu anayeweza kumjia Mungu, ila tu kwa njia ya Kristo. Na wakati Yusufu alipotoka ikulu, kabla hajaondoka, kulikuwa na baragumu iliyopigwa, na wakimbiaji walikimbia mbele zake, wakipiga makele, "Pigeni magoti! Yusufu yuaja!" Haidhuru ulikuwa wapi, ama kile ulichokuwa unafanya, jinsi kazi yako ilivyokuwa muhimu; ilikubidi kupiga magoti mpaka Yusufu alipofika pale.

Na wakati baragumu itakapolia, moja ya siku hizi, kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri. Wakati Kristo, Yusufu wetu, atakapoondoka Utukufuni na aje, kazi yako haitakuwa muhimu wakati huo. Kila goti litapigwa, na kumkiri Yeye kwamba ni Mwana wa Mungu. Hiyo ni kweli.

39 Loo, jinsi tunavyomwona katika Daudi! Jinsi Daudi, mfalme aliyekataliwa, alivyoondolewa katika kiti chake cha enzi, na ndugu zake, mwanawe hasa, akaketi kwenye Mlima wa Mizeituni, alipokuwa anapanda, juu ya Mlima wa Mizeituni, akaangalia nyuma juu ya Yerusalemu na kulia; kwa maana hapo watu wake mwenyewe, ambao alikuwa amewatumikia na kuwafundisha mambo ya Mungu, na watu wake mwenyewe walimkataa na kumtupia takataka, wakamtemea mate na kumdhihaki, wakati alipoanza kupanda kile kilima na alikuwa amekataliwa. Loo, jinsi inavyofanana kikamilifu na Mwana wa Mungu, miaka mia nane baadaye; Mfalme aliyekataliwa, miongoni mwa watu Wake Mwenyewe, alivyoketi juu ya mlima na kuulilia Yerusalemu, kama Mfalme aliyekataliwa.

Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akijiakisi Mwenyewe katika manabii hao, akimwakisi Kristo.

Ndipo akaja Mmoja aliyekuwa ukamilifu wa Mungu. Ilikuwa ni Mungu miongoni mwetu.

Na tangu wakati huo, Yeye amejiakisi Mwenyewe katika Kanisa Lake, upande huu wa Kalvari. Kwa hiyo, ninyi mnaona, sisi sote tunajaribu kufikia mahali hapa pa kuishi, hema ya Mungu aliye hai. Sasa kuna baadhi ya watu …

40 Tunaona hapa, Yeye alisema, "Kwanza tuna imani, nguvu, maarifa, kiasi, saburi, wema ama utauwa, na upendano wa ndugu." Vema. Upendo wa kindugu, na kisha uongeze upendo. Hebu nisome hili, yote, tena, ili mwe na hakika ya kulipata sasa. Sasa tutaanzia kwenye kifungu cha 5.

> *Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa;*
>
> *Na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa;*
>
> *Na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, kupendana*, ambako ni upendo.*
>
> *…mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo.*

Sasa Petro anatuelezea jambo fulani hapa kwa muhtasari, vile jinsi ya kufika kule.

41 Sasa nataka kusema jambo hili, ya kwamba, kuna baadhi ya watu walio na sehemu ya sifa hizi, maarifa, hekima, saburi, na kadhalika, ambao hata hawakiri kuwa ni Wakristo. Sasa tunaninii tu … tunafundisha shule ya Jumapili. Na hiyo ni kweli. Kuna watu walio na sehemu ya jambo hili, ambao hata

hawakubali kuwa Wakristo. Lakini hilo halininii … Hilo halitafaulu. Ni kama ndege mweusi akijaribu kuvaa manyoya ya tausi katika mbawa zake, ajifanye tausi. Anajiaibisha tu. Afadhali adumu kuwa ndege mweusi. Mnaona? Wakati anapojaribu kuishi mambo haya bila ya kuwa Mkristo, yeye kwa kweli hayuko katika nafasi yake.

Ni kama mkuyu ukijaribu kutengeneza matofaa. Usingeweza kufanya hivyo, unaona, ingawa ni mti. Lakini hauwezi kutengeneza matofaa.

Ni kama nyumbu akijaribu kutengeneza sufu, akijaribu kuwa kondoo wakati yeye ni—yeye ni nyumbu. Mnaona, yeye hawezi kutengeneza sufu. Hawezi kufanya hivyo. Sufu ni kipawa cha kondoo, si cha nyumbu. Anaweza kujaribu kufanya kama mwana-kondoo, bali yeye angali ni nyumbu. Mnaona? Kwa hiyo, yeye anasema, "Vema, ninaweza kula kama kondoo. Ninaweza kufanya jambo *hili* kama kondoo." Na haidhuru unaweza kufanya nini, huna budi kuwa kondoo kusudi upate kuwa na sufu.

42 Na hebu nisimame hapa kwa dakika moja. Kondoo hatengenezi sufu. Yeye ana sufu kwa sababu yeye ni kondoo. Watu wengi wakijaribu kusema, "Vema, nitajaribu kuwa mzuri. Nitajaribu kufanya jambo hili." Usitengeneze kitu. La, huwezi kufanya hivyo. Kondoo hana, haulizwi, hatarajiwi kutengeneza sufu. Anatoa sufu, na hufanya hivyo kwa sababu ni kondoo.

43 Na unapokuwa Mkristo, unazaa tu tunda la Roho. Hu—hulitengenezi. Hujaribu kulitengeneza. Unajaribu … Usijifanye kitu ambacho wewe sicho. Wewe uwe tu jinsi unavyopaswa kuwa, na ndipo jambo hilo linajishughulikia lenyewe. Je! umewahi kuwasikia watu wakisema, "Vema, ninakwambia. Mimi … Nimejiunga na kanisa. Mimi—kwa kweli ninapaswa kuacha uongo huu"? Unajaribu kutengeneza kitu fulani tena, sasa. Huwezi kufanya hivyo, kwa hiyo hakuna haja ya kujaribu kufanya hivyo, si zaidi ya—zaidi ya nyu—nyumbu anavyoweza kujifanya awe na sufu. Hawezi kufanya hivyo.

Ama, mla mizoga akijaribu kula pamoja na hua, mla mizoga akijaribu—mla mizoga akijaribu kuwa njiwa. Ungeweza kuwazia mwewe huko nje, akisema, "Unajua, mimi ni hua," na ajibandike manyoya machache, aseme, "mnaona, ninafanana na…" Mnaona? Yeye angekuwa na sura mbaya sana. Huyo ni m—mtu anayekiri kuwa kitu fulani ambapo sivyo alivyo. Mnaona, huwezi kufanya hivyo.

Huwezi kusema, "Sasa angalia, ninapaswa kuwa na nguvu, kwa hiyo nitakuwa na nguvu. Ninapaswa kuishi utauwa, kwa hiyo nitakuwa nao tu." Mbona, unajaribu tu kuweka manyoya. Ingawa unaweza kuyapata, bali huwezi kutia manyoya kwa ndege mwingine. Mnaona? Haitafaa kitu. Na inaonesha tu ndege huyo ni mnafiki. Mnaona? Ungeweza kuwazia maskini mwewe akijitahidi kupata manyoya machache ya hua, akisema, "Angalieni, mnaona, mimi ni hua"? Mnaona? Mbona, sisi sote tunajua yeye ni mwewe. Mnaona? Mnaona? Hivyo tu. Tunaweza kusema ya kwamba yeye ni mwewe.

44 Vema, sasa hivyo ndivyo ilivyo, kujaribu ku—kutengeneza Ukristo. Huwezi kufanya hivyo. Jambo la kwanza unalopaswa kufanya, ni kuzaliwa mara ya pili. Huna budi kubadilishwa. Mnaona? Na unapobadilishwa, unakuwa kiumbe kipya. Sasa mnakuwa sawa, sasa. Mnaona? Sasa huna sababu ya kuwa na wasiwasi kuhusu manyoya, yataota tu yenyewe, unapo—unapozaliwa mara ya pili. Naam, bwana.

Kama vile nilivyosema daima. Hebu mchukue ngu— nguruwe, msugue sana na kumvalisha suti ya kisasa, ama ya mlo wa jioni, tuseme hasa, umvalishe, na umwachilie atoke aende zake; ataenda moja kwa moja kwenye shimo la matope na kugaagaa. Maana, mnaona, haingefaa kitu. Yeye ni nguruwe. Hiyo ndiyo tabia yake. Kugaagaa ni asili yake. Huna budi kubadilisha tabia yake, na (yeye) hayo mengine yatafanyika yenyewe.

45 Sasa angalia. Huna budi kuzaliwa mara ya pili, hiyo ni kusema, kubadilishwa. Hakuna budi kuwe na badiliko.

Unasema, "Vema, Ndugu Branham, ninamjua huyu mwanamke hapa, mbona, hata hajatenda jambo lo lote baya. Yeye ni mwanamke mzuri. Ama, huyu mwanamume *fulani*, yeye ni mtu mwadilifu. Yeye kamwe hafanyi chochote. Unajua yeye hamdhuru mtu ye yote." Hilo halimaanishi cho chote. Huenda akawa ni jirani mwema, lakini yeye si Mkristo mpaka atakapozaliwa mara ya pili.

Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili," Yohana Mtakatifu 3, ya kwamba, "hata hawezi kuuona Ufalme." Sasa, hilo linamaanisha, mnaona, linamaanisha "kuelewa."

Unapoangalia kitu cho chote, unasema, "Hata sikioni." Una maana hukielewi.

46 Mtu hawezi kufahamu ni kwa nini watu hupiga makelele. Mtu hawezi kufahamu ni kwa nini lugha ya mwanadamu ingebadilika na angenena kwa lugha. Mtu wa kawaida hawezi kuona jinsi utukufu wa Mungu ungeweza kushuka juu ya macho ya mwanadamu, na angeona ono na kumwambia mtu mambo fulani, na kwamba afanye nini; atamke mambo yanayokwenda kutukia, na ataje mambo yajayo, kama Bwana alivyotufanyia hapa jana usiku, hata hivyo. Mnaona? Mnaona? A—a akili ya kawaida hujaribu kuwazia. "Vema, yeye alifanya nini? Ama, anatumia hila ya namna gani? Ana vitimbi vya aina gani?" Kuona mtu

akinena kwa lugha, wangesema…na mtu fulani akafasiri na kusema vile vile kabisa mshiriki fulani wa ule Mwili kitu walichofanya, na yale wasiyopaswa kufanya. Mnaona? Mnaona? Wanafikiri ni namna fulani ya uongo. "Kuna kitu fulani kilichopangwa kati yao."

Hawawezi kufahamu jambo hilo mpaka mtu huyo amezaliwa mara ya pili. Basi anapozaliwa mara ya pili, ndipo ameingia sasa katika ushirika, kwa maana yeye ni kiumbe kipya. Ile tabia ya kale ya ushirikina, ya kushuku aliyokuwa, imekufa. Sasa, yeye ni kiumbe kipya. Kwa hiyo, mnaona, hana sababu ya kujibandika kitu cho chote, sasa, kwa sababu itaongezeka moja kwa moja yenyewe.

47 Angalia, huna budi kuzaliwa mara ya pili. Na unapozaliwa mara ya pili, huwezi kuzaliwa mara ya pili bila ya kuwa na imani. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, kwenye mchoro wangu hapa, nimeweka msingi wenyewe, imani ndiyo msingi wa mambo hayo yote. "Kwa maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu. Yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini ya kwamba Yeye yupo, na huwapa thawabu hao wamtafutao kwa bidii." Mnaona? Hana budi kuwa. Na wakati wewe unaposhuku Biblia, wakati wewe unaposhuku Neno kwamba ni kweli, afadhali ungoje mpaka kwanza uamini jambo hilo.

Dhambi ni nini? Kutokuamini. Kuna hali mbili tu zinazomwongoza mwanadamu. Hizo ni aidha shaka ama imani, moja ama nyingine. Wewe unamilikiwa na ile inayotawala maisha yako. Inategemea tu una imani kiasi gani, kiasi gani unaweza kupanda juu.

48 Lakini, kwanza, haina budi kuwa ni imani. Hebu nidumu kwenye msingi huo kwa muda kidogo. Lakini, kwanza, haina budi kuwa ni imani. Imani ni kile… "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo." Ni, wewe unayo tayari unapokuwa na imani, kwa kuwa hufunuliwa katika imani. "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo," Waebrania 11, mnaona, "ushahidi." Ni kitu gani? Ni ushahidi wa namna gani? Ushahidi mtakatifu.

Kwa hiyo, unaposema, "Ndugu Branham, ninaamini ya kwamba Mungu ni mponyaji." Vema, kama unaamini jambo hilo, kisha umkubali kama mponya wako, wala hudanganyi, bali kweli unaamini ya kwamba kwa kupigwa kwake unaponywa, hakuna kitu kitakachokuondoa kwa hilo. Ni jambo lililolomalizika. Sasa unaweza ukawa na tumaini, unaendelea tu kuepa *hili* na kuepa *lile*. Bali unapokuwa na imani, unajua, kwa maana ni bayana. Unayo tayari. Nilikuwa …

49 Ni wangapi, mtu ye yote, amewahi kumsikia Oral Roberts asubuhi ya leo, alipokuwa akihubiri asubuhi ya leo, Oral Roberts? Ni—nilimsikia akisema jambo fulani ama lingine kuhusu kwamba kulikuwako na imani fulani, ile ya ukombozi, kuomba maombi ya imani, ya ukombozi. Yeye alisema, "Fanya mawasiliano yako kwa kugusa redio, fanya mawasiliano yako kwa kugusa kitu fulani, kusudi …" Mtu huyo alikuwa akifanya hivyo, ili kwamba jambo hilo lipate kuwapa watu kitu ambacho wangeweza kugusa kwa mikono yao. Kitu fulani, unasema, "Nimekipata sasa, kwa maana aliniambia niguse redio yangu. Nimekipata." Mnaona? Sasa, hilo ni sawa. Lakini, sasa, imani halisi na ya kweli si lazima iguse kitu cho chote kama hicho. Sasa, mimi simhukumu Ndugu Oral, hata kidogo. Yeye anafanya kazi kubwa, na ni mcha Mungu, nami kwa—kwa kweli ninampenda sana Oral Roberts. Ninasikitika sana hatuna watu wengi kama hao.

Lakini kile ninachojaribu kusema, ya kwamba—ya kwamba, imani haihitaji jambo lo lote. Mnaona? Imani huamini Neno la Mungu. Kwa maana imani huja kwa "kugusa"? La. "Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu." Hiyo inatia nanga. Iko pale. Mnaona? Na imani, kama ilivyosema, haina umbali na jambo hilo. Imani ni sasa hivi. Imani iko hapa. Sasa kama kama kuna mtu fulani …

50 Huyo mtoto mchanga, hivi majuzi. Yule mama ambaye Dada Kidd na hao wengine waliyezungumza habari zake, aliyekuwa na yule mtoto mchanga aliyekuwa na matumbo yaliyokuwa yametoka nje, asiye na njia ya haja kubwa, kupitishia chakula. Sasa, mama huyu, alipomsikia Dada Kidd na hao wengine wakishuhudia, aliamini ya kwamba kama angeweza kupata mawasiliano, nami nimwombee mtoto huyo mchanga. Sasa, mnaona, Mungu hutupa watu …

Baadhi yetu tuna matukio mengi na Mungu, ya—ya halisi mno hivi kwamba Mungu anakuwa tu ni kama kwenda hapa, kama, na kuzungumza na Ndugu Neville ama mtu fulani unayemfahamu. Na wakati mwingine tunawaomba watu hao watuombee. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Basi kama tuna imani ya kwamba mtu yule ama mwanamke yule, au ye yote yule anayetuombea, anazungumza na Mungu, basi imani yetu imeshikilia. Imeshika sana. Imetulia.

51 Hapa. Yule Mrumi alitoka akaenda kumlaki Yesu. Naye akasema, "Si—sistahili ya kwamba ungeingia chini ya dari yangu. Mimi sistahili. Mi—mimi sistahili. Na mi—mimi sikuninii… Si—sijihesabu hivyo. Lakini," kasema,"mwanangu ni mgonjwa sana. Nawe nena tu Neno, mnaona, na mwanangu ataishi."

Ilikuwa ni kitu gani? Umbali haukuleta tofauti yoyote. Mnaona? Kwa sababu, Mungu yuko kila mahali. Mungu ni mwenye nguvu zote. Na kila mahali alipo Mungu, nguvu zote zipo. Na Mungu, akiwa kila mahali, hilo linamfanya Mungu kuwa kila mahali, kote kote. Mnaona? Mungu ni mkuu vivyo hivyo huko Ujerumani, Uswisi, na huko chini Afrika, dakika hii, kama alivyo papa hapa. Loo! Haya basi.

Kwa hiyo sasa yeye alisema, "Sistahili Wewe uje chini ya dari yangu. Nena tu Neno." Ilikuwa ni kitu

gani? Ilikuwa ni imani ya huyo Mrumi. Yeye aliamini jambo hilo.

Naye Yesu akasema, "Nenda zako. Mwanao yu hai."

Naye akaondoka, safari ya siku mbili. Na kesho yake, kabla hajafika nyumbani, alikutana na baadhi ya watumishi wake wakija. Nao wakasema, "Mwanao yu hai."

Na huyo Mrumi alifurahi sana, mpaka akasema, "Ni saa ngapi alianza kupata nafuu? Ilikuwa ni saa ngapi?"

Akasema, "Yapata saa kumi na moja, yeye alianza kupata nafuu."

Ndipo huyo Mrumi akajua ya kwamba ilikuwa ni wakati ule ule ambao Yesu alisema, "Mwanao yu hai," naye akaamini. Amina.

52 Mwenye nguvu zote, aliye kila mahali, ajuaye yote, asiye na kikomo, huyo ni Mungu. Kwa hiyo, wakati walipopiga simu na kusema, "Omba!" Hilo huwasiliana! Na imani yako humleta Mungu. Ndicho kitu kinacholeta maombi na Mungu, pamoja; jukwaani. Maombi! Imani hubadilika kutoka *hapa* kwenda *hapa*. Inaunganisha.

"Nena Neno. Yote ninayokutaka ufanye ni kusema Neno, na kila kitu ni sawa." Mnaona, haikumlazimu kuwepo pale. "Sema tu Neno." Kwa nini? Mungu yuko kila mahali. Yeye ana nguvu zote. Yeye yuna nguvu nyingi tu chini ya dunia kama alivyo nazo juu ya dunia, ama upande wo wote. Yeye ni Mungu. "Na jambo pekee unalopaswa kufanya ni kunena tu Neno," akasema.

Na, sasa, imani hufanya hayo mengine. Imani ndiyo inayofanya hayo mengine. Kwa hiyo huna budi kuwa na imani kama msingi. Ukristo wote, yote uliyo, yote utakayopata kuwa, yanategemea imani katika Neno. Hiyo ndiyo sababu ninaamini Neno. Mnaona?

53 Siwezi kuweka imani yangu juu ya kitu kingine. Kama ningelikuwa ninataka kuiweka juu ya kanisa, ningeiweka kwenye kanisa lipi: Katoliki, Lutheri, Methodisti, Baptisti, Wapentekoste? Ningeiweka juu ya nini? Sijui. Yote yanayumba na mambo mengine chungu mbovu, yana mwelekeo uliopinda, na cho chote kile.

Lakini wakati ninapoweka imani yangu katika Neno Lake, imetia nanga. Hakuna mtu anayeifasiri. Hii hapa, BWANA ASEMA HIVI. Ndipo ninaamini Hilo. Huo ndio msingi wake.

54 Maskini daktari mmoja hodari mwenye akili sana hapa jijini, rafiki msiri wangu, Daktari Sam Adair. Tumekuwa wavulana pamoja. Nyote mnamjua Sam. Naye akaniambia, akasema, "Bill …" Baada ya ono hilo kuja, nikamwambia mahali ambapo angejenga mahali pake, jinsi ingeonekana. Sasa nendeni mle, mwulizeni wakati mwingine kama hilo si kweli. Miaka miwili ama mitatu kabla halijatukia, nikamwambia mahali litakapokuwa. Nikasema, "Utachukua karibu jengo hilo lote hilo la mji." Na hakuna kitu ila kimoja tu kati yake na hilo, na hicho ni mahali pale pa kurekebisha maisha ya waathirika. Daktari Adair ana sehemu hiyo iliyosalia, na duka la madawa baridi. Hivyo tu. Adair alijaza hapo sawasawa kabisa, ono hilo. Ambapo, mahali ambapo alisema, "Hapawezi kuguswa hata kwa miaka ishirini na mitano. Eneo hilo liko kortini."

Nikasema, "Daktari, Bwana anakupa sehemu hiyo, kwa sababu ya unyenyekevu wako."

Akasema, "Mimi si mzuri."

Nikasema, "Wewe ni kasa. Una gamba upande wa nje, gamba ambalo utaangalia marafiki zako nalo hapa nje, lakini ndani yako wewe ni muungwana halisi. Toka kwenye gamba hilo." Nikasema, "Mungu anakupa sehemu hiyo."

Akasema, "Sijawahi kukushuku, Billy, bali itabidi nishuku hilo."

Nikasema, "Nenda kwenye ofisi yako." Na kwa hiyo akatoka akaenda zake.

Kesho yake asubuhi, akanipigia simu, kasema, "Ninasikia baridi nusura ya kufa."

Nikasema, "Kuna nini?" Ilikuwa kwenye Julai. Nikasema, "Kuna nini, Dak?"

Kasema, "Nimenunua mahali pale tayari, Billy. Walikuwa na mkutano jana usiku huko Boston, nami tayari nimepanunua mahali pale asubuhi ya leo."

Nikasema, "Nilikwambia."

Nilikuwa huko hivi majuzi, nikizungumza naye, wakati ile bunduki iliponilipukia usoni… Akasema, "Nadhani nimewaambia jambo hilo watu elfu moja wanaokuja hapa ndani, namna hiyo." Ni kitu gani? Sasa, Mungu anaponena lolote, halina budi kutukia.

55 Jana jioni baadhi ya marafiki waliingia. Walikuwa wamesikia hilo ono lililosimuliwa juu ya yule karibou aliyekuwa na pembe ya inchi arobaini na mbili, na yule dubu mwenye manyoya ya rangi ya fedha. Sijui ni watu wangapi wamekuja nyumbani, wanaotaka kuona jambo hilo. Nikasema, "Huu hapa utepe wa kupimia. Nenda ukapime hiyo pembe." Alisikia jambo hilo likisemwa kabla halijatukia. Mnaona? Kwa nini? Mungu anaposema jambo lo lote, halina budi kutukia. Hiyo ndiyo sababu, limewekwa msingi.

Sasa, *huu* hapa mpango wa wokovu. Ndipo basi kama ono lake lilitukia kikamilifu, barabara kabisa kama wanavyosema, na kanisa hili hapa linajua hiyo ni kweli, basi na Neno Lake je! Mnaona? Hilo ni hakika zaidi kuliko ono. Kama hilo ono halikunena kulingana na Neno, basi ono hilo ni haramu. Lakini ni Neno, kwanza, kwa sababu Neno ni Mungu. Mnaona? Kwa hiyo, Yeye yuko kila mahali. Alinena jambo hilo hapa, na kulifanya likatimie huko Canada. Amina. Mnaona, Yeye yuko kila mahali. Vema.

56 Kwanza, huna budi kuzaliwa mara ya pili. Halafu basi unapozaliwa mara ya pili, una imani; unaamini Neno. Mpaka utakapozaliwa mara ya pili, utalipinga Hilo. Kama wewe ni mtu tu mwenye mwelekeo wa dini, na—na una ma—ma—maarifa kidogo ya kibinadamu ya kwamba unapaswa kufanya haki, kamwe hutaweza kukubaliana juu ya Neno la Mungu. Kamwe hutaweza. Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Na, kuzaliwa mara ya pili, kunaleta imani. Vema. Halafu, baada ya kupata imani, hii papa *hapa*, i-m-a-n-i, imani, ndipo unaweza kukua.

57 Sasa, watu wengi huenda madhabahuni, na kuomba, na kusema, "Bwana, nisamehe." Na tukio kubwa la utakaso linashuka juu yao, na kadhalika. Ndipo una wakati wa furaha kuu, unaenda madhabahuni, ukipaza sauti. Unarudi, unasema, "Mungu atukuzwe, nimeipata." La, ndio kwanza tu umeanza kufikia katika mahali ambapo unaweza kukua. Hujafanya kitu bado. Mnaona? Jambo pekee ulilofanya ni kuweka tu msingi.

Sasa unaenda kujenga nyumba, na unamimina msingi, unasema, "Jamani, nimeipata." Mnaona? Umeweka msingi wa kujengea nyumba yako. Sasa inakubidi kujenga hiyo nyumba.

Sasa hapo ndipo jambo hilo linapoingia, asubuhi ya leo, tutakalozungumza habari zake sasa. Vema. Nyumba, msingi huu ndio wa kwanza. Msingi wa Ukristo ni nini? Imani katika Neno la Mungu. Huo ndio msingi wako. Ndipo unaanza kukua. Ndipo unaanza, unaanza kuongeza kwenye msingi huu.

58 Sasa, kujenga nyumba, unaweka nguzo zako za kusimama na cho chote kile. Ndugu Woods, na baadhi ya hawa maseremala na makondrakta hapa wangeweza kutwambia jinsi unavyojenga nyumba yako. Mnaona? Lakini nitawaambia jinsi ya kujenga nyumba yenu ya kiroho, ambapo Mungu anaweza kukaa. Anataka kukaa ndani yako. Anataka kukufanya kama Yeye Mwenyewe. Anataka uakisi, uakisi, hasa, Utu Wake.

59 Mwajua, katika ule wakati wa kale walipokuwa wakitengeneza dhahabu, kabla hawajakuwa na kiyeyusho cha kuichoma moto, walikuwa wakizipiga hizo dhahabu, wakipiga matope, chuma na shaba na kadhalika, nje, na kuendelea tu kupiga , na kuigeuza, na kuipiga. Wahindi wanafanya hivyo siku hizi, kutwanga dhahabu, nao wanaitwanga. Unajua jinsi wangeweza kujua ya kwamba chuma chote kilikuwa kimetoka, na uchafu wote na kadhalika, na donge la chuma vimetoka? Ni wakati yule aliyekuwa akiipiga angeweza kuona pameakisiwa, kama kioo, ndani yake. Ilikuwa ni safi na inaakisi vya kutosha mpaka ikamwakisi mpigaji.

Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya. Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya. Yeye huchukua dhahabu ambayo amepata ardhini, na anaitwanga, kwa Roho Mtakatifu, anaigeuza, na kuigeuza, na kuigeuza, na anaitwanga mpaka (Yeye anapokea) Yeye anaweza kuona picha Yake. [Ndugu Branham alipiga makofi mara kadhaa katika sentensi hii — Mh.]

60 Na hilo ndilo tunalopaswa kufanya, kumwakisi Mwana wa Mungu. Na sasa tunapaswa kufanya kazi Yake. Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi …" Yohana Mtakatifu 14:7, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Unaanza kuakisi matendo ya Kristo.

Lakini wengi wetu tunajaribu kufanya kazi za Kristo kabla ya sura ya Kristo kuwa ndani yetu. Sasa hapa ndipo penye shida. Tunaona mambo hayo yakitendeka. Mnajua jambo hilo. Ninajua jambo hilo. Tunaona hawa, wakijikwaa njiani. Tunaona malundo ya takataka ya wahudumu, ya Wakristo, wamelundikana barabarani, ni kwa sababu hawakuliendea jambo hilo inavyotakiwa.

Na hiyo ndiyo sababu niko hapa asubuhi ya leo, kujaribu kulifundisha kanisa hili dogo, na mimi mwenyewe, jinsi ambavyo tunaweza kufanyika mahali pa kuishi pa Mungu aliye hai. Ni wangapi wanapenda kuwa hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Maskani ya Mungu aliye hai!

61 Sasa hivi ndivyo tunavyofanya. Jambo la kwanza ni nini? Uwe na imani, na uzaliwe mara ya pili. Huko ni kuweka msingi.

Halafu, baada ya kuweka msingi, pili unaongeza kwenye msingi wako. "Ongeza kwenye imani yako," Petro alisema hapa. Ongeza kwenye … Kwanza una imani, ndipo unaongeza nguvu katika imani yako. Hii

ndiyo safu inayofuata. Kwanza, mimina msingi wako, imani. Halafu, kwenye imani yako, ongeza nguvu.

Sasa, papo hapo tunaangushwa wengi chini. Naam, bwana. Naam. "Ongeza nguvu katika imani yako." Hiyo haimaanishi tu kuishi maisha safi, mnajua, kama mwanamke ama mwanamume, na kadhalika. Hilo halina uhusiano wowote na jambo hilo.

62 Biblia ilisema, tulisoma hapa katika Kitabu cha Luka, ambapo ilisema, "Nguvu zilimtoka." Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kama tutakuwa kama Yeye, hatuna budi kuwa na nguvu, basi. Hatuna budi kuwa nazo, tupate kuwa kama Yeye. Ndio wimbo wa kwanza niliopata kupenda, katika nyimbo za dini, mmojawapo wa zile kuu sana, ulikuwa, *Kufanana na Yesu*. Vema, kama nitakuwa kama Yesu, sina budi kuwa na nguvu, na bubujiko ambalo linaweza kutiririka kutoka kwangu liwaendee watu. Kwa sababu, "Nguvu zilimtoka zikawaendea watu." Nguvu! Na kabla ya kuweza kuzitoa, huna budi kuwa nazo kwanza. Kama hunazo, hazitatoka. Hakuna mahali zinapoweza kutoka.

Vipi kama mtu fulani angelijaribu kutoa nguvu hizo kutoka kwetu, na hundi hiyo ingerudishwa "Hakuna fedha za kutosha"? Mnaona? La, la, hakuna mahali pa kuzitoa, hundi imekataliwa. Mtu fulani akikuangalia kama Mkristo, na kesho akuone hapa nje ukifanya yasiyofaa kama mwenye dhambi, hakuna uweza mwingi unaoweza kutolewa kutokana na tabia hiyo. Mnaona? Kweli.

63 Nguvu lazima ziwe ndani yetu. Na mpaka tutakapopata nguvu … Ndipo tutakapopata nguvu za kweli, tunaweza kuzitia kwenye imani yetu. Huo ndio ukuta wa pili wa msingi. Sasa, kwanza huna budi kuwa na imani. Imani pekee haitafanya hivyo. Huna budi kuninii… Petro alisema, "Halafu tia nguvu katika imani yako." Huna budi kuwa na nguvu, kusudi upate kuzitia kwenye imani yako.

Sasa, basi, huenda ikawa, sababu ya wewe kutokuwa nazo, ni kwa sababu makanisa mengi ya siku hizi yanafundisha si lazima uwe nazo, ama siku zake zimepita. "Haiwalazimu kuwa nazo. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kujiunga tu na kanisa. Naam, siku hizo zimepita."

Nguvu, kila mtu anajua neno nguvu lina maana gani, mnaona, nasi hatuna budi kuwa nazo. Kama nguvu zilimtoka Yeye, kumponya yule mwanamke aliyekuwa mgonjwa, Yeye anatarajia nguvu zile zile katika Kanisa Lake, kwa maana Yeye alikuwa ni mfano wetu. Na kama Yeye alikuwa na nguvu za kuwapa watu, Yeye anatutarajia sisi kuwa na nguvu za kuwapa watu. Na wema ni nini? Wema ni nguvu, uweza.

Wengine wao hata hawaamini katika nguvu za Mungu. Wanasema, "Hizo—hizo—hizo zimepitwa na wakati. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuweka tu jina lako katika Kitabu, na unyunyiziwe, ama umwagiwe, ama ubatizwe, ama cho chote kile. Na hayo tu ndiyo unayopaswa kufanya."

64 Lakini Petro alisema hapa, "Tieni nguvu." Sasa, Petro anazungumza juu ya kuijenga Nyumba ya Mungu, mnaona, Hekalu la Mungu, kulifikisha mahali fulani. Na baada ya kuwa na nguvu, huna budi kuwa … Baada ya kuwa na imani, huna budi kuongezea nguvu kwenda pamoja na imani. Hiyo ni kweli. Uwe na nguvu kwa ajili ya ulimwengu wote.

Nilihubiri mahubiri yapata miaka ishirini iliyopita, nadhani, juu ya Kasisi Bw. Yungiyungi. Yungiyungi, yule mchungaji. Niliyatoa kutoka kwenye fungu la maneno ambapo Yesu alisema, "Tafakarini ua, jinsi hayafanyi kazi wala hayasokoti. Nami nawaambia, Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo."

Angalia yungiyungi. Linatoka huko chini kabisa kwenye uchafu. Na kila dakika ya siku halina budi kuwa likinyonya kutoka ardhini. Mnaona? Nalo linafanya nini na nguvu linazofyonza? Linautoa. Linaonesha umbile zuri kwa mwenye kulitazama. Linajifungua kwa ajili ya asali, kusudi nyuki aje achukue sehemu yake. Halilalamiki. Linayo tu, lipate kuitoa. Vipi kama nyuki akiingia ndani mle; ati hamna fedha za kutosha, hakuna asali? Maskini nyuki huyo angekuna kichwa chake na kusema, "Hilo ni yungiyungi la aina gani?"

65 Kama mtu anakuja, akijaribu kutafuta wokovu, aende kwenye kanisa linaloamini ya kwamba siku za miujiza zimepita?

Kama vile Jack Coe alivyosema wakati fulani. Mtu akiingia mgahawani, na kuchukua menyu kubwa ya vyakula; anaanza kuisoma, T-boni ya steki na kadhalika. Sema, "Nitachukua T-bone."

"Vema, hiyo ilikuwa ya jana. Hatuna."

Hata afadhali aiweke chini hiyo menyu na atoke, mnaona, hiyo ni kweli, maana hawana cho chote cha kula, hata hivyo. Kwa hiyo afadhali uende mahali ambapo mgahawa una chakula.

Naye mtu wa kiroho, ili akue, anahitaji kitu cha kula. Hilo ni Neno la Mungu. Ninaamini kila Neno Lake.

Mungu ameandaa meza ambapo watakatifu wa Mungu wanalishwa,
Anawaalika watu wake wote waliochaguliwa, "Njoni mle."
Yeye anawalisha kwa mana Yake, anatupa haja zetu zote,
Loo, ni raha kula pamoja na Yesu daima.

Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Yeye ana Neno. Kanisa lina Neno, Kanisa la Mungu aliye hai, ambalo limejengwa katika mtu huyu mkamilifu, mwenye maarifa ya Kristo. Sasa, sasa, huna budi uwe na nguvu.

66 Nilisema basi, muda si muda unajua, kuna mtu ambaye anapenda kusikia hiyo harufu nzuri. Yeye si mchoyo. Yeye ana manukato. Kabla ya yeye kutoa hiyo harufu nzuri, hana budi kuwa nayo. Kabla hajatoa asali, hana budi kuwa nayo. Kabla hajaweza kutoa urembo, hana budi kuwa nao.

Kabla hujaweza kutoa nguvu, huna budi kuwa nazo. Kwa hiyo, ongeza kwenye imani yako, nguvu. Amina. Mnaelewa? Tungeweza kudumu kwenye hilo muda mrefu, lakini wakati wetu ungetuishia. Kutia nguvu katika imani yako. Sasa, kwanza ni imani, halafu nguvu.

67 Halafu basi, tatu, unatia maarifa. Maarifa, sasa, hiyo haimaanishi maarifa ya ulimwengu, maana hiyo ni ujinga kwa Mungu; bali ni maarifa ya kuamua, kupambanua (nini?) wema na ubaya. Unapambanuaje hilo, basi, kama una maarifa ya Kikristo pamoja na nguvu zako na imani? Unapambanua kama Neno ni kweli ama ni uongo. Na kama unaweza kuweka kando kanuni zako zote za imani, na kutokuamini kwako kote, kila kitu unachodai umekwishafanya, ndipo una maarifa ya kuamini ya kwamba Mungu hawezi kusema uongo. "Neno la kila mtu na liwe uongo, bali Langu liwe kweli." Mnaona? Sasa unapata maarifa. Hayo ni maarifa ya juu kabisa. Haikubidi kuwa na digrii nne katika chuo fulani, ama kitu kama hicho, kuyapata, kwa maana sifa hizi zote zinapeanwa na Mungu, upate kuziweka kwenye msingi wako wa imani, upate kufikia kimo kikamilifu cha mtu halisi aliye hai, wa Mungu. Naam, bwana.

68 Tia, tia maarifa, kwa sababu, maarifa ya Neno Lake. Huna budi kuliamini kwa njia hii. Kwa mfano, unapaswa kuamini leo ya kwamba ninii…na kulikubali, ya kwamba siku za miujiza hazijapita. Maarifa ya kwamba yale aliyosema Mungu, Mungu anaweza kuyatimiza.

Ibrahimu aliamini jambo hilo. Na wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja, yeye hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini. Angalia jinsi Neno hilo lilivyoonekana la kipuuzi. Huyu hapa mwanamume, mwenye umri wa miaka mia moja, akimtazamia mtoto kuzaliwa nyumbani mwake, na mwanamke mwenye umri wa miaka tisini. Mnaona? Amepita umri wa kuzaa kwa karibu miaka hamsini, alikuwa ameishi naye tangu alipokuwa msichana m—mdogo, ama kijana. Na tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa. Na tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa. Na matumaini yote yalikuwa yamekwisha, tukinena juu ya matumaini. Lakini, hata hivyo, pasipo tumaini, aliamini katika tumaini, kwa kuwa alikuwa na maarifa ya kwamba Mungu alikuwa anaweza kutimiza kila kitu ambacho aliahidi.

69 Sasa, unapolipata namna hiyo, basi tia jambo hilo katika imani yako. Unapokuwa na nguvu za kweli, ziongeze kwenye imani yako. Unapoweza kutembea hapa nje mtaani, kuishi kama Mkristo, kutenda kama Mkristo, kuwa Mkristo, ongeza hilo kwenye imani yako. Unapokuwa na maarifa …

Unasema, "Vema, sijui sasa kama Maandiko *haya* ni kweli. . Sasa hapa kuna Matendo 2:38, sijui jinsi ya kuyaendea Matendo 28:19. Sijui." Vema. Usininii—usiongeze kitu, maana hujalipata Hilo bado. Mnaona? Utafanya nini? Kwa sababu, huna maarifa ya kutosha kumjua Mungu, bado, ya kwamba Biblia haijipingi Yenyewe. Liache. Usiseme Neno la zaidi kulihusu. Mnaona? Liache.

Lakini unapoweza kuona ya kwamba Maandiko hayajipingi, ya kwamba unaweza kusema jambo hilo; na unaweza kuona, ya kwamba, kwa ufunuo wa Mungu, Neno lote limeandikwa katika siri, na ni maarifa ya Mungu pekee ndiyo yanayoweza kulifunua; basi wakati unapopata na kusema, kuitikia kila Neno la Mungu kwa "amina," basi tia hayo katika imani yako.

70 Loo, umeanza kuwa mtu mzuri sana sasa hivi. Mnaona? Unakuja, mnaona. Na kitu gani? Na imani, halafu na nguvu, halafu maarifa. Mnaona mtu huyu anavyojengeka? Mnaweza kuona hakuna njia—hakuna njia ya kuepuka jambo hilo. Hii ndiyo jinsi ya kufanyika kimo kikamilifu cha Kristo. Naam, bwana.

Kupambanua, kupambanua kweli. Kupambanua kama ni kweli ama si kweli, kuamini Neno la Mungu. Kupambanua kama ni kweli ama si kweli, kama ninapaswa kutumikia kanuni ya imani ama kumtumikia Mungu. Kupambanua kama ni kweli ama si kweli, kama ninapaswa kuzaliwa mara ya pili ama kujiunga na kanisa. Ndipo unaanza. Unapambanua vizuri, wakati mhubiri anaposema, "Siku za miujiza zimepita." Biblia ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Sasa utaamini lipi?

Unaposema, "Nitamchukua Mungu." Sasa, husemi jambo hilo kwa kusema tu, "Vema, ni—nalichukua," toka moyoni mwako kabisa. Lakini, jambo fulani ndani yako, imani yako inasukuma humo ndani. Haya basi. Imani yako inasema, "Ninajua Yeye ni yeye yule. Amina. Nimemshuhudia ni Yeye yule. Hakuna kitu kinachoweza kuliondoa jambo hilo kwangu. Ninajua Yeye ni halisi." Amina. Kisha ongeza jambo hilo kwenye imani yako. Liweke kwenye ule msingi. Unapanda sasa, unakua moja kwa moja kuelekea kwenye ule Ufalme. Umefikia mahali fulani sasa. Vema.

71 Sasa, jambo lingine, mhubiri atakwambia, na watu wengi wanasema, "Ninii… Mambo haya mnayosoma katika Biblia, yalikuwa ni kwa siku za kale. Sasa, nitawaambia ni kwa nini. Kwa sababu, hatuhitaji mambo hayo leo. Hatuyahitaji. Mnaona? Hatupaswi kufanya hivyo. Hatuna haja ya kutenda mambo hayo. Uponyaji wa Kiungu. Hatuneni kwa lugha, kanisani, ku—kuliweka kanisa letu sawa. Nasi hatufanyi jambo

*hili*."

Tutalifikia hilo. Nina Maandiko niliyoandika hapa yanayohusu hayo, mnaona, kama tungali tunapaswa kuyafanya siku hizi ama hatupaswi, sasa.

Lakini umesema, "Sijui. Haitupasi kufanya jambo hilo leo. Jambo pekee ningefikiri tungepaswa kufanya, inatupasa kujifunza kuongea kwa ufasaha mbele ya umati wa watu. Tunapaswa kwenda na kuchunguzwa akili zetu na daktari wa magonjwa ya akili, aone kama Kiwango chetu cha Akili ni cha juu vya kutosha kufanya jambo hilo, na—na kadhalika namna hiyo. Nafikiri … Nasi tuna makusanyiko makubwa kuliko yote. Tunaunda madhehebu yetu."

72 Sisi hatuundi madhehebu. Mimi siko hapa asubuhi ya leo kuunda madhehebu. Kristo hakunituma kamwe kuunda madhehebu. Kristo alinituma kuwajenga watu binafsi wafikie kiwango cha Yesu Kristo, kusudi wapate kuwa kituo cha nguvu na makao ya Roho Mtakatifu, kwa Neno Lake. Kwa Neno Lake, mnaona, kumjenga mtu binafsi afikie mahali hapo. Si kujenga madhehebu kuwa madhehebu makubwa zaidi, bali kuwajenga watu binafsi kuwa wana na binti za Mungu. Hilo ndilo wazo. Mnaona? Tia katika imani yako, nguvu; katika nguvu zako, ongeza maarifa. Vema, sasa unafikia mahali fulani.

73 Sasa wakati wanapoanza kusema, "Vema, si lazima tuchukue jambo hilo siku hizi." Inakulazimu. Lazima lichukuliwe.

Maandiko hayawezi kusema uongo. "Na si ya kufasiriwa kama apendavyo mtu mwenyewe," ndivyo ilivyosema Biblia. Iamini tu jinsi ilivyoandikwa Pale. Mnaona? Unapaswa kuwa nayo haya. Na njia pekee utakavyoweza kuwa nayo, ni kuwa na maarifa yatokayo Mbinguni. Na maarifa yatokayo Mbinguni yatathibitisha Neno. Mnaona?

Huna budi kuamini, si kujifanya unayaamini. Hakuna hata moja ya haya ambayo ni ya kujifanya, unaona, kama ukijaribu kusema, "Ninayo." Usiwe ndege mweusi anaye manyoya ya tausi, unaona, maana yataanguka moja kwa moja. Hayakuota kiasili humo. Yamechomekwa ndani tu.

74 Ninafikiria mahali ambapo Daudi alisema pale, Zaburi 1, "Yeye atakuwa kama mti uliopandwa kando ya mito ya maji." Mnajua, kuna tofauti kati ya kupandwa na kuwekwa, kuchomekwa. Kama vile mwaloni wa kale, umekwisha kupandwa, ambao unanyonganyonga kwenda chini na kushikilia imara. Maskini kijiti cha kale kimechomekwa pale, hujui kitapatikana na nini. Hakina mizizi. Hakina mizizi. Mnaona?

Hiyo ni kama watu wanaotoka seminari ama cho chote kile, mnaona. Hawana… "Vema, Daktari *Fulani* aliniweka wakfu katika huduma." Haileti tofauti yo yote kwamba hicho kilikuwa ni nini..

Kristo alikuzaa humo, unaona, unaona, kwa imani yako. Mnaona? Unaongoka mara ya pili na kuzaliwa ndani yake. Halafu baada ya kuzaliwa ndani yake, haya ndiyo mambo anayokutarajia kuyatia. Endelea tu kuyatia. Sasa tunaenda kwenye jambo lenyewe moja kwa moja.

75 Sasa kutakuwa na jambo lingine juu ya maarifa haya, tungelizungumzia habari zake, maarifa ya kiungu. Mnaona? "Je! Biblia katika siku hizi imepoteza maana yake?" Mnaona, wao, watu wengi hukwambia jambo hilo, ya kwamba Biblia kabisa haimaanishi jambo hilo. Kama Mungu ananiangalia, na kunisahihisha katika dhambi yangu, na kama mimi ni mwana wa Mungu, Yeye anafanya hilo. Yeye anakufanyia hivyo, wana na [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] binti. Unapofanya kosa lo lote, Yeye anakusahihisha. Basi kama Mungu anahusika sana juu yako, kwamba anakuangalia na kukusahihisha, ni zaidi sana vipi Neno Lake, ambalo ndilo mfano wako, ambalo ni Yeye Mwenyewe!

> *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*
>
> *Naye…alifanyika mwili, akakaa kwetu;…*

76 Neno ni Ufunuo wa Yesu Kristo, Biblia ilisema hivyo, Kristo akifunuliwa katika Neno Lake. Na kama Yeye amekuangalia wakati unapovunja sheria hizi, anakuhukumu kwa jambo hilo, ni zaidi sana vipi anavyoangalia sheria Yake inayokuhukumu! Amina.

Ninaendelea, jamani, usiniambie upuuzi huo!

Ninaamini katika maarifa halisi, ya Roho Mtakatifu. Maarifa ya Roho Mtakatifu daima yataitikia Neno kwa "amina." Unapopata mambo haya yanayoonekana kana kwamba yanahitilafiana, katika Biblia, unaketi chini na kuyasoma kwa makini, na kwa maombi namna hiyo. Na muda si muda unajua, Roho Mtakatifu anaanza kuingia. Baada ya kitambo kidogo unayaona yakiungana pamoja, na hapo umeshalipata. Mnaona? Hayo ni maarifa.

77 Wengine wao wanasema, "Vema, sasa, Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni yeye yule jana, leo na hata milele."

Nalo kanisa linasema, "Kwa hali fulani, Yeye ni yeye yule." A-ha! A-ha! Tayari umeweka pengo, papo hapo. Mnaona? Naam, bwana. La, bwana. Yeye ni yeye yule. Naam, bwana.

"Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Hakuna tofauti Kwake, hata kidogo. Yeye anaishi katika Kanisa Lake, akifanya jambo lile lile. "Kitambo kidogo," kama nilivyonukuu hivi punde, "bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, bali ninyi mtaniona. Kwa maana," Yeye alisema, "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Tena, Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Tena, Yeye alisema, "Mimi nitakuwa Mzabibu. Ninyi mtakuwa matawi." Na tawi linaishi tu kwa Uhai wa Mzabibu. Cho chote kilicho ndani ya Mzabibu hutokea kupitia kwenye tawi. Utukufu! Ndipo, "Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Linatoa Uhai wa Bwana Yesu Kristo. Amina.

78 Maarifa; si maarifa ya ulimwengu (yanahoji). Aina yo yote ya maarifa ya ulimwengu hutoa hoja. Mnaona? Lakini imani haina hoja. Mungu anakufunulia jambo *fulani-fulani* litatukia, kila mwanasayansi ulimwenguni angeweza kukwambia, "Ni kinyume. Halingeweza kutukia." Unaliamini, hata hivyo. Mnaona? Naam, bwana. Hayahoji. Biblia ilisema, "Tutupe hoja." Imani haihoji. Imani haina hoja. Imani inajua mahali ilipo. Imani hutenda kazi. Imani inashikilia. Haiwezi kusogea. Hakuna kitu kinachoweza kuisogeza. Sijali chochote kinachosema hivi, vile, vinginevyo. Hausogei, hata kidogo. Inakaa pale pale, ngoja, ngoja, ngoja, ngoja. Haileti tofauti yoyote. Inakaa pale pale.

Mungu alimwambia Nuhu mambo haya yatatukia. Yeye aliamini jambo hilo. Mnaona? Mungu alimwambia Musa mambo haya yatatukia. Yeye aliamini jambo hilo. Mungu aliwaambia wanafunzi mambo fulani yatatukia, "Nendeni kule Pentekoste mkangojee." Walikaa papo hapo. Naam, bwana. Vema.

79 Sasa, maarifa, sasa, si maarifa ya kilimwengu, bali ni maarifa ya Kimbinguni. Na maarifa ya Mbinguni, wakati Mungu ni chemchemi ya maarifa yote, na Mungu ni Neno, basi, kama una maarifa ya Kimbinguni, unaamini Neno, na unahoji jambo lolote kwa Neno.

Na kesi hii ya kodi ambayo kanisa limekuwa nayo, ama ambayo mimi nimekuwa nayo. Mmoja wa watu hao wakati mmoja, katika kesi ndogo iliyosikilizwa na hakimu, yeye aliniambia. Kasema nilisema … "Hawakuweza kupata kosa lo lote." Na kwa hiyo wakaanza kuninii …

Nikasema, "Vema, basi, kama hakuna kosa lo lote, kwa nini msiache kunifuatafuata?" Mnaona? Mnaona? Nami nikaendelea, nikimwambia kuhusu Maandiko fulani.

80 Akasema, pandikizi la mtu huku akiwa ameshika sigara mkononi mwake, akasema, "Bw. Branham, mimi ni mwanafunzi wa Biblia."

Nikasema, "Nina furaha kusikia hilo."

Akasema, "Sasa ninataka kujua ushirikina huu ni nini, unatoza pesa kwa leso hizi unazotuma huko nje, kaushirikina hako ka kuombea leso na kuzituma huko nje, hizo 'leso zilivyotiwa mafuta,' kama unazoita, 'leso.'" Akasema, "Halafu unatoza pesa kwa hizo."

Nikasema, "La, bwana. Hazilipiwi."

Ndipo basi akasema, "Vema, katika ushirikina huu."

Nikasema, "Unaita jambo hilo ni ushirikina, bwana. Uliniambia dakika chache zilizopita ya kwamba wewe ni mwanafunzi wa Biblia."

Akasema, "Ndiyo."

81 Nikasema, "Ninukulie Matendo 19:11." Maarifa! Akajinasa yeye mwenyewe moja kwa moja katika jambo hilo, akajaribu kubadilisha mazungumzo. Nikasema, "Basi ninikulie Yohana 5:14." Hakuthubutu kabisa. Nikasema, "Basi Yakobo 5:14" Hakuthubutu. Nikasema, "Je! unajua Yohana 3:16?" Mnaona? Maarifa, werevu, ulimwengu! Lakini wakati …

Akasema, "Lakini, Bw. Branham, unajaribu kuamua kesi hii kwa Biblia. Sisi tunaiamua kwa sheria za nchi."

Nikasema, "Bwana, je! hivi sheria za nchi hazikuwekwa msingi wake juu ya Biblia? Ndipo ikawa ni haki." Amina! Hakika.

82 Maarifa; si ya kilimwengu. Maafira ya kiroho ya Neno, kujua yale Mungu aliposema, kufanya yale Mungu aliyosema, hiyo ni kweli. Basi ukiwa na hiyo na unaweza kuamini mambo yote haya, ya kwamba, Yeye ni yeye yule katika mambo yote haya Neno linasema ni kweli, unaitikia kila neno kwa "amina". Ni sawa. Ongeza hilo kwenye imani yako. Hilo ni sawa. Ndiyo.

Kama mtu fulani akijaribu kukwambia, ya kwamba, "Biblia imepoteza nguvu zake. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu." A-ha. Usitie hilo. Halitafaa kitu. Litaanguka. Ni kama kuweka udongo wa mfinyazi juu ya mwamba, hautasimama. Utaporomoka.

83 Tena watu wanakwambia, "Biblia haiaminiki siku hizi. Kuwa mwangalifu sasa. Usikubali kuamini jambo hilo. Haliwezi kuwa kweli." Mmesikia hayo wakati wote. Misemo midogo, "Biblia haiaminiki." Vema, kama—kama una jambo hilo mawazoni mwako, usi—usijaribu kulitia, maana halitafaa kitu. Jengo lote zima litaanguka papo hapo.

Halina budi kuunganishwa na Roho Mtakatifu. Ninamaanisha kushikamanishwa, mota inayoishikamanisha. Na kitu kile kile kinachoishikamanisha… Unajua jinsi…

Tyubu iliyotiwa kiraka cha kuchomelewa sikuzote inadumu muda mrefu kuliko kiraka cha kale kilichoshikamanishwa. Joto kidogo hushikamanisha kiraka cha kale kwenye tairi, muda si muda unajua, hebu ipate joto kidogo hiyo tairi, ikimbie mbio kidogo zaidi, basi nayo itayeyuka. Naam, bwana. Mnaona?

Na hiyo ndiyo shida ya watu wengi siku hizi. Wanajaribu kushikamanisha maarifa yao kwenye maarifa ya ulimwengu, kwa gundi kidogo ya siku nyingi ya kilimwengu, na, majaribu yanapokuja, "Vema, labda nilikuwa nimekosea." Mnaona? Ndipo upepo unatoka, unatolewa upepo katika dakika chache. Kupaza sauti kwako kote na kurukaruka hakukusaidia hata kidogo. Watu wanakuona umerudi moja kwa moja katika matope yale yale tena. Mnaona? Hiyo ni kweli.

Lakini kama ukikaa pale ukiwa na joto la kutosha la Roho Mtakatifu, mpaka ikufanye wewe na ile tyubu mmoja. Hilo ndilo jambo lenyewe. Wewe na tyubu mnakuwa mmoja. Wakati utakapokaa hapo mpaka wewe na kila ahadi ya Mungu mnakuwa mmoja, basi tia hayo katika imani yako. Vinginevyo, usitie kitu cho chote.

Unasema, "Neno haliaminiki." Usijaribu kutia jambo hilo.

84 Unasema, "Ahadi zilizomo humu, za ubatizo wa Roho Mtaktifu, zilikusudiwa tu kwa wale mitume kumi na wawili," kama vile baadhi ya makanisa yanavyosema siku hizi, usijaribu kutia hiyo. Hapo ndipo msingi wao ulipo, umebomokabomoka. Mnaona? Kama vile Uzia alivyokuwa, jana usiku, wakati alipoona msingi wa mtu huyu ambaye alimwamini, umevunjika kabisa kabisa, amepigwa na ukoma, haukufaa kitu. Sasa, "Ni kwa wale mitume kumi na wawili tu, ni wale mitume kumi na wawili tu."

85 Nilikuwa huko kwa Ndugu Wright … Nafikiri wako huko nyuma mahali fulani. Usiku mmoja, kulikuwa na mhudumu kule, nilikuwa nikizungumzia, wahubiri wanne ama watano pamoja. Mhubiri huyu alisimama na kusema, "Sasa, ninataka kuwaambia enyi watu wapendwa jambo fulani. Loo, nafikiri ninyi ni watu wazuri."

Nilisema, nilimwambia mtu fulani, nikasema, "Huyo—huyo ndiye yule anayeketi pale. Angalia."

Kwa hiyo, Junior Jackson, kule nyuma, ndiyo kwanza amalize kuzungumza. Naye akasema…alikuwa akihubiri juu ya neema ya Mungu. Loo, jamani!

Alikuwa akiwaka, akingojea. Akafika pale na alikuwa anajaribu kuelewa. "Sasa, ninataka kusema ya kwamba Bw. Branham hapa, ninawaambia, ni mpinga Kristo." Naye akaanza namna hiyo, usiku kucha.

Baadhi ya wahubiri walianza … Nikasema, "Ngoja kidogo. Sasa, msiseme kitu, ndugu. Yeye ni mmoja tu nasi tu wengi." Nikasema, "Mwacheni tu sasa. Ameniingilia." Nilipenda jambo hilo, mimi mwenyewe, sana, sikujua la kufanya. Mnaona?

86 Kwa hiyo, akasema, "Bw. Branham ni mpinga Kristo," na akaendelea akisema kila kitu wajua, karibu kila kitu. Akasema, "Akagusia pale, 'Ubatizo wa Roho Mtakatifu.'" Kasema, "Biblia ilisema kulikuwa na kumi na wawili tu waliopata ubatizo wa Roho Mtakatifu." Akizungumza juu ya kuponya Kiungu, "Wale mitume kumi na wawili tu ndio waliokuwa na uponyaji wa Kiungu." Akasema, "Tunazungumza mahali Biblia inapozungumza, na kunyamaza mahali Biblia inaponyamaza." Nilingojea mpaka alipopayukapayuka pale kwa karibu nusu saa.

Nikasema, "Ngoja kidogo. Nimeandika mengi sana hapa," nikasema, "nipe nafasi nijibu baadhi yake." Na niliposimama, nikasema, "Huyu bwana, yeye alisema ya kwamba alinena 'mahali ambapo Biblia ilinena,' kanisa lake lilifanya hivyo, 'na kunyamaza ambapo Biblia ilinyamaza.' Ninyi nyote ni mashahidi. 'Naam.'" Nikasema, "Sasa, yeye alisema 'Kulikuwa na kumi na wawili tu waliompokea Roho Mtakatifu.' Biblia yangu ilisema kulikuwa na mia moja na ishirini, risasi ya kwanza." Amina! Tupilia mbali maarifa ya namna hiyo, mnaona, aliyokuwa akijaribu.

87 Nikasema, "Basi nafikiri Paulo hakumpokea Roho Mtakatifu wakati aliposema alimpokea." Mnaona?

Nikasema, "Huko chini katika … Wakati Filipo aliposhuka akaenda kuwahubiria Wasamaria. Walikuwa wamebatizwa katika Jina la Yesu. Ila tu, Roho Mtakatifu hakuwa amewajilia. Nao wakatuma wakawaita Petro na Yohana, wakashuka wakawawekea mikono, na Roho Mtakatifu akaja juu yao. Nadhani hao walikuwa ni wale kumi na wawili tu?"

Nikasema, "Katika Matendo 10:49, wakati Petro alipokuwa juu ya nyumba, naye alikuwa ameona ono

kwamba wanaenda kwa Kornelio. Wakati Petro alipokuwa bado akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia waliolisikia lile Neno." Nikasema, "Biblia ingali inazungumza. Kanisa lako liko wapi?" Liko kule nyuma kwenye huenda-ikawa. Hiyo ni kweli. Mnaona?

Nikasema, "Uponyaji wa Kiungu, ulisema, 'Ni wale mitume kumi na wawili tu waliokuwa na uponyaji wa Kiungu.' Biblia ilisema ya kwamba Stefano alishuka akaenda Samaria na kutoa pepo na kuwaponya wagonjwa, na kulikuwa na furaha kuu mjini. Naye hakuwa mmoja wa wale kumi na wawili. Yeye hakuwa mtume. Alikuwa shemasi." Amina. Amina.

88 Nikasema, "Na Paulo hakuwa mmoja wa wale kumi na wawili waliokuwa kwenye chumba cha juu, naye alikuwa na karama ya uponyaji."

Nikasema, "Angalia tu karama za uponyaji! Na kuendelea moja kwa moja, miaka thelathini baadaye, alikuwa angali katika Wakorintho, akiweka karama ya uponyaji katika Mwili wa Kristo." Loo, jamani!

Sasa, maarifa ya namna hiyo unayojifunza kutoka kwenye kitabu fulani, afadhali uyatupe kwenye pipa la takataka. Njoni kwenye maarifa haya. Wakati Mungu aliposema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," sema, "Amina." Naam, bwana. Naam, bwana. Si kwa wale kumi na wawili; ni kwa ajili ya wote. Unapopata i—imani ya namna hiyo, wakati imani yako inapokiitikia, kila kipengele, kwa "amina," ndipo unasema, "Vema," tia hiyo kwake.

89 Nne. Itatubidi kuharakisha, kwa sababu mimi … Unajisikia vizuri sana kusimama hapa na kuzungumza juu ya jambo hilo. Amina. [Ndugu fulani anasema, "Tunafurahia jambo hilo." — Mh.] Naam. Nne … Asanteni.

Ongeza "kiasi." Loo, jamani! Tumefikia kiasi. Sasa, umekuwa na imani, kwanza; sina budi kuwa na jambo hilo, kwanza. Ndipo utie nguvu kwenye imani yako, kama ni aina sahihi ya nguvu. Kisha utie maarifa, kama ni maarifa ya kweli. Sasa utaongeza kiasi.

Wala kiasi hakimaanishi, "kuacha kunywa pombe," hapa. La, la. Kiasi hakimaanishi kwamba tiba ya pombe, si katika suala hili. Hiki ni kiasi cha Biblia, kiasi cha Roho Mtakatifu. Hiyo ni moja tu ya tamaa za mwili, bali tunazungumza juu ya kiasi cha Roho Mtakatifu. Hilo linamaanisha, jinsi ya kutawala ulimi wako, si kuwa mpiga domo; jinsi ya kuzuia hasira yako, si kuhamaki kila wakati mtu anakuudhi. Loo, jamani!

Jamani, wengi wetu wataanguka kabla hatujaanza, sivyo? Mnaona? Ndipo tunashangaa ni kwa nini Mungu hayuko katika Kanisa Lake, akifanya miujiza na mambo waliyokuwa wakifanya. Naam, bwana. Mnaona?

90 Tia na vitu hivi. Tia kiasi katika hayo. Loo, kiasi, jinsi ya kujibu kwa upendo wakati mtu anapokufokea maneno ya hasira. Mtu fulani anasema, "Enyi kundi la watakatifu wanaojivingirisha huko!" Usiruke na kukunja shati sasa. Mnaona? Si hivyo. Bali ongea kwa upendo wa kiungu, kiasi, upole. Je, hivyo ndivyo unavyotaka kuwa? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Unapogadhabishwa, usijibu kwa ghadhabu. Hebu Yeye na awe ndiye mfano wako.

Wakati waliposema, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate," Yeye angeweza kuyageuza, na kuonesha alikuwa ni Mungu. Lakini Yeye alikuwa na kiasi. Walipomwita Yeye, "Beelzebuli," Yeye alisema, "Nitawasamehe kwa kuniita hivyo." Hiyo ni kweli? Walimng'oa vigaja kadha vya ndevu kutoka usoni Mwake, na wakamtemea mate usoni, na kusema, "Shuka msalabani!"

Yeye alisema, "Baba, wasamehe. Hata hawajui watendalo."

91 Wakati, Yeye alikuwa na kipawa, alijua mambo yote, kwa kuwa ndani Yake ulikuwamo na utimilifu wote wa Mungu kimwili. Walikuwa wamemwona akifanya miujiza, kwa kuwaambia watu shida yao, na kadhalika namna hiyo. Walimfunga tambara kichwani namna hiyo, wakamfunga tambara machoni, na kumpiga kichwani kwa fimbo, na kusema, "Tabiri, hebu tuambie ni nani aliyekupiga. Tutakuamini." Mnaona? Alikuwa na kiasi.

Sasa, kama unacho namna hiyo, kitie katika imani yako. Kama ungali unashikwa na hasira na kuzozana, kugombana, kushikwa na hamaki, na kupiga makelele, a-ha, huna ninii… Huwezi kutia hayo, kwa kuwa haiwezekani. Mnaona? Havichanganyikani. Huwezi kuchukua kipande cha mpira, mnajua, na kukichanganya na kipande cha chuma. Haitawezekana kabisa. La, kinapasa kinyumbuke, kama vile kabisa mpira ulivyo. Mnaona? Na wakati imani yako na kiasi chako kinapokuwa aina ile ile ya kiasi cha Roho Mtakatifu ambayo Yeye alikuwa nacho, basi kitaunganika Naye. Unatiwa kwake.

Wakati nguvu zako ni kama nguvu Zake, basi utaingia ndani yake.

92 Wakati maarifa yako ni kama maarifa Yake, "Nimekuja kufanya mapenzi Yako, Ee Mungu." Mnaona? Kwa Neno la Baba, Yeye alimshinda kila pepo. Mbingu na nchi zitapita, bali Neno halitapita. Mnaona? Unapokuwa na maarifa ya aina hiyo, yatashikamana na imani yako.

Unapokuwa na kiasi halisi cha kweli, kama alichokuwa nacho Yeye, kitashikamana. Kama huna, ni imani nusu-nusu tu ya kujitengenezea, iliyochanganyikana, ama kiasi, "Loo, nilipaswa kumpiga kofi, lakini —lakini labda afadhali nisimpige, maana huenda wakaandika jina langu kwenye gazeti juu ya jambo hilo." Hicho si kiasi cha aina hiyo anachonena habari zake. Usijaribu kuongeza hicho. Hakitafaa kitu. Lakini wakati unapoweza kabisa, kwa upole utokao moyoni mwako, kumsamehe kila mtu, unatulia, unaachilia lipite, mnaona, ndipo basi vitaungana. Unaweza kutia hiyo katika imani yako. Whiu!

93 Si ajabu kanisa limepungukiwa sana. Hiyo si ni kweli? Si ajabu. Ningesema, "Tubuni mkabatizwe, Biblia ilisema, katika Jina la Yesu Kristo." Na mtu wa Utatu kabisa haamini jambo hilo, anasema, "Maskini mpinga Kristo huyo wa kale. Yeye ni wa Jina la Yesu. Yeye ni wa Yesu Pekee." Kaa chonjo, jamani, sijui habari za kiasi chako sasa hivi. Mnaona? Mbona usije, useme, "Hebu na tushauriane jambo hili pamoja, Ndugu Branham. Ningetaka kusikia jambo Hili likielezwa"? Mnaona? Basi shuka uje ukasikilize. Halafu linawekwa wazi wazi mbele zako, na basi unaondoka unaenda zako; tuta—tutafikia jambo hilo mnamo dakika chache tu, katika "utauwa," mnaona. Lakini wakati unaninii—unaposhikwa na hasira, unataka kuamua mambo upesi, a-ha, hilo—hilo silo. Mnaona? Huna kiasi cha Biblia bado unapofanya jambo hilo; jinsi ya kujibu. Basi ukiwa una haya yote, unaweza kutia haya katika imani yako.

94 Halafu, baada ya jambo hilo, la nne, unataka kutia saburi katika imani yako. Kama una imani, "inaleta saburi," Biblia ilisema. Mnaona? Kwa hiyo, *hii* ni saburi. Sasa, hicho ndicho kitu kingine kitakachojenga kimo hiki. Mnajua, Mungu ana vifaa halisi katika jengo Lake.

Mnaona jinsi tumepungukiwa, ndugu, dada? Mnaona? Mnaona ni kwa nini, mahali tulipo? Naam, bwana. Mnaona? Tuna utukufu, tuna kupaza sauti na kadhalika, kwa maana tuna imani. Lakini tunapofikia mambo haya hapa, Mungu hawezi kutujenga tufikie kimo hicho. Mnaona? Hawezi. Hawezi kutuumba tufikie mahali pa namna hiyo. Tuna mambo haya mengine yote. Tunaanguka, tunateleza pamoja nayo. Mnaona? Hawezi kulijenga Kanisa Lake.

95 Saburi na kitu gani? Saburi ya namna gani? Jambo la kwanza, mtu awe amekuwa na saburi na Mungu. Kama una imani halisi, ya kweli, utakuwa na saburi halisi na ya kweli, kwa maana imani huleta saburi. Mungu anaposema jambo lo lote, wewe liamini. Hivyo tu. Una saburi.

Unasema, "Vema, nilimwomba jana usiku aniponye, nami ningali mgonjwa tu vile vile asubuhi ya leo." Loo, jamani! Ni saburi ya namna gani?

Mungu alimwambia Ibrahimu, na miaka ishirini na mitano baadaye hapakuwa hata na dalili moja. Yeye alikuwa angali anaamini. Alikuwa na saburi na Mungu. A-ha.

Mweke sikuzote mbele zako. Hebu Yeye na awe ndiye kitu kingine cha kuvuka. Huwezi kumvuka Yeye, kwa hiyo dumu kumweke tu mbele zako. "Yeye alisema jambo hilo, na litatimia." Mnaona? Mweke daima mbele zako. Hiyo ni kweli.

96 Nuhu alikuwa na saburi. Naam. Nuhu alikuwa na saburi halisi, ya kiungu. Mungu alisema, "Nitauangamiza ulimwengu huu kwa mvua," naye Nuhu akahubiri miaka mia moja na ishirini, hata hivyo. Subira tele. Hata umande haukushuka kutoka Mbinguni. Hakukuwa na kitu. Kulikuwa na mavumbi tu kama ilivyowahi kuwa, kwa miaka mia moja na ishirini, bali yeye alikuwa na saburi.

Halafu, Mungu hujaribu saburi yako. Hiyo ni kweli. Mungu huwajaribu.

Baada ya Yeye kumwambia Nuhu, sasa Yeye alisema, "Nuhu, ninataka uendelee na kuingia katika safina. Nitawaingiza wanyama humo ndani, nami ni—ninataka wewe uingie ndani. Panda huko ghorofani juu, sasa, kusudi upate kuangalia nje, dirisha la juu. Sasa, ninataka wewe uingie mle. Ninataka uwaambie watu hawa, 'Kesho, yale nilivyokuwa nikihubiri kwa miaka mia moja na ishirini, yatatukia.' Vema, shuka uende kule ukawaambie."

97 Ishara ya kwanza ilikuwa ni nini? Nuhu aliingia katika safina. Hakukuwa na mvua. Nuhu alijitayarisha, na kuvaa koti la mvua, na kila kitu, ili aweze kuangalia nje, mara kwa mara. Akawa tayari. Lakini kesho yake …

Ninaamini huenda aliiambia familia yake, na wakaza wanawe na hao wote, akasema, "Loo, jamani! Kesho mtaona jambo fulani ambalo hamjapata kuliona. Kwa sababu, mbingu nzima, itakuwa nyeusi. Na ngurumo na radi zitatokea. Ule upanga mkubwa wa Mungu utapasua mbingu. Atalihukumu kundi hili la wenye dhambi ambalo halikutuamini, kwa miaka hii mia moja na ishirini. Ninyi angalieni tu muone." Mnaona?

Baadhi ya wale waamini-nusu, unajua, wanaorandaranda huku wala kamwe hawaingii, mnajua. M—mngali mnao, mnajua. Basi wa—wakaja, wakasema, "Vema, huenda maskini yule mzee alikuwa anasema kweli, kwa hiyo tutaenda kule na tungoje siku chache, ama tungoje masaa machache asubuhi, basi tuone."

98 Kesho yake, badala ya wingu jeusi, hili hapa jua linachomoza kama lilivyofanya sikuzote. Nuhu akaangalia nje. Kasema, "Ala, hakuna wingu lo lote."

Jamaa huyo akaja, akasema, "A-ha, mimi nilijua ulikuwa mmoja wao. Mnaona, unarandaranda hapa karibu."

"Vema, samahani, bwana. Ha-ha. Labda mi—mi—mimi ninaninii tu, mwajua, ni ushabiki wangu tu, mwajua. Kwa namna fulani, mnaona. Ha-ha-ha."

Lakini, Nuhu, alikuwa na saburi. Kasema, "Kama haikuja leo, itakuwa hapa kesho." Kwa nini? Mungu alisema hivyo.

"Ni wakati gani alikuambia hilo, Nuhu?"

"Miaka mia na ishirini iliyopita. Nimefika umbali huu, kwa hiyo ninangojea tu hapa sasa." Mnaona jambo hilo? Baada ya kitambo kidogo …

Tunaona, Mungu alikuja umbali huu, akilingojea Kanisa, pia, bali litakuwako. Msiwe na wasiwasi. Yeye aliahidi jambo Hilo.

99 Nilingojea wakati huu wote kwa ajili ya ufufuo. Kutakuwako na mmoja. Usijali. Mungu aliahidi jambo hilo. Ngojeni tu kwa subira. Ukilala usingizi, hilo halita- … Huenda ukalala kidogo kabla halijatukia, bali utaamka wakati huo. Yeye aliahidi jambo hilo, mnaona. Kulala kidogo, mnaona, kile tunachoita usingizi wa mauti, mnajua. Tunachokiita mauti, usingizi mdogo tu, ama kulala mauti katika Kristo. Hakuna kitu kama kufa katika Kristo. Uzima na mauti havipo pamoja. Mnaona? Tunalala tu kidogo, usingizi mdogo ambao marafiki zetu hawawezi kutuamsha. Yeye Ndiye pekee anayeweza kuita. "Yeye ataita, nami nitamjibu," akasema Ayubu. Ayubu amekuwa amelala sasa kwa miaka elfu nne. Usijali. Yeye ata—ataamka. Usijali. Yeye angali anasubiri.

100 Nuhu alingoja. Siku ya nne ikapita. Hakuna mvua. Ni sawa. Litatukia.

Ninaweza kumsikia Mke wa Nuhu akija na kusema, "Baba, una haki-…?

"Usizungumze namna hiyo."

Alikuwa na saburi, maana alikuwa na imani. Naam, bwana. Alikuwa na nguvu. Alikuwa na maarifa ya kwamba Mungu alikuwa sahihi. Alikuwa na kiasi. Hakushikwa na hamaki, aseme, "Vema, sijui maana ya haya yote. Nimepoteza umaarufu wangu wote huko nje." La, la. "Watu hawanijali mimi tena. Nitaondoka niende huko na kuanza tena, upya tena." La, la. Alikuwa na saburi. Mungu aliahidi. Mungu atafanya jambo hilo. Mungu atalifanya, maana Mungu alisema hivyo.

101 Nami ninaweza kuona mwanawe akija, akisema, "Baba, mnajua…" Akalaza kwa mkono mvi zake ndefu, mnajua. Naye alikuwa na umri wa mamia ya miaka, mwajua, ameketi pale. Kasema, "Ninajua wewe ni mzee mzee. Ni—ninakupenda, baba. Lakini je! Ingewezekana kwamba ungekuwa umekosea kidogo?"

"Loo, la. La."

"Kwa nini?"

"Mungu alisema hivyo!"

"Vema, baba, hizi ni siku sita ambazo tumeketi hapa. Tumeketi hapa katika safina hii kubwa, ya kale iliyokauka tumeketi papa hapa. Na imetiwa lami kila mahali, ndani na nje. Nasi tumekuwa tukiijenga kwa miaka hii yote. Nawe ulisimama kule nje na kuhubiri, mpaka ukapata mvi na ukatoka upara. Na ndio wewe uko hapa sasa, ukijaribu kusema kitu *fulani*. Na watu wanacheka, na wanakutupia nyanya zilizooza na kadhalika kando yake. Ona basi hayo unayofanya. Mbona, unajua …"

"Uwe na subira, mwanangu."

"Una hakika?"

"Itanyesha!"

Mke wa mwanae akasema, "Baba, unajua…"

"Itanyesha!"

"Lakini tumekuwa miaka hii yote, tukingojea. Tumekuwa tukijitayarisha. Nawe ulituambia itanyesha, juma moja lililopita. Nasi tuko hapa ndani, na milango yote imefungwa, nasi tuko hapa ndani tukitembea tembea ndani hapa, na jua likichoma moja kwa moja kama kawaida."

"Lakini itanyesha!"

"Unajuaje?"

"Mungu alisema hivyo!"

102 Sasa tukiwa namna hiyo, tuitie. Lakini kama huko hivyo, usi—usijaribu kuitia. Haitafaa kitu. Haitafaa katika kuponya. Haitafanya kazi katika cho chote kile. Mnaona? Haina budi kushikamana na kitu kile kile ilichochanganywa nacho. Hiyo ni kweli. Huna budi kuitia. Saburi na ahadi ya Mungu. Naam, bwana. Nuhu aliamini jambo hilo. Naye alikuwa na saburi na Mungu, miaka mia moja na ishirini.

103 Musa, alikuwa na saburi na Mungu. Naam, bwana. "Musa, nimesikia kilio cha watu Wangu. Nimeona mateso yao. Ninashuka kuja kuwakomboa. Nitakutuma huko."

Na tofauti ndogo pale kati yake na Mungu, na Mungu akamwonesha utukufu Wake. Kasema, "Mimi hapa." Mara alipoona utukufu wa Mungu, unaona, akapata imani.

Kasema, "Hiyo ni nini mkononi mwako, Musa?"

Akasema, "Fimbo."

Akasema, "Itupe chini."

Ikageuka kuwa nyoka. Akasema, "Loo, jamani!" Akaanza …

Akasema, "Ichukue, Musa. Kama ninaweza kuigeuza kuwa Nyoka, ninaweza kugeuza tena."

A-ha! [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu — Mh.] Amina! Kama Mungu anaweza kunipa uhai wa kawaida, Yeye anaweza kunipa Uzima wa kiroho! Kama Mungu aliweza kunipa kuzaliwa kwa kwanza, angeweza kunipa Kuzaliwa mara ya pili! Amina! Kama Mungu aliweza kuuponya *huu*, kwa kuponya Kiungu, anaweza kuuinua tena kwa ajili ya utukufu Wake, katika siku ya mwisho. Hiyo ni kweli.

"Ninaweza kutupa kijiti hiki chini na kukifanya nyoka. Ninaweza kuigeuza tena ikawa fimbo. Ishike mkia."

Musa akanyosha mkono akaishika. Hiyo hapo, fimbo. Anaanza kuongeza maarifa basi. Mnaona?

"Mkono wako una nini, sasa, Musa?"

"Hakuna kitu."

"Uweke Kifuani pako."

"Vema. Vipi kuhusu …" Mweupe kwa ukoma. "Ee Bwana, angalia mkono wangu!"

"Urudishe kifuani pako, Musa."

Akaurudisha namna *hiyo*, ukageuka tu kama… Akaanza kuitia namna *hii*, basi, mnaona. Naam, bwana.

104 Akashuka akaenda kule. Na tofauti ya kwanza … Alishuka akaenda kule. Akatoka kule na kusema, "Bwana Mungu alisema, 'Waachilie watu Wangu waende.' Farao, ninataka ujue jambo hili. Nimekuja kama mwakilishi wa Mungu. Huna budi kunitii."

Farao akasema, "Kukutii? Je! unanijua mimi ni nani? Mimi ni Farao. Kukutii, mtumwa?"

Kasema, "Utanitii, la sivyo utaangamia. Utafanya lo lote utakalo." Kwa nini? Yeye alijua alichokuwa anazungumzia. Alikuwa na agizo. Alikuwa huko chini. Alizungumza na Mungu. Alikuwa na imani. Alijua mahali alipokuwa.

"Unataka nikutii? Ondoka hapa!"

"Nitakuonesha."

"Nioneshe ishara."

Akatupa fimbo chini; ikageuka ikawa nyoka.

105 "Mbona," akasema, "hicho kiinimacho chako rahisi cha uchawi! Njoo hapa kwa dakika moja. Njoo hapa, Yane, wewe na Yambre, tupeni fimbo zenu chini." Wakazitupa chini, nazo zikageuka zikawa nyoka.

Kasema, "Sasa, ewe kiinimacho duni, umeshuka ukaja hapa kwangu mimi, Mmisri, farao wa Misri. Nawe umekuja hapa na kiinimacho chako duni, mizaha yako," unajua, kusoma mawazo. Mnajua ninalomaanisha. Natumaini mnasoma habari zake. "Telepathia ama cho chote kile, mnaona, naam, unashuka unakuja hapa na hayo." Kasema, "Vema, tunaweza kufanya jambo lile lile unalofanya."

Musa alikuwa nini? Yeye hakusema, "Loo, Bw. Farao, na—nasikitika, bwana. Nitakuwa mtumwa wako."

La, bwana.

106 Alisimama kimya. Amina. Kaeni papo hapo. Mungu alisema, hakukuwa na shaka kabisa moyoni mwake, “Nyamazeni. Nitawaonesha jambo fulani.” Ukiisha kutimiza kabisa yale Yeye aliyosema ufanye, inaonekana kama kwamba mambo yameenda mrama, simama kimya, uwe na subira.

Musa alisema, “Unajua, nilipowekwa kwenye msingi huo, kulikuwa na saburi iliyowekwa juu pale, kwa hiyo nitangoja tu na nione kile Mungu atakachofanya.”

Hao hapo wale nyoka wa zamani, wakitambaa kote, wakipigiana mluzi, wakipuliziana wao kwa wao. Muda si muda unajua, Nyoka wa Musa akafanya, “Ng'au, ng'au, ng'au,” na kuwameza wote. Alikuwa na saburi.

> Hao wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya;
> Watapanda juu kwa mbawa kama tai.

Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Mnaona? Naam.

> Watapiga mbio wala hawatachoka, watakwenda kwa miguu wala hawatazimia.

Mnaona, mngojeeni tu Bwana. Iweni na saburi. Mnaona? Naam, bwana.

107 Ndipo Israeli walikuwa watolewe. Zile tofauti kuu zikaja, naye Musa akangojea.

Ndipo akaingia nyikani. Ni kama tu safari ya siku tatu au nne. Ni maili arobaini tu kutoka mahali alipovuka pale, ni pale pale ng'ambo ya mahali walipovuka tena. Lakini, Musa, huko jangwani, alingojea miaka arobaini. Saburi. [Ndugu Branham anacheka — Mh.] Amina. Hiyo ni kweli. Yeye alingojea miaka arobaini. Loo! Naam, bwana.

108 Nasi tunapaswa kuwa na subira sisi kwa sisi, pia. Mnaona? Wakati mmoja … Tunapata—tunakosa subira sana sisi kwa sisi. Tunafikiri hatuna budi kuwa kama Musa. Musa alikuwa na saburi na watu. Angalia, hilo ndilo lililowafanya wasivuke. Mnaona? Kama unajaribu kufanya jambo fulani …

Kama vile, nimejaribu kuufikisha Ujumbe huu kwenye Maskani, kuona ya kwamba kila mshiriki wa Maskani anakuwa Hiki. Ni vigumu kufanya hivyo. Nimejaribu kuwa na saburi; hii ni miaka thelathini na mitatu. Mnaona? Iweni na saburi. Wanawake wangali wanakata nywele zao, wangali vivyo hivyo. Lakini iweni tu na saburi. Mnaona? Iweni tu na saburi. Ngojeni. Yakubidi kungoja. Kama hunayo, usijaribu kujenga juu ya huu *hapa*. Uwe na saburi.

109 Hata wakati mmoja, wakati kundi lile la waasi lilipokosa saburi kabisa, walimfanya Musa afanye jambo baya. Lakini, hata hivyo, wakati ilipofikia kwenye hatua ya kudhihirisha mambo, Mungu alichoshwa na matendo yao. Yeye alisema, “Jitenge, Musa. Nitaua kundi lote lao, na kuanza upya.”

Yeye alijitupa katika pengo, na kusema, “Mungu, usifanye hivyo.” Nini? Saburi na watu waliokuwa wakimwasi.

Sijui kama tungeweza kufanya jambo hilo? Kama huwezi, usijaribu kujenga juu ya *huu*, maana hau—haubadiliki, mnajua. Hivyo ndivyo la kwanza lilivyochanganywa katika hili, na hivyo ndivyo inavyompasa kila mmoja wao kuchanganywa. Kama huninii, hufikii kimo hicho cha makao ya Mungu aliye hai, kama huna saburi, saburi, mmoja kwa mwingine. Vema.

110 Wana wa Kiebrania walikuwa na saburi. Hakika, walikuwa nayo. Mungu alikuwa amewaahidi, akawaambia, “Msisujudu sanamu yo yote.” Lakini walikuwa na saburi. Kasema, “Mungu wetu anaweza. Lakini, hata hivyo, hatuisujudii sanamu yako.” Saburi, wakijua jambo hili, ya kwamba Mungu atamfufua katika siku ya mwisho tena.

Maisha haya hayana thamani sana, hata hivyo. Mnaona? Mungu atakufufua tena katika siku za mwisho. Lakini ikifikia kusujudia sanamu, hatutaisujudia. Sasa, tutampa Kaisari yaliyo ya Kaisari, lakini, ikifikia ambapo Kaisari anamwingilia Mungu, Mungu ni wa kwanza.

“Mungu akasema, 'Msiisujudie sanamu hiyo.' Nami sitaisujudia. Mungu wetu anaweza kutukomboa. Kama hatukomboi, sitaisujudia sanamu hiyo.”

Kasema, “Vema, ile pale tanuru.”

“Vema,” akasema, “loo, nafikiri, itanesha sana usiku wa leo na kuizima.” Bali haikunyesha. Bado wana saburi.

111 Kesho yake asubuhi, walipoletwa mbele ya mahakama, huyo hapo Nebkadreza ameketi. Akasema, “Vema, vijana, mko tayari kunikumbuka kama mfalme wenu?”

“Hakika. Uishi milele, Ee mfalme.”

"Sasa sujudieni sanamu yangu."

"Loo, la."

"Vema, mtachomwa moto. Ninyi ni watu wenye hekima. Mna akili. Umekuwa msaada mkubwa kwetu. Mmekuwa baraka kwa ufalme wetu. Hivi hamwezi kuelewa mimi sitaki kufanya jambo hili? Lakini nimetoa tangazo hapa, na halina budi kutimizwa. Sitaki kuwatupa mle ndani. Loo, enyi watu, hivi kuna nini?"

"Najua jambo hilo linasikika sawa. Lakini, Mungu wetu anaweza kutukomboa. Lakini hata hivyo …" Nilikuwa na saburi.

Wakaanza kupanda ngazi. Wakaangaliana. "Ni sawa. Vema." Wana saburi. Walipiga hatua moja, Mungu hakuwako. Hatua mbili, Yeye hakuwako. Hatua tatu, hatua nne, hatua tano, ziliendelea tu, bado Yeye hakuwako. Naye akaingia moja kwa moja kwenye tanuru ya moto. Walikuwa na saburi. Lakini Yeye alikuwa pale. Mnaona? Moto wa kutosha tu uliwagusa, kuunguza kamba kutoka mikononi mwao na miguuni mwao. Na basi alipofika chini ya lile shimo, Yeye alikuwako. Mnaona? Walikuwa na saburi.

112 Danieli vivyo hivyo. Danieli alikuwa na saburi. Hakika. Yeye hangekata tamaa. La, bwana. Alifanya nini? Aliyafungua madirisha na kuomba, hata hivyo. Lilikuwa ni sharti la Mungu. Alikuwa na saburi. Alimngojea Mungu, akijua Mungu aliweza kutimiza Neno Lake. Wakamtupa kwenye tundu la simba, wakasema, "Tutawaacha simba wa kukule."

Akasema, "Hilo ni sawa." Alikuwa na saburi. Kwa nini? "Vema, nimemngojea Mungu wakati huu wote. Kama itanibidi kungojea miaka elfu chache zaidi, nitafufuka tena katika siku ya mwisho. Kwa hiyo, alikuwa na saburi, akangoja."

Paulo alikuwa na saburi. Bila shaka alikuwa nayo. Angalia yaliyompasa Paulo kufanya. Nena kuhusu subira!

113 Vipi kuhusu wapentekoste? Mradi tu wana agizo, "Ngojeni mpaka," mnaona, "ngojeni mpaka mtakapovikwa Nguvu." Muda gani? Hawakuwa na swali, itakuwa muda gani? Walipata jibu tu, "Ngojeni mpaka."

Walipanda wakaenda kule na kusema, "Vema, jamani, labda dakika kumi na tano tangu sasa Roho Mtakatifu atashuka juu yetu nasi tutapokea huduma yetu." Dakika kumi na tano zikapita, hakuna mtu. Siku moja ikapita, la; mbili, tatu, nne, tano, sita, saba.

Baadhi yao huenda walisema, "Aisee, hivi hudhani tayari tumempata?"

"La, la, la, la." Ndivyo ilivyo. La. Hiyo ni kweli.

"Afadhali tutoke, enyi jamani." Ibilisi akasema, "M—m—mnajua mmepata kile mlichotaka tayari. Endeleeni, anzeni huduma yenu."

"La, la, la. Hatujampata, bado. Kwa sababu, Yeye alisema, 'Kutakuja, kile kitakachotukia katika siku za mwisho: Kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha ngeni nitasema na watu hawa, na hii ndiyo ile Raha niliyosema,' mnaona, Isaya 28:19." Kasema, "Hii ni—hii Ndiyo, u—utampata wakati… Mbona, tutajua wakati atakapokuja. Tutajua wakati itakapotukia. Tutajua, 'Ahadi ya Baba.'" Pale alingojea kwa siku tisa. Na ndipo katika siku ya kumi, "Tulikuwapo." Walikuwa na saburi, kungoja.

114 Sasa, kama una saburi ya aina hiyo, Mungu akiisha kukupa ahadi na unaiona katika Biblia, "Ni yangu," basi ngoja. Basi, kama una saburi ya aina hiyo, itie katika imani yako. Basi mnaona jinsi unavyopanda juu sasa? Unafikia hapa juu kabisa sasa. Vema. Mkono wa saa unazunguka uso mzima, pia, sivyo? Vema. Vema. Tia hii katika imani yako.

Daima ukimweka Yeye mbele zako, ukikumbuka, Yeye Ndiye aliyeahidi. Haikuwa ni mimi, niliyeahidi. Haikuwa ni mchungaji, aliyeahidi, Ndugu yetu Neville. Haikuwa ni mhudumu mwingine, aliyeahidiwa. Haikuwa kasisi fulani ama papa. Haikuwa ni mtu ye yote duniani. Mungu ndiye aliyeahidi, na Mungu anaweza kutimiza kila kitu alichoahidi. Vema. Kama una aina hiyo ya imani, kujua ya kwamba Mungu aliahidi jambo hilo! Unasema, "Ndugu Branham, mimi ni mgonjwa. Ninahitaji uponyaji vibaya sana." Ukubali. Ni karama uliyopewa, naam, bwana, kama unaweza kuamini. "Vema," unasema, "ninaamini." Basi sahau jambo hilo. Hivyo tu. Yote yamekwisha. Mnaona?

115 Kuwa na saburi, kama una saburi. Kama huna, unaporomoka kutoka kwenye Jengo hili hapa, mnaona. Litaangusha hayo mengine yote, jambo hilo moja. Huna budi kuwa nayo. Usiliongezee, kwa sababu, litavunjavunja jengo lako kama huna saburi, kama huna nguvu za kuongeza kwenye imani yako unayosema unayo. Na kama huna imani yo yote, na unajaribu kuweka nguvu juu yake, itavunjilia mbali imani yako. Mnaona? Unasema, "Vema, sasa, ngoja kidogo. Labda haya yote ni makosa, hata hivyo. Labda Mungu si Mungu. Labda hakuna Mungu." Mnaona, itavunja kitu hicho vipande viwili. Mnaona?

116 Lakini kama una imani halisi, basi weka nguvu halisi juu yake, halafu maarifa halisi, halafu kiasi halisi, halafu saburi halisi. Mnaona? Unapanda moja kwa moja juu kwenye njia sahihi. Vema.

Ya tano, tia utauwa. Loo, jamani! Kutia utauwa. Uungu maana yake nini? Niliangalia katika kamusi nne ama tano wala hata sikuweza kupata maana yake. Hatimaye, nilikuwa kule chini kwa Ndugu Jeffery, tukalipata katika—katika kamusi fulani. Utauwa maana yake ni "kuwa kama Mungu." Loo, jamani! Baada ya kupata imani, nguvu, maarifa, kiasi, saburi, basi uwe kama Mungu. Whiu!

Unasema, "Siwezi kufanya hivyo, Ndugu Branham." Loo, naam, unaweza.

Hebu niwasomee tu Maandiko machache hapa, kwa dakika moja. Mathayo 5:48. Tutachukua hili kisha tuone vile linavyosikika, Mathayo 5:48, na tuone kama unapaswa kuwa kama Mungu. Mnajua Biblia inasema, "Ninyi ni miungu." Yesu alisema hivyo. Kwa nini? Nguvu zote, mambo yote yaliyo katika Mungu, yako ndani yako. Mathayo 5:48, "Iweni…" Yesu akinena, katika zile heri.

> *Kwa hiyo iweni p-e-r-f-e-c-t*, (Hiyo ni nini?) *Mkamilifu, kama vile Baba yenu … aliye mbinguni alivyo mkamilifu.*

Umepanda sana juu huku sana, kabla hujaambiwa kufanya jambo hilo. Mambo haya yote hayana budi kuongezwa kwanza. Ndipo utakapofika hapa juu, Yeye amekutaka sana uwe mkamilifu, utauwa, wana na binti za Mungu. Hiyo ni kweli. Ni mambo mangapi ningeweza kusema kwenye mstari huo!

117 Hebu na tufungue Waefeso 4, na tuone hapa ni kitu gani, katika Kitabu cha Waefeso, kinasema kuhusu jambo hili, pia, kuhusu jinsi tunavyopaswa—jinsi tunavyopaswa kufanya. Waefeso, mlango wa 4, na kuanzia na kifungu cha 12. Waefeso 4, na kuanzia na kifungu cha 12. Vema. Hebu tuanzie hapa kwenye kifungu cha 11.

> *Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii;…*

Mnakumbuka jana usiku? Usijaribu kuchukua huduma ya mtu mwingine. Mnaona?

> *…na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu;*

"Kwa kukamilishwa kwa Mungu"? Je! haisomeki hivyo? [Kusanyiko linasema, "La." — Mh.] Ukamilifu wa nini? ["Watakatifu."] Watakatifu ni akina nani? Waliotakaswa. Amina. Hao walianzia hapa chini.

> *…kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke* (huduma ya Yesu Kristo), *hata mwili wa Kristo ujengwe* (kwa kuhuisha, kuujenga, kuhuisha): mpaka…

> *Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na . . . kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye uhakikisho*, (loo, jamani), *hata kufikia kwenye cheo che kimo cha utimilifu wa Kristo:*

118 "Ukamilifu," inahitaji uungu. Inakubidi kuongeza kwenye imani yako, utauwa. Unaona, unaanzia hapa chini, ukiwa na nguvu. Kisha unaenda kwenye maarifa. Halafu unaenda kwenye kiasi. Halafu unaenda kwenye saburi. Sasa uko kwenye utauwa. Utauwa! Loo, jamani! Wakati wetu unakwisha. Hebu tuone. Bali unajua maana ya utauwa. Mmeimba wimbo huu:

Kufanana na Yesu, kufanana na Yesu,
Duniani ninatamani kufanana Yeye;
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani kwenda Utukufuni
Ninaomba tu kufanana Naye.

Huo ni utauwa. Alipopigwa kofi upande mmoja wa uso, aligeuza upande huo mwingine. Aliponenewa vibaya, Yeye hakuongea. Hakughadhabikia mtu. Mnaona? Utauwa, daima akitafuta jambo moja, "Daima ninafanya lile linalompendeza Baba." Mnaona? Naam, bwana. Daima. Huo ni utauwa. Mnaona?

119 Ukiisha kuja kutoka *hapa*, mpaka *hapa*, mpaka *hapa*, mpaka *hapa*, mpaka *hapa*, mpaka *hapa*, sasa unakuja kwenye kimo kikamilifu sasa cha Mwana wa Mungu. Lakini huna budi kuwa na *hii*, pamoja *haya* yote, wala hata huwezi kuanza mpaka umepata *hii*.

Sasa kumbukeni yule ndege mweusi mwenye manyoya ya tausi. Msimsahau. Mnaona? Usijaribu kuongeza hilo mpaka umezaliwa mara ya pili kweli. Maana, wewe, haitafaa kitu, nawe—nawe huwezi kulifanya hilo lifanikiwe. Itafikia *hili* ama *hili* hapa, itaporomoka mahali fulani.

120 Lakini unaposhuka kwenda chini *hapa*, hua halisi aliyezaliwa mara ya pili, basi hutii cho chote. Inajitia kwako, mnaona, inapanda, vema, ikifikia kwenye utimilifu sasa. Vema.

Halafu, la sita, hebu na tuongezee, Biblia ilisema hapa, kutia upendo wa ndugu…upendano wa ndugu. Sasa, hilo ni jambo zuri sana, papa hapa, la sita, saba. Vema. Vema. Kuongezea upendano wa ndugu. Vema. Tutakapofikia jambo hilo, upendano wa ndugu, jiweke mwenyewe mahali pake, kwenye jambo hilo. Sasa unasema …

“Ndugu yangu alinikosea,” Petro alisema. “Je! nimsamehe,” akasema, “mara saba kwa siku?”

Akasema, “Sabini mara saba.” Mnaona?

Upendo wa ndugu. Sasa, unaona, kama ndugu ameenda kombo kabisa, usikose kumvumilia. Mnaona? La. Mnaona? Kuwa mwema kwake. Nenda, hata hivyo.

121 Mtu fulani alisema, si muda mrefu uliopita, alisema, “Unawezaje kuamini mambo haya jinsi unavyoyaamini, na bado uende kwa Waassemblies, na Oneness, na hao wengine wote?” Weka, mnaona, upendano wa ndugu. Mnaona? Mnaona? Ukitarajia, siku moja, unaona; ukimvumilia, mnaona; mwenye kiasi, ukistahimili pamoja naye; maarifa, kufahamu yale anayoamini, kumbukeni, liko moyoni mwake, hivyo ndivyo ilivyo; nguvu, katika nafsi yako wewe mwenyewe, kuziachilia ziambatane na huruma, upole, kwake; ukiwa na imani ya kwamba siku moja Mungu atamwingiza. Mnaona?

Upendano wa ndugu, jambo la saba. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. [Ndugu Branham anagonga ubaoni mara saba — Mh.] Mnaona, jambo la saba. Halafu, sasa, unakuja.

Jambo linalofuata, basi, tia kupendana, ambao ni upendo. Huo ndio jiwe la kifuniko. Moja ya siku hizi, kanisani …

122 Sasa, tafadhali, hebu na ijulikane kwenye kanda, na po pote pale tena, sifundishi jambo hili kama fundisho, kile ninachotaka kusema sasa. Bali ninataka tu kuwaonesha ya kwamba, kwa msaada wa Mungu, ni jambo gani hasa, ya kwamba, Biblia ya kwanza ambayo Mungu alipata kuandika ilikuwa ni ile Zodiaki mbinguni. Inaanza na bikira. Inaishia kwa Leo yule simba. Na nitakapofikia Muhuri wa Sita na wa Saba, mtaona, wakati Muhuri ule mwingine ulipofunguliwa, ile alama ya Zodiaki ya mahali hapo ilikuwa ni kaa, yule samaki aliyekingama. Na huo ndio wakati wa kansa tunaoishi sasa, umefunuliwa. Na jambo la pili ule Muhuri uliporaruka, ulimfunua Leo yule simba, kule Kuja kwa pili kwa Kristo. Yeye alikuja, wa kwanza, kwa bikira; Yeye anakuja, halafu, Leo yule simba. Nitaleta hili kwa …

Sasa, sijui kama nitakuwa na wakati asubuhi ya leo. Nitafanya vizuri niwezavyo, kuwaonesha ya kwamba hatua hizi zimo kwenye mapiramidi, barabara kabisa, Biblia ya pili aliyoandika Mungu. Henoko aliziandika, na kuziweka kwenye piramidi.

123 Na ya tatu, Mungu daima hukamilishwa katika ya tatu, ndipo basi Yeye akalifanya Mwenyewe kuwa Neno Lake.

Hapa, sasa, kumbukeni, katika piramidi… Nadhani wengi wenu enyi askari na kadhalika mlifika Misri. Ile piramidi haina kifuniko juu yake. Haijawahi kamwe kuwa nacho. Lile—lile Jiwe la Scone, na cho chote kile walicho nacho, lakini bado…

Kama una noti ya dola mfukoni mwako, hebu iangalie noti hiyo ya dola, na utaona ya kwamba, kwenye upande wa kuume, ina tai aliyeshika bendera ya Marekani. Na ilisema, muhuri “wa Marekani.” Upande huo mwingine, ina piramidi iliyo na jiwe kuu la kufuniko na jicho la mwanadamu. Inasema upande huu, “Muhuri mkuu.” Vema, kama hili ndilo taifa kuu, kwa nini muhuri huu mkuu usiwe muhuri wake wa taifa? Mungu anawafanya washuhudie, haidhuru wataenda wapi.

124 Nilikuwa nikizungumza na daktari fulani wakati mmoja, naye alikuwa akinikosoa vikali sana, kuhusu uponyaji wa Kiungu. Nilikuwa nimesimama barabarani. Akasema, “Bw. Branham, unawachanganya tu watu.” Kasema, “Hakuna uponyaji, ila tu kwa madawa.”

Ikawa kwamba niligeuka, nikaangalia ishara yake kwenye gari lake, ilikuwa na ile nyoka kwenye mti. Nikasema, “Ni heri uondoe ishara hiyo kutoka kwenye gari lako, basi, maana alama yako mwenyewe inashuhudia ya kwamba Mungu ni mponya.”

Daktari halisi anaamini jambo hilo. Hao ni watu madaktari wanaojifanya. Naam, bwana. Yule nyoka juu ya mti! Musa alimwinua nyoka juu ya mti. Alisema, “Mimi ni Bwana ninayeponya magonjwa yako yote.” Nao wakamwangalia huyo nyoka, kwa ajili ya uponyaji wa Kiungu. Na hata hivyo wanashuhudia dhidi yake; hata hivyo ishara yao wenyewe inashuhudia dhidi yao. Whiu!

125 Hapa, taifa letu, wakisema mambo wanayosema, na kuyafanyia mambo haya mzaha, na pesa zao wenyewe, fedha yao, zinashuhudia ya kwamba muhuri wa ulimwengu mzima ni Mungu. Mnaona jicho hilo linalosimama pale juu ya hiyo, juu ya hiyo noti ya dola? Huo ndio ule muhuri mkuu.

Kamwe haukuwa umewekwa umewekwa juu ya piramidi. Wasingeweza kuelewa ni kwa nini. Lile Jiwe la kufunika lilikataliwa, Kichwa, Kristo. Lakini litakuja, siku moja.

126 Sasa, katika kujenga, ule wema… Kujenga mnara huu mkuu, kujenga kimo hiki, mnaona, inaanzia na jiwe la msingi; imani, nguvu, maarifa, kiasi, saburi, utauwa, upendano wa ndugu. Sasa hilo linafanya nini? Ndipo wanangojea Jiwe la Kuweka Juu, ambalo ni upendo, kwa maana Mungu ni upendo. Na Yeye anatawala, Naye ndiye nguvu za kila moja ya vitu hivi. Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

Papa *hapa* ndani, papa hapa ndani, unaona nina, hapa katikati, kazi hizi zote hapa, na hapa mawimbi haya madogo yanakuja. Ni kitu gani hicho? Roho Mtakatifu akishuka, kupitia kwa Kristo, mnaona. Roho Mtakatifu! Roho Mtakatifu yuko juu ya yote *haya*, akiunganisha hili pamoja, akijenga (nini?) Kanisa kamilifu, kwa ajili ya Jiwe la Kufunika kulifunika.

Ni kitu gani kimefanyika tena? Imejidhihirisha kupitia katika Nyakati Saba za kanisa, na wale wajumbe saba wa Kanisa.

127 Ilianzia *hapa* nyuma. Kanisa lilianzishwa wapi kwa mara ya kwanza? Kanisa la Kipentekoste lilianzishwa wapi kwanza? Na Mtakatifu Paulo, huko Efeso, nyota ya Wakati wa Kanisa la Efeso, Efeso.

Wakati wa pili wa Kanisa ulikuwa ni Smirna. "Nguvu." Ireneo, yule mtu mashuhuri aliyeishikilia Injili ya Paulo.

Wakati uliofuata wa Kanisa ulikuwa Pergamo, ambaye alikuwa ni Martin. Martin alikuwa ndiye mtu mashuhuri aliyeendelea. Paulo, Ireneo, Martin.

Ndipo huko Thiatira akaja Columba. Mnakumbuka? Hili hapa, limechorwa papo *hapo*. Columba. Baada ya Columba … Zile Nyakati za Giza zikaingia mle.

Ndipo ukaja wakati wa Sardi, ambao maana yake ni mauti. Luther. Haleluya! Vipi basi? Ni nini kilichofuata baada ya Sardi, Luther?

Ndipo ikaja Filadelfia. "Utauwa." Wesley, utakatifu! "Wenye haki wanaishi kwa imani," Luther alisema. Utakaso kupitia kwa Wesley.

Ndipo ukaingia upendano wa ndugu, kupitia Laodikia. Nasi tunaamini ule ujumbe mkuu wa kule kutokea kukuu mara ya pili kwa Eliya, katika siku hizi za mwisho, kutaifunika nchi.

128 Haya basi, Nyakati Saba za Kanisa, hatua saba. Mungu akilijenga Kanisa Lake, ni kama mtu mmoja katika mtu binafsi, katika Nafsi Yake Mwenyewe. Utukufu, Nguvu za Mungu, zikishuka kupita hii, zikilishikamanisha pamoja. Kwa hiyo, Wapentekoste waliowaacha Waluteri, waliowaacha Wawesley na kadhalika, hawajui kile wanachonena. Mnaona, wao waliishi katika sehemu hii ya hekalu. Hivyo ndivyo ilivyo, watu fulani wanaweza kupanda juu kiasi hicho kisha wakaporomoka. Lakini kuna sehemu iliyo halisi ya hao, inayoendelea kulijenga jengo hilo lipande. "Nitarudisha," asema Bwana.

Mnakumbuka ule *Mti wa Bibi-arusi?* Mnakumbuka mahubiri juu ya *Mti wa Bibi-arusi?* Waliula ukaisha, bali Yeye aliupogoa matawi. Wakaweka matawi ya kimadhehebu; Yeye akayapogoa. Wakainua kanisa lingine, matawi ya kimadhehebu; akayakata. Bali moyo wa mti huo uliendelea kukua. "Na katika wakati wa jioni kutakuwako Nuru." Mnaona? Hapo ndipo Kristo alipokuja, Roho Mtakatifu. Yesu anashuka na kuketi Mwenyewe kama Kiongozi wa Kanisa basi, Naye atalifufua Kanisa hili, likiwa ni Mwili Wake Mwenyewe. *Kule* ndani ndiko kuliko na Mwili.

Na jinsi ambavyo Mungu anatutarajia sisi kama watu binafsi kukua, jinsi ambavyo amelikaza Kanisa Lake. Kila wakati wa Kanisa, unakuwa Kanisa moja kubwa. Mnaona?

129 Watu *hawa* hawatakiwi kuwa jinsi watu hawa walivyo. *Hawa* hawakutakiwa kuwa jinsi *hawa* walivyokuwa. Mnaona? Lakini Yeye alileta Kanisa Lake namna ile ile. Yeye alilijenga Kanisa La—Lake namna ile ile anavyowajenga watu Wake. Ndipo Petro anasema hapa, kwanza, mambo saba: imani, nguvu, (mnaona, kwenda juu), maarifa, kiasi, saburi, utauwa, upendano wa ndugu, tieni na upendano wa ndugu, na kisha upendo wa Mungu. Roho Mtakatifu, Kristo katika utu wa Roho Mtakatifu, anashuka juu yako, katika ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu, nawe una nguvu hizi zote zimetiwa muhuri ndani yako. Ndipo, Mungu anaishi katika maskani, inayoitwa Jengo, maskani hai ya makao ya Mungu aliye hai.

130 Mtu anapokuwa na vitu vya namna hii, basi Roho Mtakatifu huja juu yake. Hata ingekuwa, ungeweza kunena kwa lugha, unaweza kuiga karama yo yote aliyo nayo Mungu. Unaweza kufanya hivyo. Lakini mpaka nguvu hizi *hapa* ziingie ndani yako, bado ungali uko mbali na ule msingi halisi na wa kweli wa imani. Lakini wakati nguvu hizi zinapokua ndani, nawe unatia hiyo kwenye hiyo, basi wewe ni mnara hai. Wewe ni sanamu hai, inayotembea.

Lakini, unajua, ka—kafiri, wanasujudia mbele ya sanamu fulani, mungu wa kuwazia. Na katika njia ya kimawazo wanaamini ya kwamba mungu huyo wa kuwazia anazungumza nao. Huo ni ukafiri. Huo ni Urumi. Wanasujudia mbele ya watakatifu wa kila namna na cho chote kile. Nao wana akina Mtakatifu Cecelia, mungu wa nyumbani, na vikorokoro vingi sana mbalimbali namna hiyo. Wanaisujudia hiyo, na kwa kweli wanaamini hivyo katika njia ya mawazo. Ni—ni mfano wa jinsi gani, wa Mungu wa kweli aliye hai.

131 Lakini wakati sisi, si kwa njia ya kimawazo, bali tunaanguka kifudifudi mbele ya Mungu aliye hai, nguvu zilizo hai, maarifa hai, saburi hai, utauwa hai, Nguvu hai zitokazo kwa Mungu aliye hai, zinamfanya mtu aliye hai kuwa sanamu hai katika kimo cha Mungu. Yeye anafanya nini? Mambo yale yale aliyofanya Yesu; akitembea vile vile alivyotembea, akifanya mambo yale yale aliyofanya. Kwa sababu, si jambo la

kuwazia. Kuna uhalisi unaothibitisha.

Mnaona ninalomaanisha? Mnaona jinsi nguvu hizi, vifaa hivi vya ujenzi, vinavyolingana na wale wajumbe wa Kanisa, pamoja na nyakati za Kanisa? Sasa, moja ya siku hizi, tutachukua kila moja ya maneno haya, na kuyachambua, na kuonesha ya kwamba inathibitisha jambo hili. Yote yanaambatana. Hakika. Mnaona? Loo, jamani! Hilo ni la ajabu jinsi gani, mnaona, kuona vile—vile inavyokuwa.

132 Sasa, hiyo ndiyo Nyumba ambamo Mungu anaishi; si jengo lenye kengele kubwa juu yake, na mnara mrefu. Mnaona? "Lakini Mwili uliniwekea tayari," Mwili ambao Mungu anaweza kuishi ndani yake, Mungu anaweza kutembelea, Mungu anaweza kuona nao, Mungu anaweza kuzungumza humo, Mungu anaweza kufanya nao kazi. Amina! Chombo kilicho hai, Mungu, Mungu akitembea kwa miguu miwili, ndani yako. Utukufu! "Hatua za mwenye haki zinaongozwa na Mungu," Mungu akitembea ndani yako. "Kwa kuwa ninyi ni barua zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote." Na kama Uhai ulio ndani ya Kristo ukiwa ndani yako, utaleta maisha aliyokuwa nayo Kristo.

133 Kama ambavyo nimekuwa nikisema sikuzote. Toa utomvu katika mpichi, na kama ungeweza kuuhamisha, kwa utiliaji, katika mtofaa, mtofaa ungezaa mapichi. Hakika. Utazaa bila shaka. Haidhuru matawi yakoje, yana utomvu wa mtofaa ndani yake, mnaona, ama mti wo wote ule. Mnaona? Kutoa uhai wake kutoka kwenye mtofaa, utoe wote, na uutie u—utiliaji wa utomvu, na kuunyonya kutoka katika mpichi uuhamishie kwenye mtofaa. Inakuwaje? Hautazaa mapichi tena. Mnaona? La, bwana. Hautazaa. Kama uhai wa mpichi ukiingia katika mtofaa, hasa, hautazaa tofaa tena. Utazaa mapichi, mnaona, mnaona, kwa sababu una uhai ndani yake.

134 Vema, hebu utuchukue sisi, ambao si kitu ila mtango-mwitu, kichwa kigumu, mnaona, wala sisi hatuna kitu, kwa kuwa sisi sote tumekufa katika dhambi na makosa. Sote tuko katika hali za namna hii. Halafu sisi, sisi wenyewe, tunaweza kujinyenyekeza, tujisalimishe, mpaka Mungu atakapochukua mrija wake wa utiliaji, Jina la Yesu Kristo, maana, "Hakuna Jina lingine chini ya Mbingu ambalo mwanadamu anaweza kuokolewa kwalo," na kuuhamisha Uhai wa Kristo ndani yetu. Ndipo tuna imani ya namna hii, imani aliyokuwa nayo Kristo. Na imani ya Kristo haikuwa na msingi wake katika hao Mafarisayo, wala Masadukayo, wala katika vyungu vyao, mabirika, na sufuria, na kutawadha kwao. Iliwekwa msingi kwenye Neno la Mungu, amina, sana sana, mpaka Kristo akawa hilo Neno, Neno lilifanyika mwili. Ndipo tunapoweza kuwekewa kwa wingi sana Nguvu Zake, hata tupate kufia mawazo yetu wenyewe, na imani yetu inakuwa imani halisi, haleluya, ndipo Uhai wa Kristo unawekwa ndani yetu. Tunakuwa viumbe hai vya Mungu, makao ambapo Roho Mtakatifu anaweza kutuma miali ya baraka Zake za upendo kupitia humo, ndipo tunakuwa katika kimo cha Kristo.

135 Yesu alisema, "Je! haikuandikwa? Mmenihukumu Mimi, nikisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.' Hivi haikuandikwa, ya kwamba, 'Ninyi ni miungu.' Hivi torati yenu yenyewe haisemi hivyo?" Kama Musa, kama Eliya, kama wale manabii walioishi karibu sana na Mungu, mpaka Mungu akajihamishia tu Mwenyewe akaingia ndani yao kabisa. Nao wakanena, si hao wenyewe, bali Mungu. "Msiwazie mtakayosema, maana si ninyi mnaonena. Ni Baba akaaye ndani yenu; Yeye ndiye anayenena." Maneno Yake si yake mwenyewe, maana, uhai wake, yeye amekufa.

136 Kama ukifa, ukitoa damu ndani ya mtu, unamhifadhi asioze. Shida yake ni kwamba, wengi wao hawajawahi kuhifadhiwa. Ukitoa damu kutoka kwa mtu, ameisha kufa. Basi jambo pekee unalofanya ni kumrudishia damu nyingine mwilini mwake; ataishi tena. Ulitoa damu.

Na sasa tunaweka Damu ya Yesu Kristo ndani, mnaona, na hiyo inaleta imani ya Yesu Kristo, nguvu za Yesu Kristo, maarifa ya Yesu Kristo, kiasi cha Yesu Kristo, saburi ya Yesu Kristo, utauwa wa Yesu Kristo, upendano wa ndugu wa Yesu Kristo, na upendo wa Mungu, ambao ni Yesu Kristo. Yeye ndiye Kichwa kinachokutawala. Na miguu yako ndiyo msingi, imani. Amina! Kutawaliwa na Kichwa, kuchukua…? … Haya basi. Huyo hapo mtu mkamilifu wa Mungu, anapokuwa na sifa hizi.

137 Halafu, Mungu, akiwakilisha Kanisa Lake kama Bibi-arusi, mwanamke. Mungu huwakilisha Kanisa Lake kama Bibi-arusi. Na jinsi anavyomjenga kila mtu binafsi kuwa mwanawe, kuingia katika Bibi-arusi huyo, pia amemleta Bibi-arusi kupitia katika nyakati hizi, [Ndugu Branham anagongagonga kwenye ubao wake wa chaki mara saba—Mh.] mpaka atakapolifikisha Kanisa hili moja kamilifu *humu*.

Miguu yangu inatembea. Kwa nini? Kwa sababu kichwa changu kinasema hivyo. Sasa, haiwezi kusogea kama mkono wangu, kwa maana ni miguu yangu. Luther hawezi kufanya mambo yale tuliyofanya, wala Wamethodisti, kwa sababu wao walikuwa ni kitu kingine. Mnaona? Miguu husogea kwa maana kichwa kinasema hivyo. Wala kichwa kamwe hakisemi, "Sasa, enyi miguu, mwe mkono. Sikio, unakuwa macho." Mnaona?

Lakini, kila wakati, Mungu ameweka mambo haya katika Kanisa Lake, na kulifanya kwa mfano kwa kuonesha ya kwamba kila mtu binafsi ana hizi, ana sifa hizi. Na *Hiki*, kitakapokamilika, ndilo Kanisa la Mungu linalokwenda kwenye Unyakuo. Na mtu huyu, hapo anapokakamilishwa, ndiye mtumishi wa Mungu, katika Kanisa la Mungu, atakayekwenda kwenye Unyakuo. Utukufu! Mnaona ninalomaanisha? Haya basi.

Hilo ndilo jambo kamili.

138 *Huyu* hapa anakuja mtu, Paulo, akiweka msingi. Ireneo alianza kumimina *hiki* juu yake. Anayefuata akamimina *hiki*. Huyo mwingine akamwaga *hiki*. Mwingine *hii*, na *lile*, na *lile*, na kuendelea moja kwa moja mpaka inafikia kwenye wakati wa mwisho. Lakini ni kitu gani? Ni Roho yule yule.

Roho yule yule anayeishi ndani yangu, anasema, "Ninyi mikono, chukueni kasha lile." Roho yeye yule anasema, "Enyi miguu, tembeeni." Mnaona ninalomaanisha?

Ndipo, kimo chote cha utu wako kinatawaliwa na kuongozwa na mambo haya, bali hakiwezi kutawaliwa kabisa mpaka kitakapopata sifa hizi kwa utimilifu.

139 Je! Ulipata kusikia jambo hili? Sasa hebu niwaambie jambo hili. Na mweke kabisa … Wekeni hili kwenye sikio lenu la kusikilizia. Mnaona? Mnyororo una nguvu sana kwenye kiungo chake kilicho kidhaifu sana. Hiyo ni kweli. Huna nguvu zaidi kuliko kiungo chake kilicho kidhaifu sana.

Haidhuru *hizi* zimejengwa kwa nguvu vipi, *hiki* kimejengwa imara; kama kina kiungo kidhaifu, hapo ndipo utakatikia. Wala hakina nguvu kuliko hicho kiungo chake kilicho kidhaifu sana. [Ndugu Branham anarejea kwenye mchoro wake wa uboani—Mh.] Sasa kama unaninii, unasema una *hii, hii, hii*, huna *hii*, hapo ndipo inapovunjikia. Kama una *hii*, wala huna *ile*, kitavunjikia papo hapo. Una *hii*, wala huna *ile*, kitavunjika. *Hii*, na huna *hii*, kitavunjika. *Hii*, wala huna *hii*, itavunjika. Mnaona? Na kama huna … Wala huwezi kuwa na *hii* bila ya kuwa na *hii*.

Kwa hiyo wakati unapojisalimisha utu wako wote, ndipo Roho Mtakatifu anajimimina tu kupitia kwako, katika nguvu hizi, ndipo wewe ni maskani iliyo hai. Ndipo watu wanaangalia na kusema, "Yule ni mtu aliyejaa nguvu, maarifa (anaamini Neno), kiasi, saburi, utauwa, upendano wa ndugu, amejaa upendo wa Roho Mtakatifu. Mnaona, huyo hapo, akienda kote." Ni kitu gani? Kimo ambacho wasioamini wanaweza kuangalia na kusema, "Huyo hapo Mkristo. Huyo hapo mtu, ama mwanamke, anayejua kile wanachonena. Hujapata kuona mtu mwema kuzidi, mpole kuzidi, mwenye utauwa kuzidi." Umetiwa muhuri. Muhuri unaonyesha pande zote mbili. Kama unaenda ama unakuja, mnaona muhuri vile vile tu. Haya basi. Mnaona? Wakati mwanamume ama mwanamke anapokuwa na hii, basi Jiwe la Kifuniko linashuka na kuwatia muhuri katika Ufalme wa Mungu, ambao ni Roho Mtakatifu.

140 Ndipo Neno, likishuka kutoka *Hapa*, linajidhihirisha Lenyewe kupitia kila moja ya asili hizi, unaona, na kumfanya Mtu huyu aliyekamilika maskani ya Mungu aliye hai, mfano wa Ukristo unaotembea, ulio hai. Kile alichokuwa Kristo, ndicho walicho watu hawa, kwa maana Uhai Wake umo ndani humu. Wamo katika Kristo. Na uhai wao umekufa na kufichwa katika Kristo, kwa njia ya Mungu, na kutiwa muhuri mle ndani na Roho Mtakatifu. Wakorintho wa Kwanza 12. Hiyo ni kweli. Mnaona? Unajihesabu kwamba umekufa, basi umezaliwa kwa imani. Na, wewe, nguvu na mambo haya yanaongezwa kwako mpaka unakuwa mfano mkamilifu ulio hai wa Mungu. Hilo ni la ajabu? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.]

141 Na halafu Mungu, kupitia jambo hilo, ameleta pia Nyakati Saba za Kanisa, kuonesha zile hatua saba ambazo Yeye alileta, akimjenga mtu Wake binafsi kwa sura Yake, Yeye amejenga Kanisa lote katika sura Yake. Na kwenye ule ufufuo, Mwili huu mzima utafufuliwa kuishi Naye milele, kwa maana ni Bibi-arusi. Mnaona? Kwa hiyo hicho kinaingia katika kila wakati, kila wakati unaokuja.

Na kuna mengi zaidi yanayohitajika, kumbuka. Unakumbuka yale Paulo aliyosema hapa katika Waebrania 11? Hebu niwasomeeni tu jambo fulani hapa kabla hatujafunga, kwa dakika moja tu. Na ndipo ninyi… Kwa namna fulani linakufanya kidogo ujisikie wa kigeni wakati mimi… sikuzote, ninaposoma jambo hili. Nitafungua Waebrania 11, na nitaanzia na kifungu cha 32.

*Nini tena, nami niseme nini tena? Maana wakati usingenitosha kuleta habari za Gideoni, ... na Baraka, na ... Samsoni, na ... Yeftha; …Daudi na Samweli, ... na za manabii;*

*Ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga kinywa cha simba,*

*Walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga. Walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza ... majeshi ya wageni.*

*Wanawake walipokea wafu wao waliofufuliwa: … wengine walipitia kwenye maumivu, waliumizwa vibaya, wasikubali ukombozi; ili wapate ufufuo ulio bora;*

*Hapa* chini kabisa. Mnaona? [Ndugu Branham anarejea kwenye mchoro wake ubaoni — Mh.] Vema.

*Wengine walijaribiwa…dhihaka…mapigo, naam,…mafungo,…kwa kutiwa gerezani:*

*Walipigwa kwa mawe, wakakatwa kwa misumeno, walijaribiwa, waliuawa kwa mapanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi ya mbuzi; walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendwa mabaya;*

*(Ambaye ulimwengu haumstahili):* …

Mnaona, katika mabano hapo, unaona katika Biblia yako.

*…walikuwa wakizunguka-zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi.*

*…watu hawa wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao,…*

Hapa! [Ndugu Branham anarejea kwenye mchoro wake ubaoni — Mh.]

*…kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi;* (Unaona?)

*Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.*

142 Mnalipata? Watu hawa waliokufa, hapa, wanatutegemea na kutungojea sisi. Kwa hiyo, Kanisa *hili* halina budi kufikia ukamilifu, kusudi lipate kuleta ufufuo. Nao wako chini ya ninii, nafsi chini ya madhabahu, wakingojea Kanisa hili lifikie ukamilifu Wake, hapo ndipo Kristo atakapokuja.

Na Kanisa hili, unaona, linakuwa dogo zaidi, katika uchache. [Ndugu Branham anarejea kwenye mchoro wake ubaoni — Mh.] Limechongoka zaidi ya hapo, lakini ningetaka tu kuandika hilo pale, mnaona. Limefikia kwenye ncha ya sindano. Mpaka, Kanisa, katika uchache, halina budi kufikia mahali mpaka liwe na aina ya huduma ile ile ambayo *hili* liliacha, kwa sababu, wakati Jiwe hili la Kufunika litakaporudi ...

Lina kitu kama mfuko mdogo *hapa*, ambapo litaketi moja kwa moja pale, kwenye piramidi ya kawaida. Si kwamba ni kifuniko tu kinachokingama juu. Ni kilimi kidogo, na inabidi kuketi pale juu, maana kitiririsha maji.

Na kitakapokuja, Kanisa hili halina budi kuchongoka.

Haya yote, mawe mengine kwenye piramidi, yamewekwa kikamilifu sana hata huwezi kupenyeza wembe kati yao, yenye uzito wa tani nyingi, yamewekwa pale. Jinsi walivyoyafikisha kule juu, wao hawajui. Lakini yalijengwa.

Na *hapa* juu, Kifuniko cha piramidi kikija, piramidi Yenyewe, ule Mwili wa Kristo itabidi uchongoke. Si kanuni fulani tu za imani na mafundisho, ama kitu kingine tulichopitia. Itabidi liwe kama Kristo kabisa, mpaka, wakati Yeye atakapokuja, Yeye pamoja na huduma hiyo watafungamana pamoja kikamilifu. Mnaona? Ndipo Unyakuo utakapotokea, kule kwenda Nyumbani.

143 Angalia mahali tunapoishi sasa, katika Laodikia, ambapo kanisa lilikuwa na wakati mbaya kuliko nyakati zote za kanisa walizopata kuwa nazo. Katika Biblia, tunaona, ulikuwa ndio wakati pekee wa kanisa ambapo Mungu alikuwa nje ya kanisa, akipiga hodi, akijaribu kurudi kwenye jengo Lake mwenyewe. Kanuni za imani na madhehebu vilikuwa hata vimemfukuza kanisani Mwake mwenyewe. "Tazama, nasimama mlangoni na kubisha. Mtu akiwa na kiu na afunge mlango, nitaingia, na kula pamoja naye." Mnaona? Hii hapa, katika wakati *huu* wa kanisa. Hatua kwa hatua wakamtupa nje, mpaka kufikia *hapa* wakamfukuza kabisa. Hawataki uhusiano wo wote Naye.

Sasa mnaona leo mahali tunakoelekea. Hata wakati wa mwisho wa Kanisa la Laodikia umekuwa wa kawaida sana, mpaka huo pamoja na Ukatoliki, ambao uliuvunja papa hapa, zinakuja pamoja na kuungana kama kanisa moja kuu. Kukiweko na muungano wa makanisa, ni kitu kimoja na Ukatoliki.

144 Kuna tofauti moja tu, kama wanaweza tu kuisuluhisha hiyo, nayo ni kufanya ushirika. Hilo ndilo jambo pekee kwenye dayosisi, ambalo—ambalo—ambalo linazuia Ukatoliki na Uprotestanti kuungana, ni utaratibu wa ushirika. Kanisa Katoliki linasema, "Ni mwili." Na kanisa la Kiprotestanti linasema, "Unawakilisha mwili." Wakatoliki hufanya misa kutoka kwake. Misa ni, kwamba, wanafanya ushirika, wakitumaini wamesamehewa. Mprotestanti anaula kwa imani, akimshukuru Mungu, katika ushirika, ya kwamba wamesamehewa. Mprotestanti anasema, "Tumesamehewa." Mkatoliki anasema, "Tunatumaini tumesamehe." Misa na ushirika. Wao wanaiita misa; sisi tunauita ushirika. Misa ni kutumaini kwamba ndivyo ilivyo. Ushirika ni kujua ndivyo ilivyo, na kumshukuru Yeye kwa ajili ya jambo hilo. Mnaona? Na hilo ndilo jambo pekee ambalo hawawezi kukubaliana. Watakubaliana.

145 Loo, linaonekana ni jambo zuri sana. Itaungana, kuendeleza… Ita—itaendeleza ninii yote… Vema, Biblia ilisema, "Na mnyama huyu akampa yule kahaba nguvu zake," mnaona, wakaungana pamoja. Mnaona? Vile vile kabisa Biblia ilisema watafanya, wanafanya jambo hilo sasa. Linaendelea sasa hivi, juma lili hili. Si kwamba nina jambo lo lote dhidi ya Wakatoliki, si zaidi na Waprotestanti.

Enyi Wamethodisti na Wabaptisti, na wengi wenu ninyi enyi Wapentekoste, wakati makanisa yenu yameingia moja kwa moja katika muungano huu wa makanisa, huku wamejenga lile mochwari kubwa kule New York, la ule muungano wa makanisa, ni sawa na Umoja wa Mataifa na kadhalika. Wanajaribu

kuunganisha Uprotestanti wote pamoja.

Sasa, Wakatoliki wana busara kwa jambo hilo, na wataenda kumleta huyu Papa Yohana wa ishirini na tatu, ama ishirini na mbili, cho chote alicho. Yeye anakazana, katika njia nyenyekevu, na ya kujidhili, kuleta imani yote ya Kiprotestanti na ya Kikatoliki kuwa imani moja, vile vile hasa Biblia ilivyosema wangefanya. Haya basi. Nao Waprotestanti wakinaswa kabisa katika jambo hilo, ndoana, kamba, na kuzama.

Kwa nini? Kwa nini? Kwa sababu hawamiliki vitu *hivi*. *Maarifa*, "Neno ni kweli." *Subira*, "Wao wamngojeao Bwana." Mnaona ninalomaanisha?

146 Ni kama vile yule askofu wa Kimethodisti alivyosema hivi majuzi, walipopitisha mswada huo. Na kila mtu anajua jambo hilo, jinsi, kile kilichochochea jambo hilo, kujaribu kufanya sala fulani itakayosemwa kanisani, ama shuleni. Nao walitaka kuninii… Nafikiri ilikuwa ni kitabu cha sala cha Kipresbiteri, ama cho chote kile, nao wazazi wakashtaki shu—shu—shule kwa kuwa wasingekubali sala hii isemwe shuleni. Na askofu huyu wa Kimethodisti alikuwa ni mzee mwenye hekima, akasimama na kusema, "Hilo ni kosa." Kasema, "Linavunja katiba." Yeye alipata fununu yake juu ya jambo hilo. Akasema, "Kama vile katika kanisa letu la Kimethodisti," akasema, "katika kanisa letu la Kimethodisti," kasema, "wengi wa watu wetu daima wanazungumza juu ya kashfa ya Hollywood, na asilimia tisini na tano yao wanaenda kuiangalia hata hivyo."

Kuna nini? Waliacha hii. Hiyo ni kweli kabisa. Waliacha hilo.

147 Nilikuwa nikizungumza papa hapa katika chumba hiki, hivi majuzi, na a—a—afisa wa moja ya makanisa makubwa sana ya Kimethodisti yaliyopo kule Falls City, moja ya makanisa ya kiroho sana ya Kimethodisti katika Falls City. Nikaonesha, wakati wa Kimethodisti unaotangulia wakati wetu pale, wa Kipentekoste. Ndipo akasema, "Katika St Louis, Missouri, walifanya utafiti, yapata miezi mitatu ama minne iliyopita, na wakatambua." Mtu huyo huenda ameketi hapa asubuhi ya leo. Vema, yeye ni mkandarasi anayejenga hili, anayetujengea jengo hili. Methodisti ya Main Street, ambamo yeye hushiriki, ambako Ndugu Lum na hao wengine ndiye mchungaji. Kwa hiyo basi tunaona ya kwamba, katika jambo hilo, ya kwamba ninaamini ilikuwa asilimia sabini na kitu ya Wamethodisti katika ule utafiti, uchunguzi wa St. Louis, ulionesha ya kwamba asilimia sabini na kitu ya Wamethodisti walivuta sigara, na asilimia sitini na nane yao wanakunywa pombe. Mmethodisti! Na jambo la ajabu lilikuwa, wakati huo uchanganuzi ulipotolewa, ama makadirio kati ya wanaume na wanawake; wanawake, ilikuwa sabini, asilimia sabini na kitu, ukilinganisha na asilimia hamsini ya wanaume. Wanawake wengi zaidi wanavuta sigara na kunywa pombe kuliko wanaume. Asilimia sabini, asilimia sabini-na-kitu, wanawake zaidi ya wanaume.

148 Sasa vipi kama tungeenda kwenye Fundisho la Biblia la kuvaa suruali, na kukata nywele, na vitu kama hivyo, mnaona, ambapo utauwa, wanawake wanaokiri utauwa na utakatifu? Karamu za kadi na cho chote kile, wapiga domo, wapayukaji, wasioweza kunyamaza. Ndimi zao zinazungumza na kupiga domo, na kuzurura. Na wanaume je? Karamu za kadi, michezo ya gofu, huko nje wakiwa nusu uchi, wamevaa nguo fupi na chafu, huku wanawake wakirandaranda mitaani huko. Si ajabu!

Mnaona ujanja huo mchafu aliofanyiwa yule mhubiri, mhubiri wa jela, asubuhi ya leo? Naam, bwana. Siamini kwamba mtu huyo ana hatia ya jambo hilo. Ilifanya nini? Huyo ni Ndugu … Siwezi kukumbuka ninii yake… [Mtu fulani anasema, "Dan Gilbert." — Mh.] Naam. Dan Gilbert, mhubiri wa gerezani. Wakati mtu huyo alipoingia na kumwua Dan, hapa miezi michache iliyopita, na sasa mke wake atapata mtoto. Bila shaka, Dan amekufa, hawawezi kumpa mtoto damu sasa. Anasema Dan alimnajisi, na huyo ni ninii wake… "Huyo ni mtoto wa Dan." Kama ninii… Siamini jambo hilo zaidi ya nisivyoamini ya kwamba—ya kwamba—ya kwamba kunguru ana manyoya ya njiwa. La, bwana. Ninaamini ni uongo. Ninaamini Dan Gilbert alikuwa mtu wa Mungu. Nami ninaamini huo ni mpango wa ibilisi.

149 Ni kama kitu kile kinachojaribu kuwekwa juu ya hizo sala. Yule askofu mzee wa Kimethodisti—Methodist alikuwa mwerevu vya kutosha kugundua jambo hilo. Kama angalininii, kama mswada huo ungalipitishwa, huo ulikuwa umechochewa na kitu kingine. Hiyo ni kweli.

Ni kama tu shida hii ya ubaguzi huko Kusini, jambo lile lile. Ninaamini watu wanapaswa kuwa huru. Ninaamini taifa hili linatetea uhuru. Mimi simlaumu Bw. Kennedy kwa kuwatuma wanajeshi. Ingawaje, mimi si—si "mwenye mawazo mageni," wala mimi si Mdemokrati. Mimi si Mripablikani. Mimi ni Mkristo. Kwa hiyo ninaninii … Lakini mimi siamini jambo hilo. Wala siamini watu weusi wanapaswa kuuza haki yao ya mzaliwa wa kwanza kwa upuuzi kama huo. Ilikuwa—ilikuwa ni chama cha Ripablikani. Damu ya Abraham Lincoln iliwaweka watu hao huru kwa kuwa alikuwa ni mcha mungu. Nafikiri wanapaswa angaa kushikilia chama chao endapo kwa vyo vyote watapiga kura.

Lakini ninawaambia jambo moja, huyo mvulana hakuwa kule chini kwa sababu hiyo tu, shule yao. Mvulana huyo ni raia. Yeye ni Mmarekani. Huu ni uhuru kwa wote. Rangi ya mtu haipaswi kusababisha tofauti yake. Sisi sote … "Mungu," kasema, "kwa mtu mmoja, aliumba damu yote, mataifa yote." Sisi sote ni mmoja. Lakini, mvulana huyo, alikuwa askari. Yeye ni mwanajeshi mstaafu. Alipigania haki yake.

Alikuwa na haki ya kwenda shuleni. Hiyo ni kweli. Lakini alikuwa na shule nyingi sana angaliweza kwenda.

150 Ni kile jambo hilo lilicho. Kama ukilichunguza, ni upuuzi wa madhehebu haya ya kisasa kule, huo ndio unaochochea jambo hilo. Kwa nini? Wao wanachukua hizo kura za watu weusi kutoka kwa Ripablikan na kuzipeleka kwa Demokrati, na wanauza haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa jambo hilo. Ni kweli kabisa. Roho Mtakatifu hayupo hapa …

"Yeye aliye na hekima." "Yeye aliye na maarifa." Kweli kabisa. Ni kama tu kanisa hili, wakati huu wa sasa, lilivyojiuza lenyewe. Hivi hamwezi kuona kitakachotukia?

Sijali kama jambo hili linarekodiwa. Hili hapa linakuja. A-ha. Naam. Kuna nini? Mama yangu mzee alikuwa akisema, "Mpeni shetani haki yake."

Kuna mtu mmoja aliyefanya jambo pekee lililokuwa la busara, huyo alikuwa ni Castro kule chini. Naam, bwana. Alishuka akaenda kule. Na mabepari walikuwa na miwa yote na kila kitu... wao, iko kwenye mfumo wa dhahabu, kama vile Marekani. Angefanya nini? Alinunua hati hizo zote. Akapata pesa kwa njia yo yote aliyoweza. Alifanya nini basi? Alibuni pesa za bandia, na kuzibadilisha. Akazirudisha moja kwa moja. Hilo ndilo jambo pekee taifa hili lingeweza kufanya.

151 Je! hivi mlisikia *Life Line* hivi majuzi asubuhi? Mbona, mnajua, ni kama tu kuuza hati kwa dhahabu. Hizo hati tayari zimechukuliwa. Na serikali hii iliyopo sasa inatumia peza za nini? Pesa za kodi watakazokusanya miaka arobaini tangu sasa. Taifa limekwisha. Hilo ni *Life Line* moja kwa moja kutoka Washington D.C. kabisa, kote nchini. Kodi wanazotumia, na kujaribu kununua za kigeni. Vema, wao wanazitoa tu hata hivyo. Hivi hamwoni? Hivyo ndivyo—ndivyo hasa watakavyofanya. Mnaona? Ni kitu gani? Sasa, kama taifa hili likifilisika, jambo pekee linaloweza kufanya ni kufilisika. Jambo pekee linaloweza kufanya ni kufilisika.

Hilo ndilo jambo pekee la busara kufanya, kubadilisha sarafu. Lakini hawatafanya hivyo, chini ya utawala huu wa sasa. Kanisa Katoliki la Kirumi linamiliki dhahabu ya ulimwengu. Na jambo watakalofanya ni kujiuza, "Hawa matajiri," na kadhalika, "wa duniani," kama vile Biblia ilivyosema. Watafanya nini, kabla ya kupata hasara? Ile Kampuni ya Tumbaku ya Brown na Williamson, karibu yote ni Katoliki, hata hivyo. Na mambo haya mengine yote, watafanya nini? Watakubali jambo hilo, nao watachukua fedha kutoka Rumi, na ndipo limeuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Rumi inalisaidia. Naam, bwana. Italisaidia. Nao wanapata sera za kutosha sasa, wanajichukulia za kutosha, akiingiza baraza lake la mawaziri. Angalia kile Bw. Kennedy anachoomba.

152 Na wakati mnapoona jambo hili, hivi majuzi, hakuna haja ya kupiga kura tena. Kuna faida gani ya kupiga kura? Wakati, waliweka jambo hili gazetini, na kulithibitishia watu, nao wakakataa kufanya kitu juu yake. Ambapo, walithibitisha ya kwamba zile mashine kote nchini zilikuwa zimetegwa kijanja, hata wakamchagua Bw. Kennedy kwa kura ya uongo. Je! Biblia haisemi ya kwamba angeingia kwa udanganyifu? Bila shaka, uongo. Sasa, mimi sipingi chama cha Demokrati si zaidi ya vile ninavyopinga cha Ripablikani, lakini mimi ninatamka tu mambo ya kweli kutoka katika Biblia. Kuna faida gani ya kupiga kura? Wanajua ni nani anayeingia mle.

153 Ni wangapi wenu wanaokumbuka yale matangazo ya televisheni ambapo walikuwako na wanawake wawili waliosimama? Na mmoja akasema, "Nitampigia kura Bw…" Ama, mwanamke Mprotestanti alisema, "Nitampigia kura Bw. Kennedy."

Wakasema, "Kwa nini?"

Kasema, "Kwa sababu nafikiri yeye ni mtu mwerevu kuliko Bw.Nixon. Atakuwa Rais bora zaidi."

Ndipo akasema, "Huyu ni mwanamke Mkatoliki. 'Utampigia kura nani?'"

Akasema, "Mimi ni Mkatoliki, Mromani Katoliki, Mkatoliki mwaminifu." Akasema, "Nami nitampigia kura Bw.Nixon."

"Kwa nini?"

Akasema, "Kwa sababu, nafikiri Bw. Nixon atakuwa Rais bora kwa sababu yeye amezoea mambo hayo zaidi. Yeye anajua zaidi ukomunisti." Mwanamke huyo alisema uongo.

154 Nina *Ka*…wanachokiita, *Kanuni za Imani Yetu*, kitabu cha hali ya juu sana cha Kikatoliki kinachoweza kununuliwa. Nacho kinasema mle ndani, "Kama kuna Mkatoliki anayegombea kiti, anayeshindana na Mprotestanti; kama Mkatoliki akimpigia Mprotestanti kura, wanaondolewa katika ushirika wa kanisa Katoliki." Kweli. "Na endapo kuna Wakatoliki wawili wanaopigania kiti kimoja, watamchagua Mkatoliki aliyemwaminifu zaidi kwa 'kanisa mama' na kuwapigia kura."

155 Mnaona jinsi, huo undanganyifu, wanavyojaribu kufanya? Kutoa pesa, kununua. Kwa nini? Wao wanajaribu kulivunja. Nao wanafanya jambo hilo, nalo limefilisiki. Na ni kitu gani? Liko kwenye mfumo wa

dhahabu. Na kanisa Katoliki, ile serikali yao, linamiliki dhahabu ya ulimwengu. [Mtu fulani anasema, "Dola bilioni mia moja na sitini na nane."—Mh.] Bilioni mia moja na sitini na nane. Haya basi. Italirudisha moja kwa moja kwenye mfumo wa dhahabu, nanyi watu mtaweka nyumba zenu na kadhalika, lakini ninyi ni mali ya kanisa Katoliki. Taifa hili ni mali ya kanisa Katoliki. Kila kitu kimenaswa ndani yake moja kwa moja namna hiyo, kwa fedha zao. Je! Biblia haineni juu ya jambo hilo? Hiyo ndiyo picha ambayo Biblia inatuchorea.

Kile ninachojaribu kusema, leo, ndugu. Watasema, "Hilo litalifanya kanisa zuri. Utauunganisha Uprotestanti." Linaonekana ni zuri kwa macho ya kawaida, bali maarifa ya ulimwengu huu ni upumbavu kwa Mungu.

"Na ilimpendeza Mungu, kwa u—upuuzi wa kuhubiri, kuwaokoa wale wanaopotea, kwa huduma ya Kiungu aliyoiweka katika Kanisa Lake, kulijenga Kanisa juu ya sifa hizi za kiroho wala si juu ya kitu cho chote cha duniani."

156 Petro alisema, "Na kwa sababu mmeokolewa na upotovu wa ulimwengu kwa sababu ya tamaa ya pesa, na tamaa ya kujifurahisha, na anasa, na kula, na kunywa, na tamaa mbaya tulizo nazo. Mmeokolewa na hayo. Na sasa mmejengwa katika uzima. Ninaliambia Kanisa jambo hilo," akasema. Haya basi. Mlilisoma hilo? Mlilipata? Mlilisikia tulipolisoma hapa nyuma katika Petro wa Pili? Sikilizeni tu yale anayosema hapa, jinsi hilo lilivyoandikwa vizuri hapa, jinsi yeye a—anavyolielezea. Vema. Msikilizeni sasa anaponena. Vema.

> Petro, *Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika hali ya Mungu wetu, na Mwokozi Yesu Kristo.*
>
> *…amani i—ongezwe kwenu katika kumjua Mungu na katika Yesu Kristo Bwana wetu.*
>
> Kwa kuwa—kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote…

Ni nani atakayeirithi nchi na vitu vyote? [Mtu fulani anasema, "Watakatifu." — Mh.] Hakika. "Vipasavyo…" Naam. Vema.

> *…vinavyopasa uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake* hata utukufu
>
> *Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, ya thamani: ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu* (Sikilizeni hilo) *uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.*

157 Tamaa ya pesa, tamaa ya mambo makubwa, tamaa ya kujulikana na watu, mambo haya ni mafu kwa mwamini. Hatujali. Hema ama kibanda, kwa nini nijali; niishi au nife, nizame au nife maji? Jambo hili ndilo ninalotaka, Ufalme wa Mungu. Kama ninatunza nyumba yangu, kama ninaitunza familia yangu, kama ninatunza cho chote kile, hebu na nidumu na Kristo, tumaini la Utukufu.

Nijenge, Ee Bwana, katika *Hiki*. Kristo na awe ndiye Kiongozi wangu, kwamba atende kazi kupitia kwangu. Juu ya msingi wangu, imani yangu iliyo ndani Yake, jalia nguvu, maarifa, kiasi, saburi, utauwa, na upendano wa ndugu, vitende kazi ndani yangu, Ee Bwana, ndilo ombi langu. Sijali; niishi au nife, nizame au nife maji; madheheubu, bila madhehebu; rafiki ama pasipo na rafiki. Hebu Hilo na litende kazi ndani yangu, jalia nguvu za Kristo, maarifa Yake, yamiminike, ili niweze kuwafundisha hao.

"Kwa maana Mungu ameweka katika Kanisa, mitume, manabii, waalimu, wachungaji, na wainjilisti, wote kwa ajili ya kukamilisha na kuingiza sifa hizi zote ndani yake, kwa ajili ya ule ukamilifu wa Kuja kwa Mwana wa Mungu." Kila moja ya mawe haya ni vifaa zilizotolewa kwa Huyo. *Hiki* ni kifaa cha Huyu. Kila moja ya sifa hizi ni Zake, nazo zinatiririka kutoka Kwake, kupitia kwazo. Amina.

158 Saa sita kamili. Yote yanaenda wapi? Amina. Je! Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnaamini jambo hilo? ["Amina."] Sikilizeni, enyi watoto wadogo.

Dada Kidd alisema, asubuhi ya leo, "Ndugu Bill, sijui kama nitakuona tena." Hilo karibu liniue. Mnaona? Yeye anafikiri anakuwa mzee, naye anazeeka. Nilimwomba Mungu amjalie yeye pamoja na Ndugu Kidd, maisha marefu.

Hebu niwaambieni, hatujui tutakuwa pamoja kwa muda gani. Sijui nitakuwa pamoja nanyi kwa muda gani. Mungu anaweza kuniita niondoke ulimwenguni. Anaweza kuniita kwenye uwanja mwingine wa huduma. Anaweza kukuita mahali fulani. Hatujui. Lakini, hebu—hebu tupate. Hebu tusiache jambo hili litupite tu. Hebu na tuchukue jambo hilo.

Hilo hapo, katika Biblia. Hili hapa, linafananisha kila kitu kingine. Na laiti ningalikuwa na wakati wa kufanya jambo hilo! Huwezi kufanya jambo hilo katika siku moja. Unajua jambo hilo. Lakini, anaweza kuunganisha kitu hicho chote pamoja!

Angalieni, tulipomaliza ujumbe huo pale, mnaona kile Roho Mtakatifu alifanya pale ukutani, sivyo? Ni wangapi waliokuwa hapa wakati huo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Mnaona? Hakika! Akashuka akaja moja kwa moja, akachora kitu kile kile, huyo Malaika wa Bwana.

159 Mnaona, ni kweli. Usiache likupite. Lishikilieni, enyi watoto. Shikilia hilo. Kumbukeni, jengeni katika imani yenu, nguvu, maarifa, saburi!

Sasa, hapa, nafikiri nilikuwa na kipande cha karatasi hapa, kama sijakiangusha mahali fulani wakati nilipokuwa nikihubiri. Hiki papa hapa. Asante, ndugu. Asanteni, sana. Kama ukitaka ku—kukiangalia, uone kama kuna jambo fulani hapa ambalo ungeweza kuninii… Labda ni mchoro ulio bora zaidi ya huo pale, ambapo unaweza kunakili kutoka kwenye huu. Nitakibandika tu hapa juu, na bila shaka unaweza ukakiangalia na—na kuunakili.

160 Nami nawatakeni muuchore na muusome, na kuulinganisha, na kisha muutekeleze. Msiusome tu, kuulinganisha, bali utekelezeni mtakapofanya hivyo. Upokee kwa uaminifu ndani yako. Usiseme, "Vema, nilifurahia kuusikiliza." Nilifanya hivyo, pia. Lakini kuusikiliza, na kisha kuupokea, ni tofauti. Mnaona? Mnaona? Ni tofauti. Mnaona?

Kuna sifa saba za kufanya kimo cha Mungu. Kuna Nyakati Saba za Kanisa, ambapo Mungu amelileta Kanisa kwenye sifa hizi. Naye amekuwa na wajumbe saba wa kufanya jambo hilo. Kuna saba, saba, saba. Mnaona? Saba ni—ni nambari ya Mungu ya ukamilisho, na tatu ni nambari ya Mungu ya ukamilifu. Kwa hiyo, kuna tatu, na saba tatu. Kwa hiyo, kimahesabu, kiroho, kwa Neno, kwa ushuhuda wa Roho Mtakatifu, yote yamekamilisha jambo hilo pamoja. Hebu na tulisome.

161 Hebu na tuongeze kwenye imani yetu mambo haya, halafu, tupate kufikia kimo kikamilifu cha Kristo; tukiunganishwa pamoja kwa upendo wa kiungu, kumcha Mungu, uchaji moyoni mwetu sisi kwa sisi, kuheshimiana sana sisi kwa sisi, kupendana kwa ndugu na kupendana kwa dada, bila utovu wa adabu, bila kitu ila usafi wa maisha ya Roho Mtakatifu. Mnaona? Kuishi pamoja, uwe Mkristo. Enenda kwa imani. Hebu nguvu wa Mungu na utiririke kupitia ndani yako; hebu maarifa ya Mungu, inapofikia kwenye mema na mabaya. Shetani anapoleta jambo ambalo si la Kimaandiko kabisa, achana nalo. Hiyo ni kweli.

162 Ninaweza kuwazia hao mitume hawakutenda kama sisi. Walienda kila mahali, labda ni watu wa maneno machache, mpaka walipoingia mimbarani. Waliingia na kufanya waliyopaswa kufanya, kisha wakatoka. Naam, bwana. Walikuwa na nguvu. Walikuwa na nguvu. Hawakubishana na watu. Wanajua mahali waliposimama. Hivyo tu. Walimjua Yeye waliyemwamini. Waliendelea kutembea katika Roho. Kufanya tu …

Kama tu nilivyosema hivi majuzi usiku. Ishara moja ndogo ya kichwa, hivyo tu ndivyo Mungu angefanya, basi hakuna kitu kingaliwazuia. Wao hawakuuliza swali wala kulichunguza, wala kusitasita na kutilia wasiwasi kama tunavyofanya, kama wangepaswa kufanya jambo *hili* ama *lile*. Waliondoka kwenda zao na kulitenda, hata hivyo. Ishara moja ndogo tu kwa kichwa kutoka kwa Mungu, hilo lilitosha, upesi sana. Kwa nini? Wangejuaje ilikuwa ni ishara kutoka kwa Mungu? Wao walikuwa na sifa hizi zote hapa ndani, sifa hizi zote. Na kibali kidogo cha kwanza cha Mungu kililingana na kila kipengele cha moja ya *hizi*, na pamoja na Neno Lake. Wao walijua ilikuwa ni Neno la Mungu, na haoo wameenda zao. Hawakuona wasiwasi juu ya jambo lo lote lile. Wakati Mungu aliponena, wao waliondoka. Tunanena …

163 Mungu anazungumza na sisi, na sisi tutasema, "Vema, tutaenda. Tutaona kama tunaweza kuishi Maisha haya." Jambo la kwanza unajua, mtu fulani anakukasirisha. Vema, hakika, huyo ni ibilisi.

Laiti mngalimwona akijaribu kunifanya nisije kwenye mkutano huu asubuhi ya leo. Mnapaswa kuwa na jambo hilo wakati mmoja. Loo, rehema! Sina budi kupigana kila ninapotaja mkutano. Na kama ninaenda kumwombea mgonjwa, na mtu fulani anakufa na hajaokoka, kutakuwako na simu thelathini zitakazopigwa katika dakika kumi, kama zinaweza kuingia upesi namna hiyo, kunizuia nisiende. "Loo, Ndugu Branham, huna budi kufanya jambo *hili*." Lakini kuna nafsi iliyo hatarini. Hakika. Naam.

164 Usiku mwingine, niliitwa mahali fulani. Kijana mmoja, nilizungumza naye hapa chini katika kile unachoita, maduka makubwa, miaka michache iliyopita. Alikuwa mlevi wa kupindukia. Nilimjua mvulana huyo, mvulana mzuri sana, bali alikuwa ni mwenye dhambi. Na kwa hiyo mama yake akapiga simu. Nafikiri alimwita Doc mara kadhaa. Mimi … Wakampigia, pia wakampigia simu Billy, na—na hatimaye nikaupata huo ujumbe. Na nilipopata ujumbe huo, jamani, sijapata kuwa na vita vikali namna hiyo maishani mwangu, kumwendea mvulana huyo.

Na nilipofika kule, maskini jamaa huyo alikuwa hanitambui tena. Huyo hapo, amelala pale, amepoteza fahamu, na anaendelea tu. Baba yake akijaribu kumpapasa, na kusema, "Mpenzi." Na mtu huyo ana umri wa miaka hamsini, miaka hamsini na moja hivi. Na kusema, "Mpenzi," *huyu*, "natulia basi." Naye alikuwa akijaribu kuamka. Maskini mikono yake iliyokonda ni mikubwa *hivi*. Mvulana huyo alikuwa na saratani nyingi sana mpaka hakuwa kitu ila saratani tupu. Viungo vyote vya mwili wake vilikuwa na saratani. Hata damu yake ilikuwa saratani, kila kitu. Naye huyo hapo, akijaribu kuinuka, na akiendelea namna hiyo.

165 Nikamshika mkono, nikasema, "Woodrow, Woodrow, huyu ni Ndugu Branham."

Baba yake akasema, "Hivi hujui? Huyu ni Ndugu Bill. Woodrow, huyu ni Ndugu Bill."

Akasema, "A-ha. A-ha. A-ha a-ha." Kama hivyo.

Ndipo baba yake akaangalia na kusema, "Billy, umechelewa kidogo."

Nikasema, "Kamwe sijachelewa sana. Yuko hapa." Nimekuwa na vita.

Na halafu hao wavulana wengine, wavulana wengine zaidi, wenye dhambi, walikuwa wamesimama pale, baadhi ya jamaa zake. Nikasema, "Mnaona, enyi vijana, jiandaeni, maana mtakuja mahali hapa. Hamna budi mshuke mje chini hapa. Mnaona? Labda si kwa saratani hii—hii. Huenda mkaja na jambo lingine, huko barabara kuu, mkitokwa na damu vibaya sana, ama cho chote kile. Hamna budi kufikia mahali hapo." Tulizungumza nao.

Nilikuwa nikingojea kuona kile Roho atakachosema nifanye. Kungoja. Muda si muda unajua, nilihisi kile kibali kidogo cha kichwa. "Mwekee mikono."

Nilitembea huku na huko, nikasema, "Nyote inamisheni vichwa vyenu." Wote waliinamisha vichwa vyao, vijana wawili ama watatu mle ndani.

Nikaweka mikono yangu juu yake. Nikasema, "Bwana Mungu, jalia mvulana huyu apate fahamu za kujua atakayofanya, kabla hajakutana na jambo hili. Yeye anakufa. Ibilisi huyu amemjerui, naye anaenda. Naye amekunywa pombe mpaka anataka kufa, na huyu hapa katika hali hii. Ninaomba Wewe umrehemu." Na nilipomwombea, asubuhi iliyofuatia alikuwa ameketi chini, akizungumza na baba yake.

166 Busty Rogers, ambaye … Waliniita hapa chini hospitalini, si muda mrefu uliopita. Nilikuwa huko nje siku hiyo, baada ya kuhubiri kule Milltown ambako Georgie Carter mdogo aliponywa. Ninyi nyote mnakumbuka hilo. Na hapo ambapo Ndugu Smith, mhubiri wa Kimethodisti, aliposema, "Kama mtu ye yote akibatizwa, katika Jina la Yesu Kristo, atoke hemani mwangu," namna hiyo. Huko juu kwenye kivuko cha Totten, nikifanya mkutano huo kule. Na, loo, akanilaani kwa kila kitu ungaliweza kuwazia. Sikusema neno; nikaendelea moja kwa moja. Nilikuwa na agizo. Bwana alinionesha ono. Kulikuwako na mwana-kondoo kule, amenaswa mahali fulani huko nyikani. Nyote mnakumbuka lile ono, ninyi nyote. Nadhani mnakumbuka. Mnalikumbuka hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Hakika. Vema. Ndipo nilikuwa nikishuka kwenda msituni sehemu zile, nikimtafuta.

167 Nilienda kwenye kivuko cha Totten. Ndugu Wright pale anajua. Tulienda kule, hatukujua la kufanya. Nikanunua kikasha kidogo cha sabuni, kwa hela moja. Nilikuwa niende kule nje, nisimame kule na kuhubiri kwenye kipandio. Yeye akasema angepanda aende kule, juu ya kilima, akafanye biashara kidogo. Nilienda pamoja naye. Kulikuwako na kanisa kubwa la kale la Kibaptisti lililoketi pale, tupu. Bwana akaniambia, "Simama hapo."

Nikasema, "Hebu nishushe papa hapa, Ndugu Wright." Nikasimama. Yeye akaenda zake kule juu kisha akarudi.

Nilienda kule, na sikuweza kuufungua mlango. Nikasema, "Bwana, kama Wewe uko kwenye jambo hili, unataka mimi niingie kanisani, nifungulie mlango." Niliketi pale na nilikuwa nikiwazia.

Nikasikia mtu fulani akija; akaja, naye akasema, "U hali gani? Nitakwambia," kasema, "unataka kuingia kanisani?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Nina ufunguo hapa."

Nikaanza mkutano. Juma la kwanza, karibu hakukuwa na mtu hata. Usiku wa kwanza, nilikuwa na kusanyiko, Ndugu Wright na familia yake. Muda si muda unajua, mwishoni mwa juma hilo, hata hawakuweza kupata nafasi ya kusimama kwenye uwanja, ilikuwa ni vigumu. Bado mwana-kondoo huyo hakuwa ametokea. Ndugu Hall aliokolewa katika wakati huo, mchungaji wa kule hivi sasa, hao wote. Sikuweza kuona mahali alipokuwa huyu mwana-kondoo. Baada ya kitambo kidogo, kwenye kanisa la Kristo, kule chini ya kilima, maskini mscichana huyo miaka tisa na miezi minane hakupata kusogea, amelala pale. Huyo hapo. Nyote mnajua hadithi hiyo. Naam, bwana.

168 Alasiri hiyo wakati Busty Rogers, lile pandikizi la mwanajeshi mstaafu limesimama pale… Nikaenda kule. Na hapo lilisimama kusanyiko la Ndugu Smith ili kunicheka, kunidhihaki, kwa kubatiza eti katika Jina la Yesu. Nikatoka kwenye maji yenye matope ya kivuko cha miguu cha Totten, ambako walikuwa na ninii… [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] … kijito kidogo pale, nacho kinanguruma sana kiwezavyo. Mashemasi wachache wakaambatana nami.

Nikasema, "Nasimama hapa alasiri ya leo kuwakilisha Maandiko Matakatifu ya Mungu." Nikasema,

"Ninasoma kwenye Biblia hapa ambapo Petro alisema, 'Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu.'" Nikageuka, nikampa mmoja wa mashemasi Kitabu hicho.

169 Nikatoka kwenda kule, ndipo nikasema, "Ye yote atakaye, anayetubu dhambi zake, anaruhusiwa kuja." Nikaingia majini. Nikasema, "Inaonekana kwangu kwamba Malaika wameketi kwenye kila tawi sasa, wakiangalia." Loo, jamani! Hata yapata wakati ilipofikia kubatiza wawili ama watatu, kusanyiko lake lote, hao wanawake waliokuwa wamevaa nguo nzuri za hariri, walijitumbukiza majini, wakipaza sauti kwa nguvu. Nikabatisa kusanyiko lake lote katika Jina la Yesu Kristo. Mnajua jambo hilo. Nina picha yake. Ilikuwa hapo.

Ilikuwa ni kitu gani? Kutia kwenye wema wako. Mnaona? Liache tu. Mungu anajua jinsi ya kufanya jambo hilo. Mungu anajua jinsi ya kuyatimiza mambo haya. Acha waseme watakavyo. Haileti tofauti yoyote. Endeleeni tu kusonga mbele.

Busty Rogers akisimama pale, alipoona jambo hilo, akasema, "Basi ninaamini hilo kwa moyo wangu wote." Naye huyoo akaja majini, akiwa amevaa nguo zake nzuri, naye akabatizwa katika Jina la Yesu Kristo.

170 Yapata miaka mitatu ama minne iliyopita, waliniita hapa nishuke hospitalini kule New Albany. Huyo hapo, anakufa, kwa saratani, ailikuwa imemla kabisa. Madaktari walimpa kuishi mpaka kesho yake asubuhi. Wakasema, "Yuafa sasa." Wakasema, "Fika mara moja."

Nilishuka nikaenda kwenye chumba hicho, nilipofika humo, nikasimama pale na kuomba. Yeye akasema, "Billy, kuna upinde wa mvua unaozunguka ile kona pale."

Ndipo nikageuka, kuangalia. Nikasema, "Busty, ni agano. Hutakufa. Agano la Damu linakuokoa."

Nikaweka mikono yangu juu yake, nikasema, "Bwana Mungu, jinsi lile ono kule ambalo linathibitisha ya kwamba Wewe uko hapa. Agano lako ni kwamba, hili, 'Kwa mapigo Yake sisi tumeponywa.'" Nikamwekea mikono, na hapo akawa mzima. Wakamrudisha nyumbani.

171 Na yapata miaka minne ama mitano, yapata miaka minne, nikivua samaki hu—huku na huku mtoni na kila kitu, nikiendelea kufanya hivyo. Na pale ambapo saratani ilikuwa kwenye umio la tumbo, pamefanywa pagumu, kulikuwa na kifundo kikubwa kigumu. Madaktari, mabingwa wa hospitalini, walimwambia ya kwamba walikuwa na matibabu ya kobalti ambayo yangelinyosha hilo, yaruhusu chakula zaidi kwa wakati mmoja. Alikuwa na wakati mgumu kumeza chakula kingi, ilibidi ale pole pole sana. Alienda kule kufanyiwa matibabu hayo. Sikujua alikuwa kule.

Ndipo walipomfanyia upasuaji, waliona ya kwamba jambo hilo lilimtia kifafa, naye akapooza. Akalemaa upande mmoja namna hiyo. Na jambo pekee ambalo angeweza kufanya ni kulia tu nusu. Ndipo akachukua penseli, namna hiyo, na kufanya, "a-ha, a-ha, a-ha." Naye akajaribu kuandika, akitetemeka namna hiyo, kwa mkono wake mzima. Mkono wake wa kushoto, ulipooza. Na kupunga mkono wake, "Yesu anaokoa, 1900 na kitu." Hawakuweza kulipata.

Kwa hiyo wakati mke wake aliposema, "Ndugu Branham, sijui analomaanisha kwa jambo hilo."

Nikasema, "Bibi Rogers, analomaanisha, ilikuwa ni mwaka wa 1900 na kitu, naye aliokolewa na kubatizwa katika Jina la Yesu chini kule. Hilo ndilo linalomsaidia sasa. Yeye haogopi kufa."

Nikasema, "Bwana Mungu, mhurumie maisha yake. Ninaomba hilo, katika Jina la Yesu, ya kwamba Wewe utayahurumia maisha yake." Nikaweka mikono yangu juu yake. Kile kiharusi kikamwacha. Kifafa kikakoma. Naye akainuka kitandani. Naye amepata afya sasa, anatoa ushuhuda.

172 Tia kwenye imani yako, nguvu; tia kwenye wema wako, maarifa; katika maarifa yako, kiasi; katika kiasi chao, saburi; katika saburi yako, utauwa; katika utauwa wako, upendano wa ndugu; katika upendano wako wa ndugu, Roho Mtakatifu, na ndipo Kristo atakuja. Maana, chini Yake tu… Roho Mtakatifu ni Roho wa Yesu Kristo ndani ya Kanisa, kudhihirisha zile nguvu. Loo, jamani!

Hii hapa ni, saa sita na robo.
Nampenda … nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza,

Huku chini kabisa, kabla hakuwa cho chote.
Na kunini- … (Yeye alifanya nini?) … wokovu wangu
Mtini Kalvari.

*Hili* nikoje? Kwa sababu Yeye alinipenda, kwanza.
Nampenda, nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza … (Hicho hapo chanzo.)
Na akanunua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

173 Ninaahidi, asubuhi ya leo, Kwake, kwa moyo wangu wote, ya kwamba, kwa msaada Wake na kwa neema Yake, ninaomba ya kwamba nitaomba kila siku, bila kukoma, mpaka nitakapojisikia kila moja ya mahitaji haya yakitiririka katika umbo hili langu dogo la kale, mpaka niweze kuwa udhihirisho wa Kristo aliye hai. Kwa kuwa, Yeye alifanyika dhambi kama mimi, kusudi nipate kuwa … haki ya Mungu, kama Yeye. "Yeye alipachukua mahali pangu; Bwana, hebu nipachukue mahali Pake sasa." Kwa sababu, hilo ndilo kusudi alilolifia. Ni wangapi watakaoahidi jambo lhilo hilo, kwa neema ya Mungu? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa, na mikono yetu imeinuliwa juu. "Mimi …"

Ninaahidi hilo, Bwana, kanisa hili linaahidi hilo, "Kimo kikamilifu cha Yesu Kristo!"

Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na akanunua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7